Jumatano Julai 3, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579960
www.ippmedia.com
twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Samia akemea Tanzania kuwa dampo bidhaa feki

UKURASA 2


DRC na 'safari ya matumaini' kujiunga na EAC
Ukurasa 18
Ukurasa 15
Dk. Bashiru anapowachoka wenye uchu mali za chama
siasa
JUMATANO JULAI 3, 2019
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Ukurasa 20
Mkutano wa amani Bahrain, Kushner kafaulu au kawama?
BAADA YA MIAKA 55
Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-3
MZEE Pius Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia ni mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.
Vilevile, Mzee Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.
Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu la kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa.
Wiki iliyopita tuliwaletea sehemu ya pili ya mfululizo wa kitabu hiki ambapo tulijishia kipengele cha 2.2 Haja ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hizi mbili. Sasa fuatilia kuanzia kipengele kinachofuata:
2.3. Kuimarisha udugu wa karibu uliokuwapo baina ya wananchi wa nchi hizo mbili
Tukirejea hotuba ya Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokuwa akiwahutubia wabunge
INAENDELEA UK.16
Mzee Pius Msekwa. PICHA: MTANDAO
Ukurasa 14
Homa ya uchaguzi yachanganya wabunge katika nchi ya Kenya
Rwanda, Uganda zinavyotishia amani, utengamano wa EAC Ukurasa 19

UKURASA 13

# Familia yaanika mambo mazito



• **Ni** ya Tundu Lissu, yabainisha kutuma barua 11 ofisi ya Bunge, mwenyewe afunguka... *Ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**MAPYA KESI YA MEMBE DHIDI YA CYPRIAN MUSIBA**
MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imekubali ombi la kuongezewa muda...

UKURASA WA 4
**BIL. 114/- KUZALISHA MAJI DAR NA PWANI**
MAMLAKA ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), imesaini mikataba...

UKURASA WA 26
**ALIYEDAIWA KUTEKWA DAR AKUTWA MOMBASA**
MFANYABIASHARA wa Kenya, Raphael Ongangi anayedaiwa kutekwa nyara...


## Mdandia ndege akutwa amekufa

UKURASA 25



UKURASA 2

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipokea ujumbe maalum wa Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya kwa niaba ya Rais John Magufuli, kutoka kwa Balozi wa Kenya nchini, Dany Kazungu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

# Kenyatta amtumia JPM ujumbe kauli ya Jaguar

**MICHEZO** **STARS KUREJEA KESHO, KUIVAA SUDAN** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia akemea Tanzania kuwa dampo bidhaa feki

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameonya Tanzania kuwa dampo la bidhaa hafifu huku akisisitiza kuwa serikali haitakubali kuruhusu bidhaa za nje zisizo na ubora kuingia nchini.

Samia alisema hayo jana wakati akifungua Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea katika Viwanja vya Maonyesho ya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Ili kuhakikisha mianya inazibwa, aliiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara kudhibiti kuingia kwa bidhaa zisizo na ubora kutoka nje ili kuzipa nafasi bidhaa za ndani.

Alisema ni vyema ikahakikisha bidhaa zinazotoka nje zinakuwa zenye ubora tu ambazo zina uwezo wa kuleta changamoto kwa bidhaa za ndani.

"Viwanda vya ndani vina uwezo wa kuzalisha bidhaa bora zinazokidhi mahitaji ya soko la ndani, lakini changamoto ni kuwapo kasumba ya Watanzania kupenda kutumia bidhaa za nje kuliko za ndani ilhali bidhaa zetu zina ubora unaojitosheleza," alisema.

"Tunachotaka ni kuhakikisha Wizara ya Viwanda (na Biashara) inasimamia wazalishaji kuongeza thamani na kuboresha zaidi bidhaa zetu kuwa za kisasa ili ziuzwe na nje."

Alisema baada ya bidhaa kuongezewa thamani, balozi za Tanzania nje ya nchi zitapata kazi ya kutafuta masoko.

Samia pia aliziagiza mamlaka zinazohusika na upatikanaji wa malighafi kuhakikisha

INAENDELEA UK. 8

## UBUNGE WA LISSU:

# Familia yaeleza kutuma barua 11

**Na Enock Charles**

FAMILIA ya aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, imeweka bayana mawasiliano ya barua 11 walizoiandikia Ofisi ya Spika kuhusu hali ya kiongozi huyo anayeendelea na matibabu nchini Ubelgiji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowekwa kwenye moja ya blog, kaka yake Lissu, Wakili Alute Munghwai, alisema kauli ya Spika Job Ndugai kuwa hakuna mawasiliano yoyote kuhusu mbunge huyo siyo ya kweli, kwa kuwa mawasiliano yalifanyika kila wakati.

"Mwaka juzi na mwaka jana niliwasiliana na Ofisi ya Bunge kwa jumla ya barua 11 zilizoeleza suala la afya ya Lissu na alipopelekwa Ubelgiji vilevile tuliwataarifu na walijibu," alisema Munghwai.

Alisema Januari 10, mwaka jana, Ofisi ya Bunge ilimwandikia barua ikimtaarifu kuhusu kuteuliwa kwa madaktari bingwa watatu toka Hospitali ya Muhimbili ambao wangekwenda jijini Nairobi, kuchunguza afya ya Lissu na kuombwa kutoa ushirikiano.

"Nilijibu hii barua kwamba mgonjwa hayupo tena Nairobi, yupo

INAENDELEA UK. 8




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akionyesha cheti baada ya kukabidhiwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, wakati wa hafla ya maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma iliyofanyika Kikwajuni Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

**alkhalij enterprises Limited**

**JOB OPENING**

**SALES EXECUTIVE**

**Roles and Responsibilities:**

- Present and sell the Company's products and solutions to new and existing accounts
- Accountable for ensuring timely communication and customer satisfaction at assigned accounts
- Understand each customer's business and technical applications, anticipating their needs for products and solutions
- Establish and strengthen individual relationships within purchase, maintenance, and operations departments at assigned accounts
- Identify and analyze key opportunities and threats as it relates to products, markets, and competitors
- Prepare weekly and monthly reports on customer visits, significant quotations, and overall sales activity
- Achieve the allocated sales target for assigned accounts and new business

**Requirements:**

- A degree from a reputable academic institution
- Minimum 2-3 years' sales experience related to products
- Effective communication skills and an ability to build and sustain strong customer relationships
- English proficiency is a must
- Willing to work in Dar es Salaam, Tanzania and travel to other cities

To apply, please send your CV to careers@alkhalij.com

115289902

# Kenyatta amweleza JPM kukerwa kauli ya Jaguar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, amemtumia ujumbe maalumu Rais John Magufuli unaoelezea msimamo wa serikali yake, kuhusu kukerwa na matamshi yaliyotolewa hivi karibuni na Mbunge wa Jimbo la Starehe, Charles Njagua Kanyi maarufu kwa jina la Jaguar.

Ujumbe huo wa maandishi uliwasilishwa jana na Balozi wa Kenya nchini, Dany Kazungu, na kupokelewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa niaba ya Rais Magufuli, ofisini kwa Waziri Mkuu jijini Dar es Salaam.

Akipokea taarifa hiyo Waziri Mkuu alisema Watanzania wamefurahishwa na hatua mbalimbali zilizochukulia na Serikali ya Kenya dhidi ya mbunge huyo zinazodhihirisha kwamba matamshi hayo hayakuwa msimamo wa Serikali ya Kenya wala wananchi wake, bali ulikuwa ni msimamo binafsi wa mbunge huyo.

Amesema siku zote Watanzania na Wakenya wamekuwa huru kuishi na kufanya kazi au biashara katika nchi za Afrika ya Mashariki na pale yalipotokea matatizo au kutokukubaliana na serikali husika zilikaa mezani na kumaliza tofauti hizo. "Uhusiano kati ya Kenya na Tanzania ni wa karibu mno na wa kidugu kwani kuna baadhi ya makabila yapo katika nchi mbili hizi kama vile Wamasai na Wakurya na Wajaluo, hivyo ushirikiano katika masuala ya mbalimbali yakiwamo ya kibiashara na ya kijamii haukwepeki." Hivyo, Waziri Mkuu alitoa wito kwa viongozi na wananchi wa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kujiepusha na kauli zenye viashiria vya kujenga chuki, uhasama na migongano miongoni mwa wananchi kwani kauli hizo zisipodhibitiwa mapema zinaweza kusababisha hofu na kutokuelewana miongoni mwao.

Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuwasihi Watanzania kuendelea kuishi kwa amani na upendo na ndugu zao wa Kenya na wageni wote kutoka nchi za Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla ambao wapo nchini wakifanya shughuli mbalimbali kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Mambo yetu yote katika nchi za Afrika Mashariki hasa ya biashara na ya kiuchumi kwa ujumla yataenda vizuri endapo tutalinda na kudumisha amani, bila amani tutaogopana na tutashindwa kabisa kushirikiana," amesisitiza Mheshimiwa Majaliwa.

Waziri Mkuu aliahidi kuwa Serikali ya Tanzania kamwe haitaruhusu wala kufumbia macho kauli au vitendo vyovyote vyenye viashiria vya uchochezi dhidi ya nchi jirani ili kulinda na kuunga mkono juhudi mbalimbali za ushirikiano wa kisiasa na kiuchumi zinazofanywa na viongozi wakuu wa mataifa ya Afrika.

Kwa upande wake Balozi Kazungu alimshukuru Waziri Mkuu kwa kauli yake aliyoitoa bungeni jijini Dodoma, iliyowataka Watanzania kuwa watulivu na wayachukulie matamshi ya Mbunge wa Jimbo la Starehe nchini Kenya, Njagua kuwa ni msimamo wake binafsi na siyo msimamo wa Wakenya na serikali yao. Balozi Kazungu alisema msimamo wa Rais Kenyatta siku zote umekuwa ni kuwapokea na kuwakubali ndugu zao wote wanaotoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walioamua kuishi au kufanya biashara nchini Kenya.

Mwanzoni mwa wiki iliyopita, Njagua alitoa matamshi ya kichochezi akiwataka raia wa kigeni kutoka mataifa mbalimbali wanaofanya shughuli za kibiashara nchini Kenya wakiwamo Watanzania waondoke ndani ya saa 24.

**HABARI KITAIFA**

# Kesi ya Membe dhidi ya Musiba, Agosti 6

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekubali ombi la kuongezewa muda walalamikiwa Cyprian Musiba, Mhariri wa gazeti la Tanzanite na Mchapishaji wake kuwasilisha majibu katika kesi ya madai ya fidia ya Sh.bilioni 10 iliyofunguliwa ba Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Bernad Membe.

Kadhalika, mahakama hiyo imetoa siku saba kwa walalamikiwa kuwasilisha majibu ya maombi hayo ndani ya siku saba na kwamba mlalamikaji kama atakuwa na cha kujibu afanye hivyo kabla ya Agosti 6, mwaka huu kesi ya msingi itakaposikilizwa.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Joaquine Demelo, baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili kuhusu walalamikiwa kuongezewa muda wa kuwasilisha majibu ya maombi ya Membe badala ya upande mmoja.

Jaji alisema mahakama yake imekubali maombi ya walalamikiwa kuwasilisha majibu nje ya muda na kesi ya msingi itasikilizwa Agosti 6, mwaka huu.

"Lazima pande zote zisikilizwe ijulikane haki ni ya nani, tutasikiliza kesi ya msingi Agosti 6, mwaka huu, walalamikiwa wawasilishe majibu ya maombi ya msingi ndani ya siku saba," alisema Jaji Demelo.

Katika kesi ya msingi, Musiba anadaiwa kumtuhumu na kumkashifu Membe kuwa anamhujumu Rais Dk. John Magufuli na kwamba mbinu mojawapo ya kukamilisha hujuma hizo ni maandalizi kampeni za kugombea urais 2020.

# Polisi wasaka wauaji wa Watanzania Msumbiji

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi la Msumbiji, wanawasaka watu waliohusika na mauaji ya Watanzania tisa waliopigwa risasi na watu wasiojulikana nchini humo.

Katika mauaji hayo yaliyotokea wiki moja iliyopita nchini Msumbiji, wako pia raia wawili wa Msumbiji ambao wote waliuawa katika kijiji cha Mtole.

Nipashe ilipomtafuta jana Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, ili kujua hadi sasa kama kuna watu wamekamatwa kutokana na mauaji hayo, alithibitisha kufanyika kwa msako huo.

"Jeshi la Polisi Tanzania na Jeshi la Polisi Msumbiji yako kazini kuwasaka wauaji," alisema.

Ijumaa iliyopita, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, aliliambia gazeti hili kuwa mbali na vifo hivyo, wako pia majeruhi sita.

Alisema watu hao walivamiwa wakiwa kwenye mashamba yao ya mpunga na watu waliovalia sare zinazofanana na za Jeshi la Msumbiji.

IGP Sirro alisema siku hiyo kuwa juhudi za kuwasaka waliofanya mauaji na kujeruhi watu hao zinaendelea.

"Ninawaambia wauaji kuwa damu ya Watanzania haiendi bure, walioua tutawasaka kwa kushirikiana na majeshi ya Msumbiji kuhakikisha tunawakamata wakiwa hai au wamekufa. Wahalifu hawa baada ya kufanya vurugu waliondoka na wanawake wawili wa Tanzania na mtoto mmoja na hadi sasa hawajapatikana," alisema.

Aliongeza kuwa: "Hawa Watanzania walikuwa Msumbiji wakijishughulisha na kilimo cha mpunga. Wakiwa kwenye mashamba yao ambako wameweka vibanda vya muda, ghafla walivamiwa na watu wakiwa wamevalia sare zinazofanana na za Jeshi la Msumbiji na kuwaua baadhi na wengine kuwajeruhi."

"Tumewatembelea majeruhi, wako Watanzania sita na wengine wawili ni raia wa Msumbiji wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mtwara ya Ligula," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

LATRA

**Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini**

**TAARIFA KWA UMMA**

**NAFASI ZA MAFUNZO KWA MADEREVA WANAWAKE**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini - LATRA kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatangaza nafasi za ufadhili wa mafunzo ya miezi miwili kuwajengea uwezo madereva wanawake ili waweze kupata sifa za kuendesha magari ya abiria.

Lengo mahsusi la mradi huu ni kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kuwajengea uwezo wanawake 100 ambao hivi sasa wana uwezo wa kuendesha magari madogo. Madereva watakaofuzu watapata uwezo wa kuendesha magari ya abiria ikiwa ni pamoja na mabasi ya mradi wa Mabasi yaendayo Haraka. Mafunzo yatatolewa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji - NIT.

**Sifa na Vigezo vya Mwombaji:**

1. Awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 25,
2. Awe na Leseni ya Udereva kuanzia daraja D hadi C,
3. Awe na afya njema inayomuwezesha kuendesha gari,
4. Awe na Cheti cha Kuzaliwa au Kitambulisho cha Taifa, na
5. Awe anajua kusoma na kuandika.

**Utaratibu wa kufanya Maombi:**

**Barua ya maombi iambatishwe na:**

1. Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa au Kitambulisho cha Taifa,
2. Nakala ya leseni ya udereva,
3. Nakala ya vyeti vingine vinavyoendana na mafunzo hayo iwapo anavyo na nyaraka zinazooyesha uzoefu wa mwombaji.

**Maombi yatumwe kwa anwani ifuatayo:**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**LATRA, S. L. P. 3093,**
**Dar es Salaam.**
**Au barua pepe: dg@sumatra.go.tz na info@sumatra.go.tz**

***Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 31 Julai, 2019***

215305802

## Jaji Mkuu mstaafu Chande aagwa akimiminiwa sifa

**Na Salama Namga,** MAELEZO

JAJI Mkuu mstaafu, Mohamed Chande Othman, ameagwa rasmi kimahakama, baada ya kustaafu utumishi wa umma.

Alistaafu baada ya kuwa Jaji Mkuu kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi mwaka 2017, na aliagwa katika sherehe iliyofanyika jana katika Mahakama Kuu jijini Dar es Salaam.

Jaji Othman Chande aliushukuru uongozi wa serikali kuanzia awamu ya tatu chini ya Benjamin Mkapa kwa kumpa dhamana ya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, pamoja na Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, na hatimaye Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli kwa kuendelea kumwamini na kufanya nao kazi hadi alipostaafu mwaka juzi.

Jaji Chande alisema Mahakama ya Tanzania inazingatia mgawanyo wa madaraka katika utendaji kazi wake, na kuyafanyia kazi maoni ya umma pale yanapokusanywa ili kuboresha na kuimarisha huduma za kimahakama ili hatimaye ziweze kuwafikia wananchi kwa wakati.

Kwa upande wake Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, alimweleza Jaji Othman kuwa, serikali inatambua umuhimu wake na kazi zake alizofanya zimekuwa chachu ya maboresho makubwa yanayoendelea kufanyika katika Mahakama ya Tanzania.

"Serikali inatambua umuhimu na mchango wako katika kuimarisha maboresho ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi katika Mahakama ya Tanzania, pia tutaendelea kuufanyia kazi ushauri wako ambao unaendelea kutupatia kama Jaji mkuu mstaafu," alisema Prof. Juma.

Nao baadhi ya majaji waliohudhuria katika hafla hiyo, walimwelezea Jaji Mkuu mstaafu Chande kuwa ni mtu mwenye weledi na anayesimamia sheria za Mahakama, na ametoa mchango mkubwa katika maboresho yanayoendelea katika Mahakama na wataendelea kumuenzi kwa vitendo kwa kutumia busara zake na hekima aliyonayo katika kazi zao za kila siku.

Jaji Mkuu mstaafu Chande alizaliwa Januari Mosi, 1952, ana Shahada ya kwanza ya Sheria (LLB) ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Shahada ya Uzamili (MA) kutoka Chuo Kikuu cha Webster Geneva, Uswisi.

Aliwahi kuwa Makamu wa Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Rwanda (ICTR) jijini Arusha na amewahi kushika nafasi sawa na ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nchini.

Kadhalika, Jaji Chande amewahi kufanya kazi ndani na nje ya nchi katika mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama vile Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Msalaba Mwekundu. Pia ni mtaalamu mbobezi katika masuala ya Sheria za Haki za Binadamu.

# Miradi ya bil. 114/- kuongeza maji Dar, Pwani

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), imetia saini mikataba sita na Benki ya Dunia pamoja na makandarasi yenye thamani ya Sh. bilioni 114 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Pwani.

Katika halfa hiyo iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam katika ofisi za DAWASA, ilihudhuliwa na kushuhudiwa na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa; Waziri wa Tamisemi, Suleiman Jafo; Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso; Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega; Mwenyekiti wa Bodi ya Dawasa, Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange; Mwakilishi wa Benki ya Dunia, Wakuu wa Wilaya na Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Waziri Mbarawa alisema katika miradi hiyo, Dawasa inatumia fedha zake za ndani Sh. bilioni 40 kati ya Sh. bilioni 114 kutekeleza miradi mitano kati ya sita, ambapo mmoja kati ya miradi hiyo umesainiwa na Benki ya Dunia.

Alisema mradi wa kwanza ni wa usambazaji wa maji kuanzia kwenye matangi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mpaka Bagamoyo ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo nafuu ambao utekelezaji wake ni wa miezi 18 mpaka kukamilika.

Alisema kuwa mradi huo wa Chuo Kikuu hadi Bagamoyo unalenga kuhudumia wakazi zaidi 750,000 kulingana na usanifu ambapo wateja wapya zaidi 64,000 wa majumbani wataunganishwa na kuondoa tatizo la maji katika maeneo ya Changanyikeni, Bunju, Wazo, Ocean by Zone, Salasala, Bagamoyo zone na Vikawe zone katika wilaya za Bagamoyo, Ubungo na Kinondoni.

Mradi wa pili ni wa kusafirisha maji kutoka Jeti hadi Buza ambapo kazi ya ulazaji bomba la km.1.9 imekamilika na kipande kilichobaki cha km. 5.6 Dawasa itanunua bomba kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

Mradi wa tatu ni wa uchimbaji wa visima 20 katika eneo la Kimbiji na Mpera ambavyo vitazalisha maji lita milioni 260 kwa siku, na unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu.

Prof. Mbarawa alisema mradi wanne ni wa usambazaji wa maji kutoka Kisarawe-Pungu- Gongo la Mboto-Pugu Station-Airwing-Ukonga hadi Majohe ambao unatekelezwa na Mkandarasi Chico Limited kwa gharama ya Sh. bilioni 7, na kwamba kukamilika kwa mradi huo kutakuwa na maunganisho mapya zaidi ya 50,000 lengo la Dawasa ni kuhakikisha agizo la serikali linatekelezwa la kufikia asilimia 95 ifikapo Desemba mwaka huu ya upatikanaji wa maji.

Alisema mradi wa tano utatekelezwa katika mji wa Mkuranga ambapo hali ya upatikanaji wa maji sio wa kuridhisha kwani vyanzo vyote vya maji vimekauka, kusababisha wakazi wa mji huo kutumia maji yanayotiririka kutoka kisima kilichochimbwa na Dawasa mwaka 2015 kwa ajili ya utafiti.

"Hivi sasa mtandao wa mabomba ya maji uliopo wenye urefu wa Kilomita 11 unahudumia watu 4,500 kati ya watu zaidi ya 25,500,"

INAENDELEA UK. 8



Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi (kulia), akiagana na Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman, baada ya hafla fupi ya kumuaga, iliyofanyika katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Lugola aiagiza Nida kurudisha magari 3 ya vigogo

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amemwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Dk. Arnold Kihaule, kuyarudisha magari matatu yaliyokuwa yanatumiwa na waliokuwa vigogo watatu wa mamlaka hiyo. Akizungumza na viongozi wakuu wa Nida, jana jijini Dodoma, Waziri Lugola alisema magari hayo ni pamoja na lililokuwa la aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu, Dickson Maimu.

Aliyataja magari hayo kuwa ni linalomilikiwa na Maimu lenye namba za usajili STK 2524, linalomilikiwa na Paul Gwasondi, STK 4671 na STJ 1633, linalomilikiwa na Sabina Nyoni, yote aina Land Cruiser. Alisema magari hayo yanamilikiwa na watumishi hao kinyume cha taratibu hivyo yanatakiwa kurudishwa Nida.

"Ninakuagiza Mkurugenzi Mkuu hakikisha magari matatu yanayomilikiwa na waliokuwa watumishi wa Nida kinyume cha taratibu yanarudi Nida," alisema.

Aidha, Lugola alimwagiza Mkurugenzi Mkuu huyo kuwasimamisha kazi watumishi watatu wa mamlaka hiyo, baada ya vifaa mbalimbali vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 15 ikiwamo jenereta, kompyuta mpakato, kuibiwa kituo cha kuhifadhia kumbukumbu kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani.

Watumishi hao ni Gidson Ivon, Zabron Rusohoka na George Mwandevi.

Juni 18, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, aliwaambia waandishi wa habari kuwa, wanawashikilia watumishi saba wa Nida kwa tuhuma za wizi vya vifaa vya mamlaka hiyo zenye thamani ya Sh. milioni 15 ambavyo inadaiwa waliviiba na kuviuza. Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta mpakato mbili, nyaya zake na vitambulisho vya taifa boksi moja lililokutwa na vitambulisho 15,000.

Nyigesa aliwaambia waandishi wa habari kuwa watuhumiwa hao ambao majina yao yamehifadhiwa kwa uchunguzi, huiba vifaa hivyo na kuuza ili kujipatia fedha.

Alisema watuhumiwa hao waliiba vifaa wakati ofisi ikihama kutoka ofisi ya awali ya kiwanda chakubangua korosho cha Tanita kilichopo Tumbi, mkoani Pwani kwenda jengo lao jipya la Nida mkoani humo.

"Watumishi hawa waliteuliwa na Nida kuhamisha rasilimali vifaa kutoka ofisi hiyo ya zamani kwenda ofisi mpya za Nida, wakiwa njiani ndipo walipovichepusha na kuviuza kujipatia fedha kwa manufaa binafsi," alisema.

Kamanda alisema taarifa ya tukio hilo zilipokelewa Nida Juni 14 na katika ufuatiliaji wa Jeshi la Polisi ndipo walipowakamata watumishi hao saba.

"Jumla ya thamani ya mali yote iliyoibiwa ni Sh. milioni 15," alisema.

HABARI KITAIFA

# 14 mbaroni tuhuma uchakachuaji mifuko sukari

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAFANYABIASHARA 14 wanashikiliwa mkoani Shinyanga kwa tuhuma za kuhujumu uchumi, kwa kugushi mifuko 19,703 ya kufungashia sukari.

Inadaiwa kuwa mifuko hiyo iliingizwa kwenye viwanda vya Kagera, Sugar, Kilombero na Mtibwa na kusababisha upotevu wa mamilioni ya fedha. Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari juu ya kuwakamata wafanyabiashara hao, na kubainisha kuwa kosa la kugushi mifuko feki ni kuhujumu uchumi wa nchi kwa kuikosesha mapato Serikali.

Alisema wafanyabiashara hao 14 waliwakamata wilayani Kahama wakiwa na mifuko hiyo feki ya kugushi, ambayo huzalishwa nje ya nchi na wao kuisambaza nchini kwa wafanyabiashara wengine, ili wachakachue sukari kwenye viwanda pamoja na upunguzaji wa kilo. "Natoa rai kwa wafanyabiashara waache tabia ya kurudisha nyuma juhudi za Rais John Magufuli za kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda, na kuanza kuhujumu uchumi kwa kuikosesha mapato," alisema.

"Mifuko feki yenye nembo ya Kagera Sugar tumeikamata 504, Kilombero 17,726, Mtibwa 1,430 na viwanda vingine tofauti mifuko 43 ya kilo 50, kitendo ambacho ni kuwavunja moyo wawekezaji wa viwanda na kuporomosha uchumi wa nchi." Nao maafisa kutoka viwanda hivyo vya sukari, Vicent Mtaki (Kagera Sugar) na Brayson Mgalambe (Kilombero), walikiri mifuko yao kughushiwa na kufafanua ya kuwa huwa imeshonwa kwa nyuzi mbili na ndani huwa kuna mifuko mizito ya nailoni, tofauti na hiyo feki ambayo ina nyuzi moja na nailoni nyepesi.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kuwashikilia wafanyabiashara hao 14, na kubainisha taratibu zikikamilika watawafikisha mahakamani.

## Meli mpya yanukia Ziwa Nyasa

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, amekagua ujenzi wa meli ya abiria katika bandari ya Itungi Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya inayojengwa na kampuni ya Songoro Marine.

Kampuni hiyo iko chini ya mhandisi mzalendo, Salehe Songoro, na meli hiyo ina uwezo wa kubeba abiria mia 200 na mizigo tani 200.

Akitoa taarifa kwa Waziri Kamwelwe, Songoro alisema meli hiyo ya kisasa ipo hatua za mwisho za ufungwaji wa viti na vitanda kwa vyumba 20.

Aidha, alisema kazi ya kufunga jenereta na injini imekamilika, huku ufungaji wa umeme ukiendelea vizuri.

Hata hivyo, alisema ifikapo Julai 20, mwaka huu kila kitu kitakuwa kimekamilika.

Songoro alisema baada ya ujenzi kukamilika, meli itafanyiwa ukaguzi na mamlaka husika, na baada ya kuridhishwa itaruhisiwa kufanya kazi.

Mkuu wa Wilaya Kyela, Claudia Kita, alisema wameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa meli hiyo, na kwamba inayarajia kuanza safari zake Septemba 20, mwaka huu, na kila kitu kitakuwa kimekamilika.

Songoro alisema baada ya ujenzi kukamilika meli itafanyiwa ukaguzi na mamlaka husika na baada ya kuridhishwa itaruhisiwa kufanya kazi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya Kyela Claudia Kita, alisema wameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa meli hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, Issa Solomon, alisema meli itaongeza fursa mbalimbali za kiuchumi, na kuongeza kuwa mwambao wa Ziwa Nyasa una vivutio vingi kama samaki wekundu na vyungu ambavyo vitasaidia kuwaleta watalii.

Alimuomba Waziri kuboresha barabara katika Wilaya Kyela ili kukuza uchumi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA MAFUNDI SIMU ZA MKONONI NA VIFAA VYA KIELEKTRONIKI**

Kumekuwa na mwitikio mzuri sana kwa Mafundi wa simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki katika kupata mafunzo maalum ya kitaalamu tangu mafunzo hayo yaanze kutolewa kuanzia tarehe 23/07/2018 hadi sasa. Ni dhahiri kuna uhitaji mkubwa wa kuwa na Mafundi wa simu za mkononi waliofundishwa vema na wenye kuzingatia taratibu na sheria katika kazi zao, ili kuwa na uhakika wa mawasiliano salama kwa watumiaji wa vifaa hivyo.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania **(TCRA)** kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam **(DIT)** na Vyuo vya Ufundi Stadi **(VETA)** wamekuwa wakitoa mafunzo kwa Mafundi simu hao ambapo wanafunzi 144 wamehitimu mafunzo hayo na kati yao wanafunzi 110 wamefanikiwa kupata vyeti vya usajili kutoka **TCRA.**

Mafunzo haya yataendelea kutolewa tena kikanda kama ifuatavyo; **Kanda ya Ziwa** (Mwanza, Simiyu, Mara, Shinyanga, Geita na Kagera), **Kanda ya Kaskazini** (Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga), **Kanda ya Kati** (Dodoma, Tabora, Kigoma na Singida), **Kanda ya Mashariki** (Dar es Salaam, Mtwara, Pwani na Morogoro), **Kanda ya Nyanda za Juu Kusini** (Mbeya, Songwe, Njombe, Ruvuma, Iringa, Rukwa na Katavi) na **Ofisi ya Zanzibar** (Unguja Mjini Magharibi, Unguja Kaskazini, Unguja Kusini, Pemba Kaskazini, Pemba Kusini).

Aidha, tumeshuhudia pia mwitikio mzuri wa Mafundi simu na vifaa vya kielektroniki katika kujisajili na kupata cheti cha **TCRA** ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na Mafundi simu wenye ujuzi, **TCRA** inapenda kuwatangazia kuwa kuanzia tarehe **1 Julai 2020** Mafundi wote wa simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki **ambao hawajasajiliwa na TCRA** hawataruhusiwa kutoa huduma ya kutengeneza simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki. Sharti kubwa la kupata usajili wa **TCRA** ni kuwa wamepitia mafunzo ya awali ya ufundi wa simu za kiganjani na vifaa vya kielekroniki yanayotolewa na **DIT** au **VETA.**

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**

215302601

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NDC ina mpango mzuri kwa wakulima lakini...

**TANZANIA** inaendelea kutegemea kilimo katika maendeleo ya uchumi wake. Sekta ya kilimo imekuwa tegemezi kutokana na kuongoza katika kuchangia kwenye pato la taifa tangu uhuru.

Tangu wakati huo asilimia kubwa ya Watanzania wameendelea kuishi vijijini na kutegemea kilimo katika kuendesha maisha yao. Kutokana na mchango huo mkubwa wa sekta ya kilimo, ndiyo maana ilianzishwa kaulimbiu ya 'kilimo ni uti wa mgongo'. Licha ya serikali kubuni na kuanza kutekeleza mpango wa kuipeleka nchi yetu kwenye uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda ifikapo mwaka 2025, bado kilimo kitaendelea kuwa sekta muhimu kwa kuwa kitategemewa kwa ajili ya kusapoti viwanda.

Tunasema hivyo kwa kuwa mazao yatakayozalishwa ndiyo yatakayotumika kwenye viwanda kama malighafi za kuzalisha bidhaa za viwandani. Kutokana na umuhimu huo, bila shaka msukumo mkubwa utahitajika ili uzalishaji mashambani uongezeka mara dufu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya malighafi za viwanda. Kikubwa ambacho serikali ina wadau wa kilimo watatakiwa kufanya ni kupitia kwa umakini changamoto zote ambazo zimekuwa zikiwakabili wakulima na kuzipatia ufumbuzi ili kuwapa moyo na morali wakulima wazalishe zaidi.

Kadhalika, suala la motisha kwa wakulima haliwezi kuepukika kama kweli kama taifa timedhamiria kwa dhati kuboresha kilimo chetu kiwe cha kisasa na chenye tija.

Wakati taifa likiwa njiani kuelekea kwenye uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), limesema kuwa limelenga kuondoa jembe la mkono kwa wakulima kwa kuleta mradi wa kuunganisha na kusambaza matrekta nchini. Shirika hilo linasema kwamba mradi huo ambao utawawezesha wakulima watakaofika katika Viwanja vya Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) kupata trekta kwa mkopo kwa kutoa Sh. milioni tatu kama kianzio, kisha fedha zingine kulipa kidogo kidogo mpaka atakapomaliza deni.

Akizungumza juzi katika maonyesho hayo, Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC, Prof. Damian Gabagambi, alisema mradi huo ni mpango kati ya Tanzania na Poland wenye lengo la kuwasaidia wakulima kuwaondolea jembe la mkono.

Alisema matreka hayo hupatikana kwa mkulima kwa kutoa asilimia 25 ya fedha ya bei yake, lakini katika msimu huu wa Sabasaba wametoa ofa kwa wananchi kupata mkopo wa matrekta kwa masharti nafuu kwa kuanza kutoa Sh. milioni tatu.

Mpango huo wa NDC una lengo zuri la kuwawezesha, kuwajengea mazingira bora pamoja na kuwapa motisha wakulima ili wachangamkie kilimo cha kisasa na chenye tija.

Tunasema hivyo kutokana na uzalishaji wa wakulima wengi nchini kuwa duni kutokana na kutegemea kilimo cha jembe la mkono pamoja na kukosa mbinu za kisasa za uzalishaji.

Hata hivyo, shirika hilo lilitakiwa kwanza kutekeleza mradi huo kwa majaribio kwa lengo la kuelewa changamoto zake, ikiwamo uwezo wa wakulima kurejesha mikopo kwa wakati mwafaka. Kilichotokea kwa mikopo ya matrekta aina ya power tiller iliyotolewa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali (Suma-JKT) kwa watu mbalimbali hususan vigogo, lakini wakashindwa kulipa deni hadi leo lilipaswa kuwa ni fundisho.

Kwa upande wa bei ya kununulia, inaweza kuonekana ndogo, lakini suala la kurejesha mkopo ni lingine, kutokana na changamoto zake husika riba.

Kauli ya Prof. Gabagambi kuwa matrekta hayo yatakopeshwa kwa miaka miwili bila riba isipokuwa atakaposhindwa kulipa ndani ya muda huo, atalazimika kulipa kwa riba, linapaswa kuwa ni angalizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wakulima wakizingatia mafunzo dhuluma zitaisha

Na Sabato Kasika

**MIAKA** kadhaa iliyopita, wakulima wa pamba wa mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria walikuwa wakilalamikia changamoto walizokuwa wakikutana nazo katika kilimo cha zao hilo ambazo zilisababisha wakate tamaa kuzalisha pamba.

Wakulima hao ni wa mikoa ya Shinyanga, Geita, Simiyu, Mwanza na Mara, ambao malalamiko yao makubwa yalikuwa ni kuuziwa pembejeo mbegu feki ambazo hazioti, mbole feki ya majivu na pia ukosefu wa soko la zao hilo na pia kuibiwa katika mizani wanapouza kwenye magulio.

Kufuatia kilio hicho, serikali iliingilia kati na kudhibiti wasambazaji waliokuwa wakiwapa pembejeo feki na pia kukomesha mtindo wa kuchakachua mizani, ambao ulilenga kuwaibia kilo za pamba.

Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) ulio chini ya usimamizi wa Wizara ya Viwanda na Biashara mara kwa mara imetoa elimu, kwa wakulima sehemu mbalimbali pamoja na kuhakiki mizani zinazotumika kununulia zao.

Lengo kubwa ni kuhakikisha wakulima wanatambua mizani iliyo sahihi na inayoruhusiwa, ili wajilinde wenyewe pale maofisa vipimo wanapokuwa hawapo katika vituo vya kuuzia pamba.

Wakulima wanapotambua mizani iliyochakachuliwa na kuikataa, inakuwa ni rahisi kupata faida ya thamani halisi ya jasho lao, kuliko kuendelea kuibiwa na wajanja wachache wanaojinufaisha kwa jasho la wengine.

Pamba ni miongoni mwa mazao matano ya kimkakati ya biashara, ambayo serikali imevalia njuga na kuahidi kuyasimamia ili kuhakikisha yanapata soko na pia kila mkulima anafaidika na jasho lake badala ya kudhulumiwa kwa namna yoyote.

Pamoja na pamba ni mazao mengine ni pamoja na tumbaku, kahawa, korosho na chai, ambayo yana mchango mkubwa wa kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Hivyo kwa kitendo cha kukamatwa watuhumiwa ni wazi uchakachuaji bado upo na unaweza kukwamisha juhudi za serikali za kufanikisha kilimo hicho cha mazao ya kimkakati.

Watuhumiwa wa uchakachuaji ndiyo wanaokwamisha juhudi za serikali za kuwakomboa wakulima wa pamba kwa kuendelea kuwaibiwa wakitumia mizani iliyochakachuliwa kana kwamba hakuna marufuku yoyote dhidi ya matendo hayo.

Ni hivi karibuni Wakala wa Vipimo Mkoa wa Mwanza amenasa watuhumiwa wakiwa na mizani waliyoichezea ili kuwaibia wakulima kwenye vyama vya msingi vya kuuzia zao hilo.

Tukio hilo linaonyesha kwamba pamoja na juhudi za serikali, bado mtindo huo wa kuibia wakulima ni tishio, hivyo ni vyema serikali iendelee kuwamulika watu wa aina hiyo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Vilevile kama ambavyo Wakala wa Vipimo umekuwa ukitoa elimu kwa wakulima na kuwahamasisha ili kuzitambua mizani zilizochakachuliwa, ni wakati wa kuzidisha elimu hiyo, kwa kuzingatia kwamba kuna uwezekano wa wakulima kuongezeka kila mwaka. Wakulima wanapoongezeka, maana yake wengine ni wapya na huenda wasiwe na elimu kuhusu mizani hizo na hivyo wakawa waathirika kwa kuibiwa kirahisi bila kujua na kujikuta jasho lao likiishia mikononi mwa wahalifu wachache.

Serikali imeshafufua vyama vya ushirika, ambapo ununuzi wa pamba utafanywa na vyama hivyo, tena ni vile vinavyosimamiwa na wakulima wenyewe badala ya kuuza kupitia mawakala kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Utaratibu huo unamnufaisha zaidi mkulima kwa kuuza kupitia vyama vya msingi, kwani mazao yote yanayopatikana kutoka kwenye pamba kuanzia mbegu hadi nyuzi, anahusika kupata faida ya uuzaji wa mazao hayo.

## HABARI KITAIFA

# Biteko awacharukia wachimbaji wadogo kuendekeza migogoro

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko (pichani), amewacharukia wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wa eneo la Ikungi mkoani Mara baada ya kubaini kuwa ndio chanzo cha mgogoro kati yao na kampunio ya PolyGold Limited.

Biteko alitoa onyo kwa wachimbaji hao kuacha ujanja ujanja wakati akizungumza na pande zinazohusika na mgogoro huo katika kikao kilichofanyika ofisini kwake Mtumba, jijini hapa.

Aliwataka wachimbaji hao kuacha kusikiliza maneno ya watu walio nje ya makubaliano na mshirika wao na kusema waache tamaa badala yake waheshimu maafikiano waliyofikia kwa hiari bila uwapo wa wizara.

Waziri Biteko alisema yako malalamiko ya wawekezaji katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji, hivyo hataki kuruhusu ujanja ujanja utokee kwenye wizara anayoiongoza.

Aliongeza kuwa hata kama wawekezaji ni kutoka nje, wanayo haki ya msingi pale inapoonekana kukiukwa au kuonewa kwa kuwa shughuli zao ni halali na wanafuata sheria.

"Ndugu zangu niwaambie ukweli, huyu mmoja mnayemwona (mwekezaji) ana haki kama ninyi. Akionewa huyo mjue ana watu nyuma yake, ana ubalozi hapa kwa hiyo siko tayari kuchafua jina la serikali na wizara ninayoiongoza kwa kukiuka haki ya upande fulani. Uwe mzawa uwe mwekezaji wa nje, kwangu haki yako utaipata. Kwa hiyo kaeni na mkubaliane na mwekezaji wenu, mimi na wezangu tunatoka tunawaacha nikirudi tupate majibu msimamo wangu nimewapa," alisema Biteko huku akiwa amekasirika.

Kabla ya kuwaonya wachimbaji hao wadogo, Biteko alikutana na pande husika na kusikiliza madai ya kila upande na baada ya kuona wachimbaji wadogo wana makosa, aliwatoa upande wa Polygold na kubaki nao.

Baada ya maelekezo hayo, wachimbaji wadogo wakiongozwa na Edwin Mchihiyo na Sosy Mgonya ambaye leseni yake imenusurika kufutwa na waziri, walikaa pamoja na mwekezaji PolyGold (T) Ltd chini ya uwakilishi wa Sergey Sagsyan na Benny Haule na kuzungumza kuhusu mvutano juu ya mgogoro wao na kufikia muafaka uliosababisha kumaliza mgogoro wao.



Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mchihiyo alimshukuru waziri kwa kusimamia na kutatua mgogoro wao ambao umefikia tamati na kuahidi wanakwenda kutekeleza makubaliano yaliyokuwa yanaleta msigano baina yao.

# Wavuvi wafunguka kukosa mikopo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

CHAMA cha Ushirika cha Wavuvi Tanzania (Chakuwata) kimesema kutokana na wavuvi kutoaminiwa na taasisi za fedha, kunachangia raia kutoka mataifa mengine kuwekeza na kunufaika na sekta hiyo.

Mwenyekiti wa chama hicho, Rigoberth Mpemba, alisema hayo jana katika hafla ya kutia saini mkataba wa makubaliano ya ushirikiano kati yao na Benki ya Posta Tanzania (TPB), jijini hapa.

Alisema wanashindwa kushiriki kwenye uchumi wa viwanda kutokana na vipato duni kwa kuwa hawajaaminiwa na taasisi za fedha.

Mpemba alibainisha kuwa raia wa kigeni wamekuwa wakiwekeza na kufaidika na rasilimali za uvuvi huku wazawa kwenye sekta hiyo uchumi wao ukiwa duni.

Aidha, alisema chama hicho kinaundwa na vyama vidogo 24 vyenye wanachama 2,500 katika mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam, Pwani, Kigoma, Mwanza, Tanga na Rukwa.

Naye Mtendaji Mkuu wa TPB, Sabasaba Moshingi, aliwashauri wavuvi kujiunga katika vikundi ili kusaidiwa mikopo yenye masharti nafuu na taasisi za kifedha itakayowawezesha kununua vitendea kazi na kuinua uchumi wao.

Alisema madhumuni ya akaunti hiyo ni kuwawezesha wadau wa sekta ya uvuvi kujiwekea akiba ili kunufaika na huduma za kifedha.

Alitaja lengo lingine la kuanzisha akaunti hiyo kuwa ni kutoa fursa ya kukuza shughuli za uvuvi.

Naye, Kaimu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Sadick Chikula, alikitaka chama hicho kufungua matawi kwenye mikoa yote yenye shughuli za uvuvi ili kuwa na uwakilishi mpana na kutambulika na mamlaka zingine.


## BISMILAH RAHMAN RAHIM



Familia ya marehemu **Dk. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea Marehemu Dk. Omar Ali Juma itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **4 Julai, 2019** saa kumi jioni katika Msikiti wa Ngazija.

Kufika kwenu ndio mafanikio yetu. Ndugu, Marafiki na Jamaa wote mnakaribishwa.

Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

**AMIN.**

615303502

FSSP Field Support Services Project | Tanzania

**CONSULTANCY POSITION FOR GENDER EQUALITY TECHNICAL SPECIALIST TO SUPPORT THE GOVERNMENT OF CANADA (GLOBAL AFFAIRS CANADA)**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide consultancy services as the Gender Equality Technical Specialist under the Global Affairs Canada-funded Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The specialist will provide analysis and advice on the planning, design, management, monitoring and coordination of the Government of Canada's development assistance programming and policy dialogue in Tanzania (among other tasks).

Launched in June 2017, Canada's Feminist International Assistance Policy recognizes that supporting gender equality and the empowerment of women and girls is the best way to build a more peaceful, inclusive and prosperous world. **The Gender Equality Technical Specialist will pay an integral role in the implementation of Canada's Feminist International Assistance Policy in Tanzania.**

Candidates will be evaluated based on the following key qualifications and experience:

i. Bachelor's degree from a recognized university. A qualification higher than a bachelor degree will be an added advantage.
ii. A minimum of 4 years of professional work experience as technical expert and advisor on gender equality, of which at least two years are in relation to international development work in developing countries, preferably Tanzania or East Africa region.
iii. Experience providing gender equality technical advice and support on complex international development programs and projects in one or more of the following sectors: education, health, inclusive economic growth and inclusive governance.
iv. Experience in providing written gender equality analysis and comments on program/project proposals, implementation plans, progress reports and evaluations.
v. Experience in engaging in technical forums and policy dialogue on gender equality issues with development partners and government officials.
vi. Experience in carrying out research and analysis of systemic and emerging gender equality issues and trends.
vii. Knowledge and deep understanding of gender equality and empowerment of women and girl's issues in Tanzania

The following skills and competencies, while not essential, are assets for the work to be performed. Candidates should demonstrate them to the extent possible:

- Strong research, analytical and writing skills
- Strong skills in leadership, teamwork, networking, coordination and intercultural communication
- Advanced professional proficiency in English
- General professional proficiency in Kiswahili

**Strong candidates will be offered a competitive rate.**

Interested candidates should obtain a detailed description of these services by sending request email to **procurement@fssptz.org** specifying in the requests as follows: **"Consultancy position for FSSP Gender Equality Technical Specialist."**

Requests for further information will be received up to three working days prior to the **last submission date, 12 July 2019.** Any request received later than that may not be responded to.

**FSSP Manager**

215293702

## HABARI KITAIFA



Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ilala, Christopher Myava, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2019, ambapo imeweza kukagua miradi yenye thamani zaidi ya Sh. bilioni 38 na kubaini viashiria vya rushwa. **PICHA: JOHN BADI**

# Samia akemea Tanzania kuwa dampo bidhaa feki

INATOKA UK. 2

zinazalisha zile zitakazokidhi mahitaji ya viwanda vya ndani.

Alisema kwa kufanya hivyo viwanda vya ndani vitakuwa na uhakika wa soko la ndani na nje, na kusaidia kuongeza akiba fedha za kigeni.

Pia aliziagiza mamlaka zinazohusika kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini (Blueprint) ikiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu (GCLA), Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maliasili na Utalii, kusimamia utekelezaji wake.

"Tunataka mamlaka husika zisimamie kwa nguvu zote utekelezaji wa 'Blueprint' na tutazisimamia kwelikweli kuhakikisha zinaleta mrejesho mara kwa mara wa udhibiti wa vikwazo vya biashara ili pale penye tatizo tuwe tunalishughulikia," alisema.

Makamu wa Rais alisema maonyesho hayo yamethibitishwa kuwa bora katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kati, hivyo kampuni zitumie fursa hiyo kujitangaza zenyewe, fursa za utalii na uwekezaji.

Naye Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema wako katika mkakati wa mapitio ya sera ambayo yataendana na uchumi wa viwanda na kukamilika ifikapo mwakani.

Alisema mwitikio wa maonyesho hayo kwa mwaka huu umeongezeka na idadi ya kampuni za nje zinazoshiriki kufikia 580 kutoka 508 mwaka jana.

# Miradi ya bil. 114/-

INATOKA UK. 4

alisema Prof. Mbarawa.

Aliongeza kuwa watu wa Dar es Salaam na Pwani wanahitaji maji, hivyo ni jukumu la Dawasa kuhakikisha wanasimamia vizuri utekelezaji wa mradi hiyo kwa kuwa itakuwa mkombozi kwa wananchi.

Alitaja mradi wa sita kuwa ni wa kusafirisha maji kutoka Mlandizi (Ruvu Juu) hadi kijiji cha Mboga (Chalinze), ambao utasaidia kuondoa kero ya maji katika maeneo hayo kutokana na kuongeza kwa watu na ujenzi wa viwanda unaoendelea katika eneo la Mboga.

"Mradi huu wa bomba kuu unatarajiwa kusafirisha kiasi cha lita za ujazo 9,300,000 kwa siku, ambazo zitakuwa na uwezo wa kuhudumia wakazi wapatao 120 kwa siku," alisema Prof. Mbarawa.

Naye Jafo, alisema Waziri wa Maji anafanya kazi usiku na mchana kuhudumia wananchi na kutaka viongozi wengine waache tabia ya kufanya maigizo katika kuhudumia wananchi kwani watu wana shida.

"Jana (juzi) tumeanzisha wakala wa maji vijijini na nataka nikuhakikishie tutatoa orodha ya makandarasi ambao sio waaminifu kwa kuwa kulikuwa na uhujumu mkubwa katika wizara yetu, watu walikuwa wanakuja kufanya kazi na sisi wakati hawana hata mtaji wa kutosha na mwisho wa siku wanaharibu kazi kwa kushindwa kutekeleza miradi kwa ufasaha," alisema Aweso. "Tunashuruku sana kukubali kuunganisha Mkuranga na Dawasa ili tuweze kuwahudumia na katika kuhakikisha wakazi wa Mkuranga wanapata majisafi na ya uhakika tumepeleka Sh. bilioni 5 kwa ajili ya mradi wa tangi kubwa ambapo pesa hizo ni kutoka katika mapato ya ndani," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja.






# Familia yaeleza kutuma barua 11

INATOKA UK. 2

Hospitali ya Leuven, Ubelgiji nikawapa na anuani ya hiyo hospitali," alifafanua.

Vile vile, alisema barua nyingine ni ya Februari mosi, mwaka jana, kutoka Ofisi ya Bunge ikijumlisha kuwa ofisi hiyo inawasiliana na Wizara ya Afya kwa hatua zaidi baada ya familia kumhamishia Lissu nchini Ubelgiji na kuahidi kuijulisha familia uamuzi utakaofikiwa na barua hiyo kunakiliwa kwa Spika na Lissu.

Akizungumzia madai ya kutokujaza fomu za maadili, wakili Munghwai alidai kuwa hicho ni kisingizio kipya kwa kuwa sababu za kutokujaza fomu hizo zinajulikana, ni kutokana na Lissu kuwa mgonjwa.

Lissu akinukuliwa katika kipande cha video na kufuatiwa na waraka aliousambaza kwenye mitandao ya kijamii, alisema sababu za kumvua ubunge ni za kuokoteza.

Waraka na kipande hicho cha video vimethibitishwa na Mkuu wa Idara ya Habari ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kusema dunia nzima inafuatilia masuala yanayoendelea nchini na inafahamu mahali alipo tangu alipopigwa risasi Septemba 7, mwaka juzi.

"Sababu zilizotolewa ni za kuokoteza ili kujaribu kuhalalisha maamuzi haramu waliyoyafikia muda mrefu uliopita," alisikika Lissu kwenye kipande hicho cha video.

Vile vile, Mbunge huyo alisema anashangazwa na kauli ya Spika kwa kuwa viongozi mbalimbali akiwamo Makamu wa Rais aliyefika kumjulia hali katika Hospitali ya Nairobi nchini Kenya na aliyekuwa balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Joseph Sokoine, alifika mara mbili katika Hospitali ya Chuo kikuu ya Leuven, kumuona.

Kwa mujibu wa Lissu, Bunge linajua alipo kwa kuwa Katibu wa Bunge Steven Kagaigai, amekuwa na mawasiliano rasmi na familia

yake kwa ushahidi wa barua ikiwamo ya mwezi Machi, mwaka jana.

Alisema Katibu wa Bunge anadaiwa kumwandikia barua kaka yake kuhusu mgogoro wa Bunge kugharamia matibabu yake.

### MEMBE ANENA

Akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, alisema ameshangazwa na kitendo cha Tundu Lissu kuvuliwa ubunge.

"Kama Mtanzania na mimi nilishangazwa Lissu kuvuliwa ubunge, sasa tusubiri aje, nina hakika kabisa ataenda mahakamani na kama kuna haki ataipata mahakamani," alisema Membe.

Akizungumzia matukio mbalimbali ya watu kutekwa au kupotea, Membe aliwataka viongozi wakiwamo wa dini, vyama vya siasa na viongozi wastaafu kukemea suala hilo kwa

kuwa ni utamaduni mpya aliodai unaiondolea Tanzania heshima duniani.

"Mimi naona huu ni utamaduni mpya ambao haukubaliki na ningependa kuchukua nafasi hii kusema tu kwamba suala la utekaji au watu kupotea linaweza kuiondolea nchi yetu heshima duniani," alisema Membe.

HABARI KITAIFA

# Wasiojulikana wavamia kampuni ya tumbaku, waiba kompyuta 10

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WATU wasiojulikana wamevamia na kuvunja ofisi ya kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya Alliance One na kuiba kompyuta sita na 'laptop' nne zilizokuwa zikitumika kutunza kumbukukumbu za ofisi hiyo.

Hali hiyo ilisababisha kampuni hiyo ishindwe kufanya kazi kwa zaidi ya siku tano.

Watu hao wanadaiwa kuvamia ofisi hiyo usiku wa manane wa kuamkia Juni 29 na kuiba kompyuta hizo zilizokuwa zikitumika katika kutunza taarifa za ununuzi wa tumbaku.

Mmoja wa wafanyakazi wa kampuni hiyo ambae hakutaka jina lake kuandikwa gazeti, alikiri kuvunjwa kwa ofisi hiyo na kuibwa mali hizo, na kudai watu hao wanatuhumiwa kushirikiana na walinzi wa Kampuni ya Kirumi Security Service, na kuwa walinzi walikimbia baada ya tukio hilo.

Alisema kampuni haijapoteza nyaraka zozote kutokana na kuibiwa kwa kompyuta hizo kwa sababu kazi zao zote zinahifadhiwa kwenye mfumo ambao seva yake iko Morogoro pamoja na Brazil ambapo ni makao makuu ya kampuni hiyo.

"Shughuli zetu zinafanyika kwenye mtandao na taarifa za kumbukumbu za masoko tuliyoyafanya ziko salama kutokana na taarifa hizo kuwa Morogoro na makao makuu ya kapuni yaliyopo Brazil, hivyo wakuliwa wasiwe na wasiwasi juu ya tukio hilo," alisema.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema watuhumiwa ni walinzi wa Kirumi Security Service ambao walikuwa walinzi wa zamu, na kwamba baada ya wizi walitelekeza lindo hilo na kutoroka.

Alisema kuwa juhudi za kuwatafuta na kuwakamata zinaendelea na watakapokamatwa watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua kama sehemu ya ukarabati wa Barabara ya Siwa, eneo la Viwandani, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI.**

# Mwenyekiti ataka ushirikiano wa wataalamu, viongozi CCM

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

WATENDAJI na wataalamu wametakiwa kujenga uhusiano wa karibu na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) hali itakayoleta ufanisi kwenye utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani, Ramadhani Maneno, akipokuwa akifungua mafunzo kwa viongozi wa mashina na matawi wa Kata ya Tengelea Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Maneno ambayo pia ni ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, akiwataka washiriki kuzingatia na kuyapeleka mambo waliyofundishwa kwa wanachama wengine. "Wenyeviti wa serikali za vijiji, vitongoji na madiwani kupitia chama tawala wahakikishe kupitishwa kwao na chama kugombea tena kutategemea uitishaji wao vikao vya kisheria na kusoma mapato na matumizi," alisema.

Akizungumzia mafunzo hayo ambayo ni ya kwanza kwa Wilaya ya Mkuranga, kiongozi huyo alimpongeza Diwani wa Kata ya Tengelea, Shabani Manda, kwa kudhamini mafunzo hayo sambamba na kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali, huku akiwataka viongozi kuacha nyayo wanapomaliza muda wao.

Kwa upande wake, Diwani Manda ambaye anaongoza kamati ya maendeleo ya kata aliweka wazi mafanikio yaliyopo katika vitongoji na vijiji.

Alisema utekelezaji wa ilani ya CCM utafanikiwa kwa kiwango kikubwa ikiwa kutakuwapo ushirikiano wa karibu kati ya wataalamu na viongozi wa chama hicho pamoja na wananchi kwa ujumla.

## Changamoto zakwamisha vijana kilimo cha nyanya

**Na George Tarimo, IRINGA**

UKOSEFU wa mitaji na pembejeo kumetajwa ni moja ya changamoto inayokwamisha vijana wanaojishughulisha na kilimo cha nyanya katika Kijiji cha Magubike mkoani Iringa kujikwamua kiuchumi.

Idadi kubwa ya vijana mkoani Iringa hasa waishio vijijini hutegemea shughuli za kilimo hususan cha mazao ya biashara, zikiwamo nyanya, lakini kukosekana kwa mitaji ya uhakika imekuwa shubiri kwao, hivyo kuchangia ongezeko la vijana wengi kuzurura mitaani.

Baadhi ya wakulima katika kijiji hicho Laji Ngalioma na Ezdory Malukusi wameomba serikali kuwapatia mikopo yenye riba nafuu kwa sababu wengi wao wamekwama kwenye mitaji ili waweze kuendeleza kilimo. Malukusi alisema kuwa serikali inatakiwa kuwaunganisha vijana na taasisi za kifedha ili waweze kupata mikopo kwa sababu vijana walio wengi hawakopesheki na ndio maana wengi wao wanabaki wakizagaa mitaani.

Zao hilo kwa sasa mkoani Iringa hutegemewa na wakulima wengi kutokana na uwapo wa soko la uhakika ambapo baadhi ya wakulima wa zao hilo ambao ni wanufaika akiwamo Edga Ngalima, alisema vijana walio wengi wanashindwa kuingia katika kilimo kutokana na kukosekana kwa mtaji na pia uvivu.

Ngalima ambaye ni mkulima wa nyanya katika kijiji hicho ambaye kwa sasa analima zaidi ya hekari tano za nyanya, alisema vijana wengi nchini hawataki kujishugulisha na kilimo badala yake hulalamika kuwa hakuna ajira.

Ngalima alisema zipo fursa nyingi ambazo wanaweza kufanya vijana mfano alizeti na maharage ambazo haziitaji gharama kubwa, lakini nyanya inahitaji mtaji mkubwa.

"Nawaasa vijana waondokane na mambo ya vijiweni, wafanye kazi, wajichanganye na kuacha uvivu bali wafanye mambo ya kilimo ili waweze kupata maendeleo na kujikwamua kiuchumi," alisema Ngalima. Katika kuunga jitihada za uhamasishaji wa kilimo hicho kwa vijana kampuni ya Beya Crop Science kupitia kitengo chake cha utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za mboga duniani, Seminizi, imeanza kutoa mbegu ya nyanya aina ya Firenza F1 na kuwakusanya vijana mkoani hapa kwa lengo la kutoa elimu ya namna ya upandaji wa zao hilo kitaalamu ili kujikwamua kiuchumi.

Willium Macha, Ofisa Biashara Beya Crop Science, alisema kuwa kilimo cha nyanya Iringa kimekuwapo kwa miaka mingi, lakini kampuni ya Beya Crop walifanya utafiti na kugundua wakulima walikuwa wakitumia mbegu chotara na kuwataka wakulima kutumia mbegu ya Firenze nyanya dum dum ili waweze kuongeza kipato, na pia mbegu hiyo inastahimili magonjwa, huku mkulima akipata mazao mengi ikiwamo kuzalisha hata zaidi ya tani tisa.

Macha alisema lengo la kampuni hiyo ni kuwainua wakulima wa nyanya nchini pamoja na kutoa elimu juu ya kuachana na kilimo cha mazoea, na badala yake wajikite katika kilimo cha kitaalamu.

Kwa sasa tenga moja la nyanya huuzwa kwa Sh. 50,000, lakini bado changamoto ya mitaji na ugonjwa wa Kantangaze ambao hushambulia zaidi nyanya, imeonekana kukwamisha juhudi za wakulima wengi.

# Rita yasisitiza wananchi tabia ya kuandika wosia

**Na Elizabeth Zaya**

WAKILI wa Serikali Mwandamizi kutoka Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Edna Kamara, amesema uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa kuandika wosia umekuwa chanzo cha migogoro ya kesi za mirathi.

Akizungumza katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF), yanayofanyika viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, Kamara alisema ifike wakati wananchi wajenge mazoea ya kuandika wosia kabla ya kufariki.

Alisema wosia ni kitu muhimu kwa kuwa mtu anakuwa ametoa tamko kabla ya kufa, hivyo anakuwa amechagua sehemu atakayozikwa au watu wanaotaka kurithi mali zake.

"Jamii ikiwa na uelewa kuhusu umuhimu wa wosia, masuala ya kesi za mirathi yatapungua kwani kesi nyingi zimekuwa zikisababishwa na kukosekana kwa wosia," alisema Kamara.

Alisisitiza kuwa wakati wa kuandika wosia ni lazima pawapo na mashahidi wawili, na picha ndogo za mtoa wosia.

Kamara alisema mwananchi yeyote bila kujali idadi ya mali wala jinsia anaweza kuandika wosia ambapo wanandoa wanaweza kuandika pamoja.

Alisema mara mtu anapoandika na kutunza wosia anapofariki mmoja wa mashahidi atatakiwa kutoa taarifa Rita na baada ya hapo utaratibu wa kuwasilisha wosia sehemu husika hufanyika.

Pia, alisema kuna aina mbili za wosia ambazo ni wosia wa maandishi na matamshi.




Wananchi wakiingia katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa kwenye Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

# Tira yawashauri Watanzania kutumia huduma za bima

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA), imewataka Watanzania kuhakikisha wanajiunga na huduma za bima kwa ajili ya kuwakinga na majanga mbalimbali pamoja na usalama wa mali zao.

Aidha, mamlaka hiyo imesema zaidi ya kampuni 30 za bima zimeshiriki katika maonyesho ya 43 ya kimataifa ya biashara yayofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa mtu kuwa na bima maishani. Akizungumza na waandishi wa habari katika viwanja vya maonyesho hayo vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, Ofisa Uhusiano wa Tira, Oyuke Phostine, alisema kuwa dhumuni la kushiriki katika maonyesho hayo ni kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kujiunga na bima.

Alisema pia watahakikisha wanaangalia mifumo ya utoaji wa bima inaimarika nchini na elimu hiyo kwa wananchi inaendelea kutolewa kwa wingi.

"Tunatambua kuwa mtu akipata elimu hii ya umuhimu wa bima inakuwa rahisi kwake kujiunga, hivyo TIRA tutaendelea kuzisimamia kampuni hizo ili zitoe elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa bima, lakini pamoja na utoaji wa elimu mamlaka katika maonyesho haya tutaangalia mifumo ya utoaji wa bima inaimarika," alisema Phostine.

Aidha, alisema katika maonyesho ya mwaka jana awakuboresha vitu vingi kwa sababu ilikuwa ni mara ya kwanza kwao kushiriki lakini kwa mwaka huu wameboresha na wamefanikiwa kuingia katika ushindani.

## Waziri: Siasa isiingizwe katika korosho

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema zao la korosho lisichukuliwe kisiasa, bali kama muhimili wa uchumi wa nchi.

Akizungumza katika maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara (DITF) katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema kuna baadhi ya watu wanaharibu soko la zao hilo kimataifa kwa maslahi binafsi.

Alisema hivi sasa serikali ipo katika mikakati ya kuboresha zaidi mazao mkakati ili kuleta tija nchini.

Waziri Bashungwa alisema alishafanya ziara ya kutembelea maghala ya korosho na kubaini kuwa korosho zinazolimwa Tanzania ni bora na zina thamani katika soko la kimataifa.

Pia alisema licha ya ubora wa korosho hizo lakini kuna baadhi ya watu wanathubutu kupiga simu za kuzuia wanunuzi kutoka nje ya nchi wasije kwa madai ya kuwa korosho ya Tanzania haina ubora.

"Nashangazwa na uzalendo wa baadhi ya Watanzania... mauzo ya korosho yana maslahi kwetu sote, lakini bado wanapiga simu kuweka vizuizi vya masoko hayo," alisema.

## Wito shule kushiriki maonyesho Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

SHULE ya Sekondari ya Tusiime ya jijini Dar es Salaam imetoa wito kwa shule mbalimbali hususani za binafsi, kujenga utaratibu wa kushiriki katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara kwa kuwa ndio fursa pekee ya kujitangaza kitaifa na kimataifa.

Akizungumza katika viwanja vya maonyesho hayo (Sabasaba) yanayofanyika Kurasini, Temeke, Ofisa Masoko wa Tusiime, Ndemugoba Nyagwe, alisema watu wengi ikiwamo sekta ya waendesha shule binafsi wamekuwa wakifikiri kwamba maonyesho ni ya kampuni kubwa pekee.

Alisema wao kama Tusiime ni mara ya kwanza kushiriki katika maonyesho hayo, lakini wamejifunza mambo mengi na kwamba wanaamini endapo wangegundua jambo hilo mapema wangekuwa wamefika mbali.

"Hili wazo la kushiriki katika maonyesho tumelipata mwaka huu na katika siku hizi za awali tu tumebaini kwamba hii ni fursa nzuri sana kwa ajili ya kujitangaza na kujifunza fursa mbalimbali na tunaamini tungeanza siku nyingi, tungekuwa mbali sana," alisema Nyagwe na kuongeza:

"Tatizo watu wengi wanajua kwamba kushiriki katika maonyesho haya ni mpaka uwe na kiwanda au kampuni kubwa, naomba wafahamu kwamba hapa ndio mahali pazuri pa kuanzia, kujitangaza na kujifunza pia."

# TRA yasamehe wazee kodi

**Na Zanura Mollel, ARUSHA**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesamehe kodi ya majengo yanayomilikiwa na wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60.

"Wazee wa miaka 60 na kuendelea hawatalipia jengo wanaloishi, lakini kama wanalo linalotumika kwenye biashara wanatakiwa kulipia kodi Sh.10,000," alisema Deogratius Wambura.

Akizungumza na Nipashe jana ofisi kwake, Wambura ambaye ni Ofisa Mfawidhi Mamlaka ya Mapato, Wilaya ya Longido, alisema, mabadiliko yaliyofanywa na sheria ya fedha sura 289 pamoja na sheria ya TRA kwa mwaka 2016, inafafanua na kutoa mamlaka juu ya ulipaji wa kodi ya majengo.

"Mabadiliko hayo yameipa TRA, jukumu la kusimamia na kukusanya kodi ya majengo nchi nzima, ikiwa ni lengo la serikali katika kuongeza ufanisi kwenye makusanyo ya kodi," alisema Wambura.

Aliwataka wananchi wote ambao wanahitajika kulipia majengo hayo, kufanya hivyo kwa wakati na kusema kuwa taratibu zote kisheria zinaratibiwa kusajiliwa na malipo ya kodi, inayotokana na umiliki wa majengo hufanyika katika Ofisi ya TRA Namanga.

Alifafanua kuwa serikali imeweka viwango nafuu kwa jengo la kawaida ambako mmiliki hulipi Sh.10,000 na 20,000 hadi 50,000 kwa majengo ya ghorofa kulingana na eneo lilipo.

Hata hivyo, malipo yote yanafanyika baada ya kupata namba ya udhibiti (Control Number), alikumbusha.

"Baada ya kusajiliwa kupitia mfumo wa TRA na muamala wanaweza kulipa kupitia NMB, CRDB, Mpesa, Airtel Money, Tigo pesa au Halo pesa," alifafanua Wambura.

Aidha, aliwataka wananchi kutambua kuwa kodi hii ya umiliki wa majengo inalipwa kila mwaka wa fedha wa serikali, ambao ni kuanzia Juni 30 hadi Julai Mosi kila mwaka. Hivyo aliomba wahusika wafike ofisini kwa ajili ya usajili na kulipia majengo yao.

# Wadau walaani utoroshaji madini

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

CHAMA cha Wafanyabiashara wa Madini Taifa (Tamida) na wadau wa madini wamelaani jaribio la utoroshaji wa madini kupitia mpaka wa Namanga mkoani Arusha.

Madini hayo yalikuwa yatoroshwe Juni 26 mwaka huu, kupitia mpaka huo wa Kenya na Tanzania.

Hayo yalisemwa jana wakati wa kusoma tamko la kulaani tukio hilo, lililosomwa na Mwenyekiti wa Tamida Arusha, Sammy Mollel, akisema kitendo hicho hakikubaliki kwa sababu ni kuhujumu uchumi kinachopelekea taifa kupoteza mapato yatokanayo na sekta ya madini.

Alisema serikali imeboresha na kuweka mazingira bora ya kuhamasisha wachimbaji kuuza madini yao katika masoko kwa kuwaondolea kodi ambazo zilikuwa ni kikwazo katika biashara, kodi ya zuio, asilimia tano na kodi ya ongezeko asilimia 18 na tozo hiyo sasa inatozwa asilimia sifuri.

"Lengo la kuondoa urasimu huu ni kuhamasisha biashara ifanyike katika masoko na hivyo kutokomeza ulanguzi na kudhibiti utoroshaji wa madini, ili sekta hiyo iweze kutoa mchango katika pato la taifa na kukuza uchumi wa nchi," alisema Mollel.

Aliiomba serikali ihakikishe inawasaka na kuwatia nguvuni waliohusika katika jaribio la utoroshaji madini hayo ili sheria ifuate mkondo wake na ikibidi kutaifisha madini hayo.

"Ni lazima ifike mahali kila mmoja hasa sisi wafanyabiashara tufuate sheria na kusimamia kile serikali inachotaka kwa faida ya taifa letu na familiya zetu," alisema.

Alisisitiza kuwa Tamida inampongeza Waziri wa Madini, Dotto Biteko, kwa hatua za haraka alizochukua kufuatilia jambo hilo.

Madini hayo yalikamatwa Juni 26 mwaka huu saa 7:00 mchana huko mpakani Namanga wilayani Longido, yakiwa kwenye gari namba T.716 AAC aina ya Scania Perfect mali ya Charles Shoo, yakiwa yanapelekwa nchini Kenya.

Aina za madini yaliokamatwa (majina yametoholewa ili yasomeke kwa Kiswahili) ni pamoja na tanzanite, rubi, safaya, spineli, tomalini, savoriti, grosula na akwamarini yote yakiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 958.



Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Haydom, mkoani Manyara, Dk. Emmanuel Nuwass (kushoto), akikagua mafundi wakati wakifunga mashine mpya ya kisasa ya mionzi (X-Ray) ya thamani ya Sh. milioni 300, hospitalini hapo jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wajumbe H/Kuu waipongeza serikali

**Novatus Makunga, ARUSHA**

WAJUM BE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, wameipongeza serikali kufanikisha kwa kiwango cha juu utekelezaji wa ahadi zilizotolewa wakati wa uchaguzi.

Mafanikio hayo yamo kwenye sekta za afya, mifugo na jitihada za kuupunguza umaskini.

Hatua hiyo inatokana na taarifa iliyowasilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, katika mkutano wa halmashauri hiyo wa kupokea maelezo kuhusu utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, kwa mwaka wa fedha wa Julai 2018 hadi Juni 2019.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Loatha Sanare, alisema pamoja na mafanikio kujitokeza katika sekta zote, lakini kwa kiwango cha juu zaidi yameng'ara zaidi katika afya na mifugo.

Alisema kumekuwapo na mafanikio makubwa katika sekta za elimu na miundombinu, hususani uimarishaji wa barabara pamoja na miradi ya maji, ujasiriamali kwa vijana, wanawake na walemavu pamoja madini.

"Serikali inayo kila sababu ya kujivunia mafanikio hayo ambayo imeendelea kuyapata katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ilivyoahidiwa kwa wananchi mwaka 2015," alisema.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za serikali, Gambo, aliwaeleza wajumbe kwamba mkoa huo umefikia asilimia 95 ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya.

Gambo alisema kuwa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika kila halmashauri za mkoa huo, inaendelea kuimarika ambapo kwa mwaka 2018 upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, ulifikia asilimia 93 na mwaka huu wa 2019 kiwango hicho kimefikia asilimia 95.

Alisema idadi ya kaya zilizoandikishwa katika mfuko wa afya ya jamii ni 125,003 kati ya kaya 380,491.

Aidha, Gambo alieleza kwamba idadi ya watoto waliokuwa na hali nzuri ya afya kutokana na lishe bora walikuwa 776,534 sawa na asilimia 89 kati ya watoto 869,242 waliohudhuria kliniki mwaka 2017/2018.

"Katika awamu ya tano Arusha imeongeza ujenzi vya vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 365 mwaka 2016 hadi 375 kwa mwaka 2019," alisema.

Gambo alisema serikali ilitenga Sh.bilioni 6.1 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa vituo vya afya 15 katika halmashauri zote saba za mkoa huo, ambapo vituo sita kati ya hivyo, vimekamilika na vimeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Katika kukabiliana na malaria alisema kuwa zaidi ya vyandarua vyenye viuatilifu 250,368 vimesambazwa kwa wananchi bila malipo pamoja na kufikishwa katika vituo vya afya.

Kadhalika, Gambo alieleza kuwa serikali iliupatia mkoa huo zaidi ya Sh. bilioni saba kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika halmashauri zote saba za mkoa huo.

Gambo, alisema kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kutoka zaidi ya Sh. milioni 960 mwaka 2015/2016 hadi kufikia zaidi ya shilingi bilioni saba mwaka 2018/2019.

Kwa upande wa sekta ya mifugo, Gambo alisema kuwa mkoa huo umechanja mifugo zaidi ya 1,445,436 dhidi ya magonjwa yote hatari.

Katika hatua nyingine mkoa wa Arusha umefanikiwa kuwapatia vitambulisho wajasiriamali wadogo wapatao 71,821 sawa na asilimia 57.4 ya lengo la kuwafikia wajasiriamali 125,000, ambapo kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 1.4 zimekusanywa.

# Ofisa elimu mstaafu jela miaka 12 kwa ufisadi

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

ALIYEWAHI kuwa Ofisa Elimu wa Wilaya ya Siha na Mratibu wa Mradi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) uliokuwa ukitekelezwa wilaya humo, Lawrencia Massawe, amehukumiwa kifungo cha miaka 12 gerezani, baada ya kukutwa na hatia ya kujipatia fedha isivyo halali. Sh. milioni 13.5

Massawe alikutwa na hatia juzi, baada ya mahakama hiyo kujiridhisha kuwa alitenda kosa la kughushi nyaraka za serikali na kujipatia kiasi hicho.

Mahakama hiyo, pia imemwachia huru Tumpala Ambakyse, Mhasibu wa Halmashauri ya Siha, baada ya mahakama hiyo kumuona hana hatia.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Siha, Jasmine Abdul, alisema mahakama hiyo imemwona Massawe ana hatia, baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa na mashahidi 23 wa Jamhuri.

Wakati anasoma hukumu hiyo, Hakimu huyo alisema kwa kuwa ushahidi uliotolewa dhidi ya mshtakiwa haujaacha shaka ndani yake, mahakama hiyo imemtia hatiani kwa makosa 12 ikiwamo ya kughushi na kujipatia fedha hizo.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Suzan Kimaro, kuwa washtakiwa hao, mnamo Oktoba mwaka 2017, walifanya makosa mbalimbali ikiwamo ya kughushi nyaraka na kujipatia kiasi cha Sh. milioni 13.5

Alidaiwa kuwa kosa hilo ni kinyume cha kifungu cha 28 (1) cha Sheria ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, kifungu cha 11 cha Sheria ya Mwaka 2007.

Unicef ilitoa kiasi cha Sh. milioni 23.9 kwa ajili ya kuendesha mafunzo na kwenda kuwaibua wanafunzi vijijini ambao hawakufanikiwa kupata elimu ya msingi, lakini Sh. 13.5 zilipotea kiaina.

Ilidaiwa kwamba mshtakiwa alighushi nyaraka ambazo zikionyesha alitoa semina kwa siku mbili kwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji 37, maofisa watendaji 36, watendaji wa kata 12, waratibu elimu kata 12, maofisa tarafa watano na kila mmoja alitakiwa kulipwa posho ya Sh. 180,000 badala yake walilipwa Sh. 45,000.



Mkuu wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buswelu, akishiriki katika zoezi la msaragambo na wananchi wa Kata ya Biriri, juzi, katika kuhakikisha ujenzi wa shule ya sekondari ya kata hiyo unakamilika na wanafunzi kuingia mwezi Januari 2020. **PICHA: MARY MOSHA**.

# Mil. 120/- kujenga shule kata

**Na Mary Mosha, SIHA**

HATIMAYE kilio cha wakazi wa Kata ya Biriri wilayani Siha ya kukosa shule ya sekondari, kimepatiwa ufumbuzi baada ya serikali kutenga zaidi ya Sh. milioni 120 kwa ujenzi wa shule hiyo.

Wakizungumza wakati wa msaragambo wa uchimbaji wa msingi wa shule hiyo, mmoja wa wakazi hao, Jenipha Maswala, alisema uwapo wa shule hiyo utasaidia watoto kutotembea kilomita sita mpaka tisa kufuata elimu katika Shule ya Sekondari Nuru au Kilingi.

"Hiki kimekuwa kilio chetu cha muda mrefu kuona wanafunzi wetu wanapata shule karibu ili kutokomeza matukio yanayowakumba watoto wetu hasa wa kike kutokana na umbali mrefu wanaotembea kwenda katika shule zilizopo mbali," alisema Pascali Joseph Sophia Massawe, alisema katika mazingira ya kijijini watoto wa kike wapo kwenye hatari kubwa ya kupata mimba kutokana na mazingira na vishawishi wanavyokutana navyo njiani.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema serikali imeona na kusikia kilio cha wazazi wa Biriri cha watoto kutembea umbali mrefu ili kupata elimu ya sekondari, na kuanziasha ujenzi wa shule hiyo kwa kushirikisha wadau na serikali.

Alisema lengo ni kuhakikisha ifikapo Januari 2020 shule hiyo ianze kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza.

"Sisi kama ofsi ya wilaya tumetoa tofali 400 pamoja na mchanga, CCM wilaya imetoa tofali 600 na wapo baadhi wametoa tofali 800...hii ni kuonyesha kuwa wadau tumejipanga katika kuhakikisha shule hii inajengwa na kukamilika kwa wakati.

Valerian Juwel, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, alisema zipo shule mbili mpya katika kata 17 za wilaya hiyo wanatarajia kupokea wanafunzi 2,020, hivyo kuwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi katika kufanya kazi za mikono ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika mapema. "Hii kata ni miongoni mwa kata zilizochelewa kupata shule za kata na hii ni kutokana na wananchi walikosa mtu wa kuwaunganisha... kitaalamu tumeona kunauhitaji wa wanafunzi 100 kupata mafunzo hapa," alisema na kuongeza:

"Tutawapa walimu na vitu vingine vyote vinavyohitajika ili kuhakikisha wanafunzi wa shule hii wanapata elimu bora."

Mmoja wa wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Kilingi, Ester Saimon, alikiri kuwapo kwa umbali mrefu wa kwenda shuleni, huku wakilalamikia mazingira halishi nyakati za mahindi. "Tumekuwa tukiponea chupuchupu kubakwa na hata wakati mwingine kukimbizwa na vijana wasio waadilifu kutokana na umbali ...tunaotembea na kupitia mashamba ya mahindi msimu wa masika... ikiwa shule hii itakamilika itatusaidia kupata elimu bora," alisema Faustina Alexinda.

# Wawekezaji waitwa kuwekeza Kilimanjaro

**Na Mary Mosha, MOSHI**

SERIKALI imeendelea kuwataka wawekezaji wa viwanda kuja kuwekeza mkoani hapa, huku akiwahakikishia umeme wa uhakika ndani ya siku 365 kwa mwaka pamoja na maji ya uhakika.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ndiye aliyewakaribisha wawekezaji hao alipozungumza ofisini kwake na kusema ni wakati sasa wa wanahabari kushirikiana na serikali katika kuhakikisha wanawavutia wawekezaji wengi.

Alisema umeme unaozalishwa mkoani hapa, unatosheleza na kuwataka wawekezaji wa viwanda kuja kuwekeza kwani hakutakuwa na tatizo la kukatika kwa umeme.

Alikemea vikali na baadhi ya watu kulihujumu shirika hilo kwa kuharibu miundombinu na wezi wa nyaya za umeme na kuiomba jamii kutoa ushirikiano katika kuwaibua watu hao ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki.

Alitoa kauli hiyo kufuatia taarifa iliyotolewa na Meneja wa Tanesco mkoani hapa, Mhandisi Mahawa Mkaka, ya kuwapo kwa hujuma hizo.

"Nasikitika kuona baadhi ya watu wanalihujumu shirika letu kwa kuiba umeme, wezi wa mafuta ya transfoma pamoja na nyaya za umeme... nitoe wito kuwa mtu anayefanya matendo haya ni kuhujumu uchumi, hivyo atakapokamatwa ni lazima ashtakiwe kwa kuhujumu uchumi na wananchi tunaomba ushirikiano katika kuwabaini watu hawa," alisema Mghwira.

Kwa upande wake, Mhandisi Mkaka alisema umeme unaozalishwa katika mkoa wa Kilimanjaro ni megawati 135, ambapo matumizi kwa mkoa mzima kwa sasa ni megawati 42.

Alisema kuwa, kwa miundombinu iliyowekezwa na shirika hilo katika mkoa, ina nafasi ya kutosha ya ziada hata kama wawekezaji wa viwanda wakija kuwekeza ndani ya mkoa huo hawatapata changamoto ya kukatika kwa umeme.

Alisema kuwa kuwa changamoto ambayo shirika hilo inaipitia kwa sasa ni uwapo wa madeni makubwa kwa wateja wake zikiwamo taasisi za umma ambapo wamekuwa wakizikatia huduma.

Alisema changamoto nyingine ni ulinzi wa miundombinu ya shirika hilo ambapo baadhi ya watu wasio waaminifu wamekuwa wakiharibu miundombinu, wakiiba nyaya za umeme mafuta ya transfoma, huku wengine wakiiba vyuma na wizi wa umeme.




Ukurasa 15

**Dk. Bashiru anapowachoka wenye uchu mali za chama**

## DRC na 'safari ya matumaini' kujiunga na EAC



Ukurasa 18




Ukurasa 20

**Mkutano wa amani Bahrain, Kushner kafaulu au kawama?**


# siasa

JUMATANO JULAI 3, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**Homa ya uchaguzi yachanganya wabunge katika nchi ya Kenya**

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-3

MZEE Pius Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia ni mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Vilevile, Mzee Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu la kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa.

Wiki iliyopita tuliwaletea sehemu ya pili ya mfululizo wa kitabu hiki ambapo tuliishia kipengele cha 2.2 Haja ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hizi mbili. Sasa fuatilia kuanzia kipengere kinachofuata:

2.3. Kuimarisha udugu wa karibu uliokuwapo baina ya wananchi wa nchi hizo mbili

Tukirejea hotuba ya Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokuwa akiwahutubia wabunge

INAENDELEA UK.16



Mzee Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

**Rwanda, Uganda zinavyotishia amani, utengamano wa EAC** Ukurasa 19

# Homa uchaguzi yachanganya wabunge katika nchini Kenya



Naibu Rais wa Kenya, William Ruto. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

WABUNGE nchini Kenya wanaonekana kuingiwa na kiwewe kuhusu kitakachotokea katika uchaguzi mkuu ujao licha ya kuwa kuna takriban miaka mitatu kabla vibanda vya kupigia kura havijafunguliwa.

Moja ya maeneo ambako kiwewe kimefikia hatua za kutisha ni ukanda wa kati nchini humo ambao ni ngome ya chama tawala cha Jubilee na wabunge wa eneo hilo wako njia panda kati ya kumuunga mkono Rais Uhuru Kenyatta ambaye sasa anashirikiana kwa karibu na kiongozi wa upinzani Raila Odinga.

Baadhi wanaendelea kumsikiliza Naibu Rais William Ruto.

Tatizo ni kuwa kwa wabunge wa ukanda wa kati nchini Kenya, suala la Ruto kuwa mrithi wa Kenyatta kama mgombea ni la kugombea uhai wa Jubilee, kwani kitasimama wima endapo kitaendelea kumtii Ruto, na kikiondoka kwake kama Uhuru anavyotaka, haijulikani nini mpangilio wa utii kisiasa utakavyokuwa.

Licha ya kuwa utii kwa Uhuru na Raila una nguvu, bado siasa za chini kwa chini eneo hilo zinampa tafu zaidi Ruto, kwani Uhuru hawezi kusimama kwa muhula wa tatu, na ukanda huo haumtaki Raila.

Suala la umakamu wa Uhuru linapwaya.

Bado uchunguzi unaendelea katika vyombo vya usalama na kujitafuta katika vyombo vya habari kama ni kweli kuwa Naibu Rais alitishiwa kuuawa, kwa sababu habari hizo alizitoa yeye mwenyewe, akinyooshea kidole mikutano ya mawaziri na wabunge kujadili maendeleo ya maeneo yao kikabila au kikanda.

> Licha ya kuwa utii kwa Uhuru na Raila una nguvu, bado siasa za chini kwa chini eneo hilo zinampa tafu zaidi Ruto, kwani Uhuru hawezi kusimama kwa muhula wa tatu, na ukanda huo haumtaki Raila.

Kwa vile mjadala kama huo lazima uguse suala la utii wa eneo husika katika uchaguzi mkuu ujao, Naibu Rais anaona kana kwamba ni vikao vya kumjadili yeye, halafu anaongeza kwa kuna mpango wa kumuua.

Uthibitisho wa fununu hizo bado haukuwa wazi, lakini kwa siasa za Kenya anazozifahamu fika Ruto, tishio hilo si la kupuuzia.

Mara nyingi katika nchi zenye mchanganyiko wa demokrasia na uimla wa chama kimoja, tishio kwa dola linakuwa halitoki upinzani moja kwa moja ila kwa mwanasiasa wa chama tawala ambaye jina lake linavuruga mpangilio au matazamio ya wasimamizi wa dola.

Hivyo ndivyo alivyouawa Dk. Robert Ouko akiwa Waziri wa Mambo ya Nje mwaka 1990 au Profesa George Saitoti aliyewahi kuwa Makamu wa Rais awamu ya pili ya Rais Daniel arap Moi, aliyefariki kwa ajali ya gari mwezi Juni 2012, kuondoa sehemu ya ushindani iwe ni wa kumrithi Rais Mwai Kibaki au kupata mgombea mwenza anayefaa.

Awamu zote Kenya wanasiasa wanaovuruga wamepata ajali au kupigwa risasi, kuanzia miaka ya 1960 na 1970 ambako walikufa wengi zaidi, na hata wakati wa kipindi cha vyama vingi, kwa mfano kufariki Waziri wa Mambo ya Ndani Jenerali Joseph ole Nkaissery mwezi Julai 2017, miezi michache kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu.

Maswali kama nani kamwondoa Jenerali ole Nkaissery yaliulizwa, kwani ilidhaniwa aliwekewa sumu ikamwua.

Inaelekea kuwa Naibu Rais yeye binafsi anaamini alichokisema kwani kuanzia atoe tangazo hilo anaonyesha dalili za kurudi nyuma katika kampeni zake.

Alitoa tamko siku chache baadaye kuwa watu wasiendelee na ubishi kuhusu uchaguzi mkuu ujao na badala yake waelekeze nguvu zao katika juhudi za maendeleo, mwelekeo ambao unafanana na ule ambao Uhuru amekuwa nao kwa miezi kadhaa akimtaka Ruto kufuata.

Ilibidi hata aondolewe kama msimamizi wa miradi mikubwa katika baraza la mawaziri, awekwe Dk. Fred Matiang'i, Waziri wa Mambo ya Ndani.

Ikafikia hatua ambako Ruto anasisitiza kuwa hajaanza kampeni kuwania urais katika uchaguzi mkuu ujao, wakati ajenda yake tangulizi katika miezi sita hadi mwaka mmoja uliopita ni kujua 'nani ni nani' katika chama cha Jubilee, hasa wabunge, magavana wa 'kaunti' na maseneta wa Jubilee wamesimama wapi kwa suala hilo.

Vyombo vya habari vimekuwa vikifuatilia na kwa dalili za mwezi mmoja au zaidi kidogo uliopita, ilielekea kuwa Ruto anaungwa mkono kwa nguvu maeneo mengi ya ukanda wa kati, na Uhuru aliwafokea baadhi ya wakosoaji wake, ambao wanadai anapeleka maendeleo kwingine akisema ni 'wapumbavu.' Lipo tishio la kumgeuka Ruto.

Wakati wabunge wa ukanda wa kati wanapigana na vivuli vya utii na uasi kwa Naibu Rais, yupo mbunge mmoja mwanamuziki akaamua kuingiza siasa za aina nyingine, zile za Afrika Kusini za kuwapiga na kuwafukuza wageni kutoka kwingineko Afrika wanaofurahia uchumi bora zaidi wa nchi hiyo.

Alitoa rai katika 'instagram' kuwa wageni wanaofanya biashara jijini Nairobi hasa kutoka nchi za jirani watapewa saa 24 kuondoka, na wasipofanya hivyo watafurumishwa.

Ikawa zogo kote Afrika Mashariki hasa katika Baraza la Kutunga Sheria la Jumuiya (EALA), ambako Kenya ilipeleka waziri kukanusha na kimsingi kuomba radhi kuhusu tamko hilo. Ila ni ishara.

Tamko hilo la mbunge mwanamuziki anayefahamika kwa jina la kisanii la 'Jaguar,' mojawapo ya aina za chui, lilizua woga kuwa anachosema licha ya kuwa kina chembe ya mzaha kwani ni 'rapa' lakini ni kutoka kwa wasanii kama hao ambako upinzani wa nguvu unazaliwa Afrika siku hizi.

Kuna msanii wa kisiasa aitwaye Julius Malema nchini Afrika Kusini aliyekuwa kiongozi Umoja wa Vijana wa ANC na anapenda kujitambulisha kwa kuvaa 'combat,' hasa kofia ya kijeshi.

Amepata mrithi wake eneo la Afrika Mashariki kwani yupo msanii Robert Kyagulanyi Sentamu, rapa nchini Uganda ambaye pia ni mbunge, na ni mpinzani wa jino kwa jino na mpango wa Rais Yoweri Museveni kufuta ukomo wa umri katika kugombea urais, baada ya kufuta ukomo wa mihula miaka iliyotangulia. Yeye na Museveni wanaparurana kama watani.

Mzaha kama huo hata hapa upo lakini haujachukua nafasi kubwa katika siasa nchini, lakini vipo vianzio vya viongozi vijana wanaojiamini kuwa ni watu wa kizazi kipya na wana uwezo mkubwa zaidi wa kufanya au kutoa rai ya kile wanachokitaka.

Mara nyingi zaidi wanatoa rai hizo ndani ya wigo mpana wa vyama vya siasa, ila kuna aina fulani ya 'personal style,' muhuri wa mwelekeo binafsi wa mwanasiasa husika, kwa mfano wabunge wa upinzani na matamshi yaliyowahi kuleta mizozo wakati uliopita.

Enzi za awamu ya nne walikuwa wakiongea lolote kwa kujisikia, ikafikia mahali umaarufu wao ukavuka mpaka wakaanza kuitishia CCM.

Kuongezeka kwa kiwango cha 'personal style' katika siasa ni kielelezo kuwa mifumo inapwaya na baadhi ya wanaojihisi kuwa wanapendwa binafsi watoke katika 'kisanduku' cha usimamizi wa mawazo na kutoa rai, waunde jukwaa tofauti ili kuweza kuwafikia watu.

Ni kuvuruga mpangilio wa utii kwani unakuwa hauna tija kwa kile kinachotafutwa, kwa mfano Kyagulanyi ni mfuasi wa Democratic Party nchini Uganda lakini haelekezi nguvu zake zote kukijenga chama hicho ila kujenga harakati mpya yake binafsi.

Mbunge 'Jaguar' anaweza kuwa ni mfuasi kwa kiwango fulani wa Rais Donald Trump wa Marekani na siasa kali za kuzuia uhamiaji usio wa kisheria, lakini matamshi yanaendana zaidi na mazingira ya Afrika Kusini ya kuwabebesha wageni lawama ya kuvuruga matumaini ya wenyeji kwa kupora ajira ndogo ndogo, na hata mabinti kwani wakiwa na mishahara wanasikilizwa, na si walalahoi wazalendo.

Ni sumu kama hisia hiyo ikipandikizwa na kuanza kufanya kazi, wakaa vijiweni waonyeshwe adui ni nani.... )

# Dk. Bashiru anapowachoka wenye uchu mali za chama

- Aagiza washughulikiwe kuepusha migogoro
- Akemea tabia ya kulindana na kukingiana kifua

Na Sabato Kasika

MWISHONI mwa wiki iliyopita, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, alikutana na wanachama wa chama hicho wa Wilaya ya Ubungo Dar es Salaam na kufanya nao mkutano.

Katika mkutano huo, Dk. Bashiru alibainisha kuwa ana taarifa kwamba kuna migogoro ya viongozi wa chama hicho wanaogombea mali za chama na kuagiza tatizo hilo lishughulikiwe.

Dk. Bashiru katika maelekezo yake, anataka wanachama wa aina hiyo wasivumiliwe bali watimuliwe, kwa kuzingatia kwamba chama hicho hakina uhaba wa wanachama.

"Kila mwanachama ana haki ya kuongoza, hivyo hizo tabia za kulindana na kukingiana kifua zimesababisha chama kufikia hapa kilipo... mali za chama zinatakiwa kulindwa na kutunzwa," anasema Dk. Bashiru.

Anabainisha kwamba mtindo wa baadhi ya viongozi kugombea mali za chama na wakati mwingine kuzikwapua haukubaliki na unasababisha watu wenye nia njema ya kujitolea kusaidia chama kukata tamaa.




Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally. **PICHA: MTANDAO**

### MAKONDOKANDO

Kwa maelezo hayo ya Dk. Bashiru ni kwamba licha ya juhudi zote za kuimarisha chama zinazofanywa na viongozi wa juu, bado kuna wanachama wachache wanaoifanya CCM iwe na makandokando.

Katika juhudi za kupambana na makondokando ndani ya chama, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), John Magufuli aliunda tume ya kuhakiki mali za chama, iliyoongozwa na Dk. Bashiru Ally.

Tume hiyo ya watu tisa iliundwa mwishoni mwa mwaka 2017 ikiwa na jukumu la kufuatilia na kuhakiki mali za Chama Cha Mapinduzi (CCM) kote nchini baada ya kubainika kuwa zinanufaisha wajanja wachache.

Mwenyekiti huyo aliunda tume hiyo ikiwa ni utekelezaji wa dhamira ya kupiga vita rushwa na ufisadi, kwa vile anaamini kwamba hawezi akaanza kupiga vita rushwa na ufisadi ndani ya serikali wakati chama kina rushwa na ufisadi.

Anasafisha chama ili kiachane na mambo ya rushwa na ufisadi na hivyo Tanzania isonge mbele.

Kwa hiyo hao wanaodaiwa kugombea mali za chama, ina maana kwamba hawajajua nia ya viongozi wao wa juu ya kumaliza makondokando. Kama kweli viongozi wa aina hiyo wapo ndani ya chama na wanaendelea kulindana, wanakiharibia chama ambacho kimeamua kujiweka kando na kila aina ya mambo ambayo yanakwenda kinyume na utaratibu.

### MIRADI YA CCM

Dk. Bashiru anatolea mfano mkoa wa Dar es Salaam kuwa CCM ina miradi, ambayo inaweza kujiingizia Sh. bilioni tano kwa mwaka na kuifanya ijiendeshe yenyewe kwa ufanisi.

Hata hivyo, katibu huyo anasema anaumizwa na baadhi ya watu wasiotaka utaratibu wa malipo uliopo anaoutaja kwa jina la 'control number.'

"Hapa ninamaanisha kwamba wapo baadhi ya viongozi, ambao hawafuati mfumo uliowekwa wa kutumia control number. Yaani hawalipi kwa kutumia mfumo huo, matokeo yake fedha zinatumika kiholela," anasema.

Anasema chama kitaendelea kukemea vitendo vichafu vikiwamo hivyo, ambavyo vinasababisha wananchi wakione kama hakiko imara, kumbe ni kwasababu ya watu wachache wanaopaswa kushughulikiwa.

> "CCM imejiimarisha na inaendelea kujiimarisha zaidi, hivyo haiwezi kuwavumilia watu wenye nia ya kuifanya isiaminike mbele ya umma wa Watanzania.

"CCM imejiimarisha na inaendelea kujiimarisha zaidi, hivyo haiwezi kuwavumilia watu wenye nia ya kuifanya isiaminike mbele ya umma wa Watanzania," anasema.

Dk. Bashiru anasema chama hicho kinapambana kwa dhati na kila aina ya vitendo viovu vikiwamo vya rushwa, ambavyo CCM Mpya na Tanzania Mpya haitaki kuvikumbatia.

### CCM MPYA, TANZANIA MPYA

Katibu wa Itikadi na Uenezi Taifa, Humphrey Polepole, anasema viongozi wa CCM wameshaeleza fikra na mipango yao na tayari wameanza kusimamia na kutekeleza ajenda ya mageuzi ndani ya chama, ambayo msingi wake ni kuirejesha CCM kwa watu

"Msimamo wa kufanya mageuzi kwenye CCM ni kukirudisha kwenye misingi, ambayo chama kilianzishwa, kwa maana ya chama cha wanyonge wakiwamo wakulima na wafanyakazi," anasema Polepole.

Hapa anamaanisha kwamba kinachoendelea sasa ni kufanya kazi kwa bidii kwa kutumikia wananchi, kwa vile Watanzania bado wana matumaini kwa chama hicho tawala. Anasema kinachotakiwa ni wanachama kuendelea kuheshimu maelekezo ya viongozi na kutimiza wajibu wao inavyotakiwa ili chama kizidi kukubalika mbele ya umma wa Watanzania.

"Chama Cha Mapinduzi kinachapa kazi na kinaendelea kuchapa kazi, na dhamira ya kujenga Tanzania Mpya inaakisiwa na kuleta CCM Mpya, ambayo ni kimbilio la Watanzania wengi," anasema.

### USHIRIKIANO VITANI

Binafsi naamini kwamba kila mwana CCM anapaswa kushiriki katika kufanikisha dhana ya CCM Mpya na Tanzania Mpya badala ya kudhani kwamba vita ya kupinga uovu ndani ya chama ni ya viongozi wa juu.

Kwa ushirkiano wa wanachama wote kuna uwezekano mkubwa wa kukomesha vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikipigiwa kelele kwa muda mrefu na viongozi wa chama.

Mwenyekiti wa CCM anaamini kwamba kwa Mtanzania mwaminifu kwa imani yake hatakuwa na kigugumizi cha kuwa mstari wa mbele kupambana na rushwa na ufisadi.

Hii ingekuwa ni imani ya kila mwanachama wa CCM na hata Watanzania kwa ujumla wao ili waweze kutoa mchango katika kupambana na vitendo hivyo vinavyowanyima haki wanyonge.

Vitendo hivyo vikikomeshwa hakutakuwa na kulindana wala kukingiana kifua na kusababisha chama kionekane hakifai, kumbe ni watu wachache walioamua kuziba masikio ili wasisikie maonyo.

Kwa hali hiyo sasa ni vyema wale ambao bado hawajatambua kuwa wako ndani ya CCM Mpya, wabadilike na kuchukua hatua za kubadilika haraka wasije kujikuta wanaingia kwenye anga za Dk. Bashiru.

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-3



Sehemu ya Gwaride la kusherehekea kumbukumbu ya Siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

wa Bunge la Tanganyika tarehe 25 Aprili 1964, alisema hivi:

"Tanganyika na Zanzibar ni nchi ndugu. Tunashirikiana kwa historia, lugha, mila tabia na siasa. Udugu wa Afro- Shirazi Party na TANU wote mnaufahamu. Udugu wa viongozi wa vyama hivi viwili haukuanza jana. Basi, tunazo sababu zote hizo za kutufanya tuungane na kuwa kitu kimoja. Juu ya yote hayo, kuna shauku ya Umoja wa Bara la Afrika. Basi, kwa kuzingatia yote hayo, mimi, kwa niaba yenu, na Rais Karume kwa niaba ya ndugu zetu wa Unguja na Pemba, tulikutana Unguja siku ya tarehe 22 mwezi huu, tukatia saini mkataba wa umoja baina ya nchi zetu mbili.

Mnao Mkataba huu na mtaujadili. Endapo bunge hili, pamoja na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, yataukubali mkataba huu, nchi zetu zitakuwa nchi moja. Siyo nia yangu kueleza Mkataba wenyewe. Mtaelezwa wakati wa majadiliano. Kazi yangu ni kuwaombeni muukubali Mkataba huu."

Kutokana na maneno hayo ya Mwalimu Nyerere, tunaona wazi kwamba, kuimarisha udugu uliokuwapo baina ya wananchi wa Tanganyika na Zanzibar, lilikuwa ni lengo mojawapo katika malengo makuu ya kuanzishwa kwa Muungano huu.

> Mkataba huo haukuweka sharti lolote la kutaka uthibitishwe na wananchi wote kwa kura za maoni (referendum). Ndiyo sababu zoezi hilo halikufanyika.

## SURA YA 3 MAZINGIRA YALIYOTAWALA UJIO WA MUUNGANO HUU

3.1 Mchakato ulivyokuwa hadi Kufikia Kusainiwa kwa Mkataba wa Muungano

Jambo kubwa la kuzingatia kuhusu mchakato huo, ni usiri mkubwa uliokuwapo katika mchakato wenyewe. Lakini, usiri huo ulikuwa na sababu nzuri.

### 3.2 Sababu za Usiri Uliogubika Mchakato huo

Sababu yake ya msingi ilikuwa ni hofu ya mchakato huo kuhujumiwa na maadui wa Muungano huu. Marais Julius Nyerere na Abeid Karume, wote wawili walikuwa na hofu kwamba, endapo lengo lao la kuunganisha nchi hizi mbili litajulikana mapema, maadui wa muungano huo watapata nafasi ya kufanya hujuma za kukwamisha lengo hilo lisifikiwe.

Na kweli, dalili za hujuma zilipata kujitokeza katika siku za mwishomwisho wa mchakato huo, ambapo ilitengenezwa fitina ya maneno ya uwongo yaliyosambazwa wakati Rais Karume alipokuja Dar es Salaam kwa ajili ya kukamilisha mipango ya kusainiwa kwa Mkataba wa Muungano. Gazeti la "TANU The Nationalist" lilikuwapo nyakati hizo, lilifichua fitina hiyo katika toleo lake la tarehe 20/04/1964, kwa kuchapisha uvumi uliozagaa kwamba, 'Rais Karume na familia yake wamekwenda kuishi Tanganyika.'

Ilibidi Waziri wa Mambo ya Nje, Oscar Kambona akanushe uvumi huo kwa kusema kwamba, "Rais Karume alifika Dar es Salaam kuzungumza na Rais Nyerere na kwamba, mazungumzo yao yalijikita katika kuimarisha urafiki wa nchi hizi mbili, pamoja na uhusiano kati ya TANU na Afro - Shirazi Party."

Waziri Kambona alinukuliwa na gazeti hilo akiendelea kusema kwamba, "Rais Karume anaamini katika Umoja wa Afrika, na Zanzibar itafurahi kuona Serikali ya Afrika hatimaye imeundwa, ambayo ndiyo vilevile ndoto ya Tanganyika."

Lakini, kwa lengo la kutunza siri, Waziri Kambona alificha ukweli kwamba, mazungumzo ya Marais hao yalihusu kuunganisha Tanganyika na Zanzibar.

Aidha, kwa lengo hilohilo la kutunza siri, hata siku yenyewe ya tarehe 22/04/1964 ambayo Rais Nyerere alikwenda Zanzibar kuweka saini yake katika Hati ya Mkataba wa Muungano, bado gazeti la The Nationalist lilieleza kwamba "Rais Nyerere alikwenda Zanzibar kwa ziara ya kirafiki katika Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, ambako alionana na Rais Karume, ikiwa ni ziara yake ya kwanza Zanzibar tangu Serikali mpya ya Mapinduzi ilipotwaa madaraka."

Gazeti hilo pia, lilinukuu maelezo ya Salim Rashid, aliyekuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi, aliyesema kwamba, "tumemkaribisha Nyerere kuzuru Zanzibar kwa moyo mkunjufu, kwani watu wa nchi zetu hizi mbili wakati wote wamekuwa marafiki na wenye ukaribu mno. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, ni jambo zuri kwa viongozi wetu wakuu kukutana mara kwa mara kujadili matatizo yetu yanayofanana. Hii ni ziara ya kwanza na nyeti ya Rais Nyerere tangu Mapinduzi."

Hatimaye siri yenyewe ilikuja kufichuliwa jioni ya tarehe hiyo 22 Aprili, 1964, (baada ya Mkataba wa Muungano kuwa tayari umesainiwa). Siri ilifichuliwa kwa njia ya Taarifa rasmi ya Serikali, ambayo ilitolewa na Ikulu mjini Dar es Salaam, iliyotangaza kwamba:

"Rais Julius Nyerere wa Jamhuri ya Tanganyika na Rais Abeid Karume wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, leo wamesaini Mkataba wa Makubaliano (Articles of Union ) ya kuunda Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar. Makubaliano hayo ni sharti yaridhiwe na Serikali zote mbili, pamoja na Mabunge ya nchi zote mbili."

Hata mazungumzo baina ya Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar juu ya suala hili, yalibaki kuwa na siri ya Waasisi hao wawili hadi walipofikia hatua ya kusaini Mkataba wa Makubaliano ya Muungano, kutokana na sababu za msingi zilizoelezwa hapo juu.

Lakini, mchakato haukuishia hapo. Kwani, ili Mkataba huo upate uhalali wa kisheria, na kama ilivyokuwa imeelekezwa katika kifungu kidogo cha (viii) cha Mkataba huo; ilibidi uridhiwe (ratified) na vyombo vya uwakilishi vya nchi hizi mbili, ambavyo wakati huo vilikuwa ni Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar. Kama tulivyokwishakueleza, kazi hiyo ilitekelezwa ipasavyo na vyombo hivyo viwili siku ya Jumamosi tarehe 25 Aprili, 1964; ambapo Baraza la Mapinduzi la Zanzibar lilitangulia kwa kufanya kikao chake asubuhi ya siku hiyo, na Bunge la Tanganyika likafuatia kwa kikao kilichofanyika mchana wa siku hiyohiyo.

Mkataba huo haukuweka sharti lolote la kutaka uthibitishwe na wananchi wote kwa kura za maoni (referendum). Ndiyo sababu zoezi hilo halikufanyika.

### 3.3 Mazingira ya kuzaliwa kwa Muungano wenyewe

Kama nilivyokwishaeleza, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulizaliwa tarehe 26 Aprili, 1964. Lakini, kuzaliwa kwake hakukuambatana na shamrashamra au sherehe za namna yoyote. Bila shaka, hii ilitokana na usiri mkubwa uliokuwapo wakati wote wa maandalizi yake, kwani hata yale mapatano yaliyosainiwa tarehe 22 Aprili, 1964, hayakutaja tarehe ya kuanzishwa rasmi kwa Muungano, bali yalisema tu kwamba, maisha ya Muungano huu yataanza rasmi" siku itakayofuata mara baada ya kuridhiwa kwake." Kwahiyo basi, kwa kuwa taratibu za kuridhiwa kwake zilikamilika tarehe 25 Aprili,1964 , na maisha yake yakaanza rasmi siku iliyofuata , yaani, tarehe 26 Aprili 1964, hapakuwa na muda wa maandalizi ya kufanya sherehe zozote. Ndiyo sababu siku hiyo ilipita kimyakimya tu, bila kuwa na sherehe za aina yoyote za kuadhimisha kuzaliwa kwa Muungano huu. Na kama tulivyokwishakuona, shughuli zote zilizoambatana na tukio hilo, zilifanyika na kumalizikia ndani ya Bunge tu; yaani: Mkataba wa Mapatano ya Muungano ulidhiriwa siku ya Jumamosi tarehe 25 Aprili,1964. Kesho yake, Jumapili tarehe 26 Aprili, 1964, Jamhuri ya Muungano ikazaliwa rasmi, ikiwa ni pamoja na vyombo vipya vya utawala na uongozi wa Jamhuri hiyo mpya. Siku iliyofuata, yaani, Jumatatu tarehe 27 Aprili,1964, ilikuwa ndiyo siku ambapo Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano lilipoanza kazi, kwa kuapishwa kwa Wabunge wapya walioteuliwa na Rais kuiwakilisha Zanzibar katika Bunge hilo la Jamhuri ya Muungano; pamoja na aliyekuwa Rais wa Tanganyika Mwalimu Nyerere, na aliyekuwa Rais wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume, kubadilishana HATI zilizosainiwa na Mapatano ya kuanzishwa kwa Muungano huu. Lakini, nje ya Bunge, hapakuwa na sherehe nyingine zozote. Ndiyo sababu mimi binafsi, nikiwa Katibu wa Bunge wakati huo, nilibahatika kushuhudia matukio hayo makubwa, na ya kihistoria, yakitokea ndani ya ukumbi wa Bunge, Karimjee Hall, Dar es Salaam.



Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere (aliyekaa kushoto), akitia saini Makubaliano ya Mkataba wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume (aliyekaa kulia). **PICHA: MTANDAO**

### 3.4 Madai kwamba Zanzibar haikuwahi kuridhia Mkataba wa Muungano

Katika Sura ya Tano, nitazungumzia kwa kina zaidi kuhusu suala la changamoto ambazo zimeukumba Muungano wetu katika nyakati mbalimbali za uhai wake. Ni jambo la kumshukuru Mungu kwamba, licha ya changamoto hizo, Muungano wetu haujatetereka kiasi cha kutishia kuendelea kuwapo kwake. Miongoni mwa matatizo yaliyowahi kujitokeza kuhusu Muungano huu, ni madai ambayo yamekuwa yakiibuliwa na baadhi ya viongozi wa Zanzibar, waliopo na waliokwishakustaafu, kwamba, eti hakuna kumbukumbu zinazoonesha kuwa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar liliridhia Mkataba huo wa Muungano.

Madai haya yanashangaza sana kwani, kama ilivyokwishaelezwa, ni kwamba, Kikao cha Baraza la Mapinduzi la Zanzibar kilifanyika asubuhi ya tarehe 25 Aprili, 1964, kwa madhumuni hayo tu ya kuridhia Mkataba huo. Baadaye, sheria inayoitwa "The Union of Zanzibar and Tanganyika Law" ilichapishwa katika Gazeti la Serikali ya Muungano la tarehe 1 Mei 1964, kama Government Notice (GN) no. 243; ikiwa na maelezo kwamba, sheria hiyo ilipitishwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar tarehe 25 Aprili,1964.

Kwahiyo, kwa muda wote wa miaka zaidi ya hamsini iliyopita ya Muungano huu, tumechukulia sheria hiyo kuwa ni ushahidi tosha unaothibitisha kwamba, Baraza la Mapinduzi liliridhia Mkataba wa Muungano kwa kutipisha sheria hiyo.

### 3.5. Utengenezaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano

Nchi yoyote inayotambulika hivyo, sharti iwe na Katiba yake. Ndiyo sababu kabla ya Muungano, Tanganyika ilikuwa na Katiba yake, na Zanzibar pia ilikuwa na Katiba yake, ambayo ilitungwa mara baada ya Mapinduzi ya Januari 1964 yaliyoondoa utawala wa Sultani uliokuwa umewekwa mwezi Desemba 1963, wakati Zanzibar ilipopata uhuru wake.

Baada ya kuunganisha nchi hizi mbili na kuunda nchi moja mpya, ambayo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilibidi itungwe Katiba mpya ya nchi hiyo mpya. Utekelezaji wa kazi hiyo uliongozwa na Mkataba wa Makubaliano ya Muungano, uliokuwa umetoa maelekezo yafuatayo:

- Kwamba, kuwe na kipindi cha mpito cha mwaka mmoja kabla ya kutunga Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano.
- Kwamba, katika kipindi hicho cha mpito, Jamhuri ya Muungano itatawaliwa na Katiba ya muda.
- Kwamba, Katiba ya Tanganyika itakuwa ndiyo Katiba ya muda ya Jamhuri ya Muungano, ikiwa imefanyiwa marekebisho ya kuwezesha kuwapo kwa;
- Serikali ya Zanzibar, pamoja na Baraza la Kutunga Sheria la Zanzibar, kwa ajili ya kushughulikia mambo ya ndani ya Zanzibar ambayo siyo mambo ya Muungano;
- Makamu wa Rais wawili, mmoja akiwa ni mshauri mkuu wa Rais kwa mambo yanayohusu Tanganyika na mwingine akiwa ni mshauri mkuu wa Rais kwa mambo yanayohusu Zanzibar.
- Uwakilishi wa Zanzibar katika Bunge la Muungano; na
- Mambo yoyote mengine ambayo yataonekana kuwa yanafaa na yanahitajika kwa ajili ya uendeshaji bora wa Jamhuri ya Muungano.

### 3.6 Suala nyeti la 'Serikali mbili'

Kifungu kidogo cha (iii)(a) cha Mkataba huu wa Makubaliano ya Muungano ndicho kilichoweka mfumo wa Serikali mbili, yaani, Serikali ya Muungano, na Serikali ya Zanzibar. Jambo hili lilikuja kuwekwa wazi zaidi na sheria inayoitwa "The Interim Constitution of the United Republic of Tangayika and Zanzibar, 1964" iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 1 Mei, 1964, kama Government Notice (GN) no. 246, ambapo, kifungu chake cha 4 kiliweka sharti kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na madaraka juu ya mambo ya Muungano katika Jamhuri nzima ya Muungano, yaani, upande wa Tanganyika na pia upande wa Zanzibar; na vilevile, juu ya mambo mengine yote yasiyokuwa ya Muungano kwa upande wa Tanganyika. Huu ndio unaitwa "Muundo wa Serikali mbili," ambao baadaye uliingizwa kwenye Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilipotungwa mnamo mwaka 1977; lakini, kama tutakavyoona baadaye katika Sura inayofuata, umesababisha mjadala usiokwisha hadi sasa.

> Bunge la Jamhuri ya Muungano lilipitisha Sheria iliyoruhusu kuahirishwa kwa utekelezaji wa masharti yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (viii) cha Mkataba wa Makubaliano ya Muungano.

### 3.7 Kipindi cha mpito chaongezwa

Kifungu kidogo cha (vii) cha Mkataba wa Makubaliano ya Muungano kilikuwa kileelekeza kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar, ndani ya kipindi hicho cha mpito cha mwaka mmoja kuwa;

- atateua Tume ya Katiba itakayopewa jukumu la kuandaa mapendekezo ya Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano, na
- ataitisha Bunge maalum la Katiba (Constituent Assembly), lenye wajumbe kutoka Tanganyika na wengine kutoka Zanzibar, kwa ajili ya kutunga Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano.

Wahenga walisema kwamba "mpango si matumizi" na kweli hivyo ndivyo ilivyotokea kuhusu jambo hili. Kipindi cha mpito cha mwaka mmoja kilikuwa kinamalizika tarehe 26 Aprili, 1965. Lakini, tathmini ya Marais hao wawili ilibainisha kwamba ulihitajika muda zaidi wa kipindi cha mpito, kabla ya kufikia hatua ya kutunga Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano. Kwahiyo, mnamo mwezi Machi mwaka 1965, yaani, mwezi mmoja kabla ya kumalizika kipindi hicho cha mpito, Bunge la Jamhuri ya Muungano lilipitisha Sheria iliyoruhusu kuahirishwa kwa utekelezaji wa masharti yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (viii) cha Mkataba wa Makubaliano ya Muungano, "hadi wakati mwingine baadaye, ambao utaamuliwa na Marais hao, kama watakavyoona wenyewe kuwa inafaa."

Kwahiyo, Jamhuri ya Muungano iliendelea kutawaliwa na Katiba ambayo awali ilikuwa ni Katiba ya Tanganyika, kama ilivyorekebishwa kulingana na maelekezo ya Mkataba wa Mapatano ya Muungano, na kama ilivyorekebishwa tena mwaka 1965, kwa kuifanya iwe ni Katiba ya Chama kimoja cha siasa, hadi kufikia mwaka 1977, ilipotungwa Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**ITAENDELEA**

# DRC na 'safari ya matumaini' kujiunga na Jumuiya ya EAC



Rais John Magufuli (kulia), akimtambulisha Rais Felix Tshisekedi wa DRC kwa maofisa waandamizi wa Serikali alipofanya ziara nchini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

NI dhahiri kwamba Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) inayoongozwa na Rais Felix Tshisekedi, imedhamiria kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), yenye nchi wanachama sita.

Nchi hizo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan Kusini ambazo kwa sehemu zimepakana na taifa hilo lenye utajiri wa madini yanayokisiwa kuwa na zaidi ya aina 1,100.

Barua ya Rais Tshisekedi aliyomwandikia Mwenyekiti wa EAC, Rais Paul Kagame Juni 8 mwaka huu, kauli yake na ile ya Rais John Magufuli kuhusu Tanzania kuunga mkono kusudio la DRC ni miongoni mwa vielelezo vinavyoashiria utayari wa nchi hiyo kuwa mwanachama wa EAC.

Tayari Rais Kagame ameshawasilisha maombi hayo kwa Sekretarieti ya EAC ili yajadiliwe katika mkutano wa wakuu wa nchi wanachama utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Akizungumza kwenye hafla aliyomuandalia Rais Tshisekedi, Rais Magufuli alisema Tanzania inatambua uhusiano wa kihistoria uliopo kati ya nchi mbili hizo na kwamba itakuwa tayari kuunga mkono maombi yake (DRC) ya kujiunga EAC.

> Hatua ya DRC kuingia EAC italiwezesha taifa hilo kujiunga katika miradi ya pamoja kama ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Akiwa nchini Tanzania, Rais Tshisekedi alisema nchi yake inatamani kuwa mwanachama wa EAC ili pamoja na mambo mengine, kukuza fursa za masoko, biashara, uchumi na kuimarisha hali ya utulivu kwenye ukanda huo.

Rais Magufuli alisema takwimu za mwaka jana zinaonyesha kuwa DRC na Tanzania zinafanya biashara yenye thamani ya Sh. bilioni 305 wakati uwekezaji wa nchi hiyo kwa Tanzania ukiwa ni Dola milioni 5.77 uliozalisha ajira 418.

Pia DRC imekuwa ikiitumia bandari ya Dar es Salaam kwa kupitisha mizigo yake inayokadiriwa kuwa tani milioni 1.18, hivyo kuibua umuhimu wa kuondoa vikwazo vya biashara kwa nchi hizo.

### KWA NINI DRC KUINGIA EAC

Zipo sababu nyingi zinazotumika kama kigezo kwa DRC kutaka kuwa mwanachama wa EAC, miongoni mwa hizo ni kukuza na kuendeleza uhusiano uliopo katika nyanja tofauti na mataifa yaliyo mwanachama wa EAC.

Itakumbukwa kwamba katika mkutano wa kimataifa wa wawekezaji uliofanyika jijini Kigali, Rwanda hivi karibuni, Rais Tshisekedi alishiriki na kuelezea fursa nyingi zilizopo nchini mwake, lengo likiwa ni kuwavutia wawekezaji zaidi.

Lakini pia ni kwamba DRC inapakana karibu na nchi zote za EAC kiasi kwamba miongoni mwa hizo zimewahi kuwa katika uhusiano mbovu wa kidiplomasia unaotokana na madai ya kusaidia vikundi vya wanamgambo na wizi wa madini nchini humo.

Johnson James ni mtaaluma wa uhusiano wa kimataifa, anasema ingawa DRC ipo kwenye jumuiya nyingine kama ilivyo kwa baadhi ya wanachama wa EAC, lakini kuingia katika ukanda huo (Mashariki), kutainufaisha kwa karibu na haraka.

"Kwa mfano DRC ni mwanachama wa SADC kama ilivyo Tanzania, lakini hauwezi kuyaona manufaa ya nchi nyingine ya SADC kama Lesotho kwa mfano, kuwa na athari za karibu na moja kwa moja kwa Tanzania ama nchi nyingine za EAC," anasema.

Anasema kama DRC ikifanikiwa kuwa katika EAC, itachagiza ukuzaji wa fursa za kiuchumi kwa taifa hilo lakini pia kurahisisha uingizaji bidhaa na huduma kutoka nchi nyingine zilizo kwenye jumuiya hiyo na ambazo pia ni majirani zake wa karibu.

### FURSA ZA KIUCHUMI

James anasema DRC itakapoingia kwenye EAC itakuwa imetanua wigo wa soko kwa bidhaa zake hasa zinazotokana na madini na vito, ili kuwafikia watu wa ukanda huo.

Pia DRC ina sehemu kubwa ya ardhi yenye rutuba hasa katika ukanda wa Mto Congo na hivyo kuwa sehemu inayofaa kwa uzalishaji wa chakula na viungo vinavyoweza kupata soko kubwa na la karibu katika ukanda wa EAC.

Hatua ya DRC kuingia EAC italiwezesha taifa hilo kujiunga katika miradi ya pamoja kama ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, hivyo kuifanya sehemu yake kufikika kwa urahisi zaidi.

Mchambuzi wa masuala ya siasa aliyepo Nairobi nchini Kenya, Jeremiah Owiti, aliliambia gazeti moja hivi karibuni kuwa hatua ya DRC kujiunga EAC, kutatanua wigo wa biashara na mawasiliano kutoka ukanda wa Afrika ya Kati.

Tangu alipoapishwa Januari mwaka huu kuchukua nafasi iliyokuwa ikishikiliwa na Rais (mstaafu) Joseph Kabila, Rais Tshisekedi amekuwa akionyesha dhamira ya wazi kutaka DRC ijiunge EAC.

EAC ina masharti kadhaa kwa mwanachama mpya kujiunga, miongoni mwa hayo ni kuheshimu misingi ya demokrasia, utawala wa sheria, uwajibikaji, uwazi na haki za binadamu.

Mkataba ulioanzisha jumuiya hiyo unaelezea pia kuwa, mbali na sababu za kijiografia, usawa katika fursa, usawa wa kijinsia na kutambua, kuendeleza na kulinda haki sawa kwa mujibu wa tamko la Umoja wa Afrika (AU) kuhusu haki za binadamu, ni miongoni mwa vigezo vya kuwa mwanachama wa EAC.

Mkurugenzi wa kampuni ya TradeMark East Africa nchini Rwanda, Patience Mutesi, alikaririwa na gazeti moja akisema ukubwa wa kijiografia na idadi ya watu katika ukanda wa EAC kunatoa fursa pana za biashara na wateja.

### BIASHARA

Katika kipindi cha mwaka jana, takwimu zinaonyesha kuwa Uganda inauza bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 398 kwenda DRC huku ikipanga kukuza biashara hiyo kufikia dola bilioni 2 ifikapo 2020.

Wakati huo huo, Uganda iliingiza bidhaa za DRC zinazokadiriwa kuwa na thamani ya dola milioni 2.5.

Kwa upande wa Rwanda, takwimu zinaonyesha kuwa nchi hiyo iliuza bidhaa zenye thamani ya dola milioni 456 wakati ikinunua bidhaa zenye thamani ya dola milioni 11.2 kutoka DRC.

Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya dola milioni 153 kwa mwaka 2017 na kuingiza zenye thamani ya dola milioni 1, kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kwa simu namba 0754691540 ama barua***

# Rwanda, Uganda zinavyotishia amani, utengamano wa EAC

**Na Mashaka Mgeta**



Rais Yoweri Museveni wa Uganda (kushoto) akiwa na Rais Paul Kagame wa Rwanda. **PICHA: MTANDAO**

VITA ya maneno inazidi kuongezeka kati ya mataifa mawili yaliyo wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Rwanda na Uganda kiasi cha kutishia amani na usalama katika ukanda huo wenye nchi sita zilizo wanachama wa jumuiya hiyo.

Mbali na Rwanda na Uganda, wanachama wengine wa EAC ni Tanzania, Kenya, Burundi na Sudan Kusini.

Rwanda na Uganda zimekuwa na mgogoro wa kidiplomasia kwa nyakati tofauti, lakini zaidi baada ya kuibuliwa madai kwamba Uganda ilikuwa inawakamata na kuwaweka ndani Wanyarwanda waliokuwa wanaingia nchini humo.

Hali hiyo ilikuwa ni sehemu ya historia ya migogoro ya mara kwa mara kwa nchi hizo, kama ilivyowahi kutokea katika miaka ya 1990 ziliponusurika kuingia kwenye vita kutokana na mapigano ya majeshi yao huko DRC.

Majeshi hayo yalikuwa yanashiriki katika mapigano ya kumuondoa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, wakati huo ikijulikana kama Zaire, Mobutu Sese Seko.

Mgogoro mwingine ni wa hivi karibuni na unaoendelea 'kutokota' ambapo Uganda iliishutumu Serikali ya Rais Kagame kwa kuzuia malori ya mizigo na magari mengine kutoka nchini humo kuingia Rwanda.

Utawala wa Rwanda uliyazuia maroli na magari mengine kutoka Uganda kuingia nchini humo, Msemaji wa Serikali ya Rais Museveni, Ofwono Opondo, aliwaambia waandishi wa habari.

Kwa mujibu wa Opondo, maroli ya mizigo yanayofikia 129 kutoka Uganda yalikuwa 'yamekwama' kwenye mpaka wa Gatuna kwa wakati huo.

Hata hivyo, Serikali ya Rais Kagame kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Richard Sezibera, ilikanusha shutuma hizo na kufafanua kwamba magari hayo yalielekezwa kupitia mpaka wa Kagitumba ulioko Kaskazini mwa nchi hiyo ili kupisha ujenzi wa barabara yenye shughuli nyingi katika mpaka wa Gatuna.

"Walioitikia wito wa kupitia mpaka wa Kagitumba wameingia Rwanda na kuendelea na shughuli zao," akasema Sezibera.

Kwa upande mwingine, Mamlaka ya Mapato Rwanda (RRA) ilisema hatua hiyo iliyofikiwa kwenye mpaka wa Gatuna unaojulikana pia kama Katuna, ilikusudia kupisha ujenzi wa jengo la kituo kimoja cha mpakani.

Inaelezwa kuwa barua iliyoandikwa na RRA kwenda kwa Kamishna wa Forodha wa Mamlaka ya Mapato Uganda (URA), ilifafanua kuhusu hatua ya kuyahamishia magari hayo kupita kwenye mpaka mwingine.

Pia Sezibera amesema zuio la raia wa Rwanda kuingia Uganda lilitokana na kukamatwa kwao kwa kuhisiwa kuwa ni mashushushu wanaokwenda kufanya shughuli za upelelezi na pia hawapatiwi huduma muhimu wanapokamatwa.

> Watu wanaingia na kutoka isipokuwa kwa raia wa Rwanda ambao wamesisitizwa wasisafiri kwenda Uganda kutokana na changamoto za kiusalama wanazokutana nazo huko.

"Watu wanaingia na kutoka isipokuwa kwa raia wa Rwanda ambao wamesisitizwa wasisafiri kwenda Uganda kutokana na changamoto za kiusalama wanazokutana nazo huko," akasema.

Sezibera akaongeza, "sio juu yetu (Rwanda) kulitatua hilo, bali lipo kwa upande wa Uganda. Kwa maana Waganda wanakaribishwa kwetu (Rwanda) na hatuna matatizo kwenye upande wa mpaka wetu."

Lakini Msemaji wa Serikali ya Uganda, Opondo akasema magari ya kutoka nchini humo yaliyopitia mpaka wa Kagitumba nayo yalizuiwa kuingia Rwanda.

Pia Opondo alikanusha madai ya kushikiliwa kwa raia wa Rwanda kwa tuhuma za kuwa mashushushu, badala yake akasema kama wapo Wanyarwanda kwenye magereza ya nchi hiyo watakuwa wanatokana na makosa yaliyoshughulikiwa kupitia polisi na mfumo wa mahakama nchini Uganda.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa kwa takribani muongo mmoja tangu vikosi vya majeshi kupigana hadi kumwaga damu kwenye jiji la Kisangani, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Uganda na Rwanda wamekuwa katika mgogoro wa kidiplomasia.

Hata hivyo, mzozo huo ulichukua sura tofauti Julai 2011 pale Rais Museveni alipofanya ziara iliyowashangaza wengi kwenda Rwanda na kutumia siku kadhaa, akiwa na timu ya wataalamu wake walioingia mikataba kadhaa ya ushirikiano kati ya nchi mbili hizo.

Kwa kiasi kikubwa, wachambuzi wa masuala ya ushirikiano wa kidiplomasia wanaielezea hali iliyopo sasa kwamba ni 'matunda' ya uhusiano uliokuwapo zamani na 'kutibuka' kwake.

Ukanda wa Afrika Mashariki unakabiliwa na changamoto nyingi katika kufikia ustawi endelevu na maisha bora kwa wananchi wao, hivyo kuwapo haja ya kuepuka migogoro miongoni mwa nchi wanachama na majirani.

Hivi karibuni, taarifa zilisambaa zikielezea hatari ya kuibuka vita kati ya Uganda na Rwanda.

Lakini akiwa nchini Ubelgiji, Rais Kagame akaliambia gazeti la Taz la Ujerumani kwamba ipo haja ya kuepuka vita kati ya Rwanda na Uganda, kwa vile kila nchi lazima 'itapoteza kitu' ikiwa vita hiyo itapiganwa.

Wakati akielezea hivyo, Rais Kagame akasisitiza kwamba Uganda inashiriki katika mpango wa kusaidia vikundi vya wana mgambo kwenye maeneo ya karibu na mpaka wa nchi hizo, ili kuihujumu Rwanda.

"Watu wanahofia kuwapo vita kati yetu (Rwanda na Uganda), sioni kama hili litatokea kwa sababu ninadhani Uganda inajua madhara yatakayotokea ikiwa tutaingia kwenye vita, hatutaki kwenda njia hiyo kwa maana kila nchi itapoteza kitu," akasema Rais Kagame.

Akifafanua kuhusu tishio lake la kuibuka vita kati ya nchi hizo, Rais Kagame akasema, "ndio (itatokea), kama unavuka mpaka unaweza kutumia chochote kinachowezekana ndani ya himaya yako, kama kukamata watu.

Lakini kama wanavuka mpaka na kuingia nchini kwetu na kutaka kufanya jambo lolote kwenye himaya yetu, hilo ndilo nililokusudia."

Rais Kagame akasema Uganda bado inaendelea kuwakamata Wanyarwanda kwa tuhuma za ujasusi, kuwashikilia kwa muda mrefu na kisha kuwaachia, jambo analosema si zuri.

Mbali na mgogoro huo na ule unaoikabili Rwanda na Burundi, kumeibuka pia kauli zenye utata kutoka kwa wabunge wawili wa Kenya na Tanzania, zikitafsiriwa kuwa na nia ya kufifisha uhusiano kati ya nchi hizo.

Kauli ya kwanza kutolewa na Mbunge wa Jimbo la Starehe, Charles Njagua maarufu kama Jaguar alikisema hataki kuwaona wafanyabiashara kutoka China, Tanzania na Uganda kwenye jimbo lake.

Akadai kuwa wamekuwa kikwazo kwa wafanyabiashara wazawa wa nchi hiyo kukuza biashara zao kutokana na mashindano ya kibiashara baina yao.

Katika kipande cha video kilichosambaa mitandaoni, Jaguar ambaye pia ni mwanamuziki, akasema saa 24 wafanyabiashara hao ambao ni raia wa nje kuondoka nchini humo la sivyo watawapiga mawe na kwamba hawaogopi mtu wala kitu chochote.

Kauli hiyo ikafuatiwa na ile wa Mbunge wa Mtera (CCM), Livingstone Lusinde maarufu kama Kibajaji, akitaka hali kama hiyo iwakute Wakenya waliopo nchini.

# Mkutano wa amani Bahrain, Kushner kafaulu au kawama?




Baadhi ya waandamanaji waliokuwa wakipinga mkutano wa kiuchumi kuhusu Palestina ulioratibiwa na Mshauri wa Rais Donald Trump aliye pia ni mkwewe ambao ulifanyika Bahrain. **PICHA: MTANDAO**

**Na Anil Kija**

VYOMBO vya habari eneo la Mashariki ya Kati, Marekani na kwingineko duniani vimeingia katika mjadala mpana kuhusu kufaulu au kukwama kwa mkutano wa kimataifa kuhusu Mashariki ya Kati uliofanyika Bahrain, moja ya falme za Kiarabu eneo la Ghuba ya Uajemi.

Mtoa mada na mhusika mkuu wa mkutano huo alikuwa Jared Kushner, mkwe na mshauri maalum wa Rais Donald Trump wa Marekani, ambaye kwa matamshi yake aliwaghadhibisha mamilioni ya wasomi na wananchi wa kawaida wa Palestina, ila ilibidi wamsikilize.

Alisema kwa mfano kuwa 'Rais (Donald) Trump hajakata tamaa kuhusu Palestina,' na kuwa Wapalestina 'hawana sababu ya kutokumuamini Trump,' wakati kila hatua aliyochukua hadi sasa inaelekea kwingine.

Akizungumzia madai ya msingi ya kambi ya Wapalestina ambao pia walikataa kuhudhuria mkutano huo, uliohudhuriwa na nchi tano za Kiarabu, Israel, Marekani na washirika wao Ulaya na mashirika kadhaa ya kimataifa, Kushner alisema Wapalestina 'hawana rekodi nzuri ya kufikia makubaliano yanayoeleweka,' akisisitiza kuwa mwelekeo wa sera za Marekani kwa suala hilo utaendelea kusimamia njia ambayo utawala wa Trump unataka ifuatwe.

Kati ya washirika wa Marekani katika mkutano huo, mkuu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kulikuwa na aina ya ukosoaji, mkurugenzi mtendaji Christine Lagarde akisema Israel lazima iondoe vizuizi vya usafiri.

> Balozi wa Marekani nchini Israel, David Friedman, alizusha zogo mwezi uliopita aliposema ni sahihi kwa baadhi ya maeneo yanayokaliwa ukingo wa Magharibi kumegwa, lakini si eneo lote.

Ukosoaji huo ni kielelezo cha kutokuaminiwa kwa mpango huo kwani eneo la Palestina ni vipande vipande tu vyenye utii kwa kundi la Hamas upande wa Gaza Magharibi ya Israel (au Kaskazini Mashariki ya Misri) na utii kwa chama cha ukombozi wa Palestina Al Fatah kwa upande wa ukingo wa Magharibi wa mto Jordan.

Ni eneo ambako wahamiaji wa Israel wanaendelea kujenga makazi na pale ambako imekuwa kama miji, hatua zinaendelea kuweka maeneo hayo chini ya sheria ya Israel, yaani kuondoa dhana kuwa yanakaliwa kijeshi na Israel.

Balozi wa Marekani nchini Israel, David Friedman, alizusha zogo mwezi uliopita aliposema ni sahihi kwa baadhi ya maeneo yanayokaliwa ukingo wa Magharibi kumegwa, lakini si eneo lote.

Baadhi ya walioshiriki katika mkutano huo walisema katika mahojiano ya hapa na pale kuwa kilichojadiliwa Bahrain siyo mpango halisi iwe ni wa amani au wa maendeleo ya Palestina na nchi zinazozunguka Palestina ila ni taswira tu ya kile kinachotakiwa kufanyika.

Suala ambalo wajumbe walikwepa kulijadili na waandamanaji wa Palestina kote Mashariki ya Kati na kwingineko duniani wakilipigia kelele kuwa inatakiwa kwanza suluhisho la kisiasa, ndipo mpangilio wa kukuza uchumi ufuate.

Wanasema mpango wa Kushner ni kinyume cha uelekeo halisi unaotakiwa, suala ambalo wataalamu wengine wanapuuzia, wakisema msingi wa kila kilichojadiliwa hapo ni kukwama kwa utafutaji wa suluhisho la kisiasa, lile la nchi mbili huru.

Kwa maana hiyo mkutano wa Bahrain unaanzia pale Wapalestina wanapomalizia, kuwa nje ya kuwapo taifa huru la Palestina hawaoni cha kujadili.

Kushner anachosema ni kuwa ili kuwe na mjadala wowote inabidi kuachana kwanza na suala la kuunda nchi mbili huru, kwani halitatuliki, na badala yake kutafuta njia za kupunguza matatizo yanayowakabili Wapalestina katika maisha ya kila siku.

Wazungumzaji wa Kipalestina walitaja matatizo ya serikali ya Palestina, si biashara.

Hata hivyo uwepo wa Israel katika mkutano huo haikuwa ni jambo rasmi, na zaidi walikuwa ni wafanyabiashara, kwani haikutakiwa ionekane kana kwamba utawala wa Trump unahusisha Israel na nchi za Kiarabu kwa pupa.

Mkutano wenyewe hasa ulikuwa ni kati ya Marekani na marafiki (washirika) wake katika eneo hilo, kuweka mikakati ya kiuchumi ambayo inalenga kuvunja nguvu na ushawishi wa Iran katika eneo hilo, hasa kwa vile msingi wa ushawishi huo ni upinzani kwa Marekani kuhusu suala la Palestina.

Ni nyenzo inayotumiwa na Iran kufikia malengo yake, ambayo hayaanzii katika suala hilo ila matazamio kisiasa na kidhehebu ya kihistoria nchini Iran.

Ni matazamio hayo ambayo yanatofautiana sana na yale ya nchi za dhehebu la Sunni ambazo hasa ni jumuiya yote ya nchi za Kiarabu, na kutokana na hali halisi zimetupilia mbali mwekeleo wa kivita - kwani nchi mbili hazitafikiwa huku Wapalestina wanadai 'haki ya kurudi' kule baba zao walipokimbia nchini Israel miaka ya 1940-1950.

Utawala wa Iran ni tofauti kwani uliundwa kwa kuondoa utawala wa Mfalme wa Iran Reza Pahlavi aliyekuwa mshirika wa Marekani, na tangu 1979 kuna uadui wa kukata na shoka na Marekani.

Hivi sasa utawala wa Marekani uko mbioni kukamua pumzi ya uhai kiuchumi nchini Iran, wananchi waondoe utawala wa siasa kali.

Matazamio hayo ndiyo 'roho' ya mkutano wa Bahrain, kuwa makundi ya kijihadi ya Gaza na wakosoaji wakubwa wa Marekani upande wa utawala wa PLO-Al Fatah yanaanza kutengwa na nchi za Kiarabu ambazo zina amani na maendeleo ya kutosha, hasa eneo la Ghuba.

Kutengwa kwa makundi hayo ni kuachana na mijadala ya kutambuliwa kwa Yerusalemu kama mji mkuu wa Israel, kuchukuliwa rasmi kwa eneo la mlima Golan ambalo kwa jadi ni la Syria kuwa sehemu rasmi ya Israel, kuwa kamwe halitarudishwa Syria, hatua ambayo imebarikiwa na utawala wa Trump.

Kuchukuliwa kwa maeneo kadhaa ukingo wa Magharibi kutafuata punde.

Licha ya kuwa baadhi wanaona kana kwamba mkutano huo ulikuwa jambo rahisi kwa sababu nchi hizo ni washirika wa Marekani, ukiangalia kwa karibu unakuta kuwa ni hatua kubwa iliyofikiwa kufanya nchi za Kiarabu zianze kuachana na suala la kuundwa kwa nchi mbili, kuwa ni kuendeleza mifarakano na mkwamo wa maendeleo milele.

Kwa mfano gazeti la Haaretz nchini Israel lilisema kuwa waandishi sita wa habari wa Israel waliruhusiwa kuhudhuria ili kuandika habari kuhusu mkutano huo, 'licha ya kuwa hakuna mahusiano ya kidiplomasia kati ya Israel na Bahrain,' yaani kimsingi ni maadui. Ilikuwa pia jambo adimu kwa wachunguzi kuona wafanyabiashara wa nchi za Kiarabu na wenzao wa Israel wakijadili masuala ana kwa ana si kificho.

Wazungumzaji wa Kipalestina, katika mazingira ambayo kimsingi yalionekana kana kwamba ni tahadhari ya kidiplomasia au kitaaluma kuwa hakuna uwezekano wa kutatua masuala ya uchumi ya Palestina bila kutatua suala la mustakabali wake kisiasa, ni kama walikuwa wanaaga.

Ni hali ya mabadiliko kutoka jukwaa la kisiasa kuhusu kuwepo kwa nchi mbili kwenda katika jukwaa la kiuchumi ambako kuanzia sasa nchi za Ghuba zitakuwa zinajadili na Mamlaka ya Palestina na ile ya Hamas eneo la Gaza kuhusu masuala ya kiuchumi.

Licha ya kuwa vipo vizuizi vingi vya kuingia ukingo wa Magharibi kutoka Gaza kwa mfano, kwani usalama wa Ukingo wa Magharibi upo chini ya polisi wa Israel, yapo maeneo ya uwasilianaji na hata uwekezaji yanayowezekana.

Gaza ina uhusiano mzuri na Qatar inayowekewa vikwazo na Saudia kuhusu Iran; haijafaulu kuleta ari mpya eneo la Gaza kuhangaikia uchumi na si jihadi ya kurudi Israel, lakini mabadiliko yanakuja.



# Ng'ombe 10 wadaiwa kufa kila siku kwa kunywa kemikali

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

ZAIDI ya ng'ombe 10 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wanadaiwa kufa kila siku kwa sababu ya kunywa maji yanayodaiwa kuwa na kemikali aina ya Cynide inayotumika kusafisha madini aina ya dhahabu.

Hayo yalibainishwa jana na wafugaji wa Wilaya ya Chunya, walipokuwa wakizungumza na Nipashe namna wanavyoweza kuchunga mifugo yao isipate athari kwenye machimbo ya dhahabu.

Walisema kemikali aina ya Cyanide inayotumika kusafisha dhahabu kwenye planti nyingi za madini hazina mifumo imara ya kudhibiti maji machafu na kusababisha mifugo yao kunywa maji hayo yenye sumu.

Miongoni mwa wafugaji hao, Mashaka Kibuda, alisema maji hayo yenye sumu yanasababisha kifo cha ng'ombe ndani ya muda mfupi na kuiomba serikali kusimamia vyema udhibiti wa maji hayo kwenye planti za madini.

Alisema wafugaji wengi wamepata hasara kutokana na mifugo yao kufa na kwamba hali hiyo inatishia usalama wa mifugo kwa kuwa wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya maji.

Mwenyekiti wa wafugaji katika wilaya hiyo, Shang'ai Ole Rapoyi, alisema wafugaji wanaochunga mifugo yao karibu na planti wako katika hatari ya kupata magonjwa ikiwamo kansa kutokana na kuwapo kwa kemikali hatari ya Cyanide.

"Kemikali inayopatikana kwenye maji ya dhahabu ina madhara makubwa kiafya kwa binadamu kwa mwanamume anaweza kupoteza nguvu za kiume, lakini pia kupata magonjwa ya kansa," alisema Ole Rapoyi.

Pia alishauri namna ya kuepuka kadhia hiyo ni kutenga maeneo ya malisho na majosho na kuzuia ujenzi wa planti kwenye makazi ya watu ama maeneo hatarishi.

Daktari wa mifugo wilayani Chunya, Dk. Benedict Namatogo alithibitisha kupokea taarifa za mifugo kufa kwa sababu ng'ombe kunywa maji yenye kemikali ya Cyanide.

Naye Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Chunya, Julius Ngwita, alisema serikali imebaini changamoto hiyo na kuchukua hatua kali ikiwamo kuwafungia huduma baadhi ya wamiliki wa planti walioshindwa kudhibiti maji yaliyoathiriwa na kemikali.

**Alisema wafugaji wengi wamepata hasara kutokana na mifugo yao kufa na kwamba hali hiyo inatishia usalama wa mifugo kwa kuwa wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya maji.**

# Mbeya yahitaji uniti 8,000 za damu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ZAIDI ya uniti za damu 8,000 zinahitajika kwa mwaka katika Mkoa wa Mbeya ili kukidhi mahitaji ya kila mgonjwa mwenye uhitaji hususani wajawazito, watoto na watu ambao wanapata ajali

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Charton Meena, alisema jana wakati wa kuchangia damu na kuwahusisha wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji Teku kwenye Hospitali ya Uwata, jijini Mbeya.

Alisema Mkoa wa Mbeya unaongoza kwa kuwa na uhitaji mkubwa wa damu hali inayosababisha wagonjwa wengi kushindwa kupatiwa kwa wakati licha ya kuwapo kwa jitihada mbalimbali za kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchangia.

Meena alisema uhaba mkubwa wa damu katika Mkoa wa Mbeya unasababishwa na mwitiko mdogo wa wananchi kuchangia na kwamba changamoto hiyo inasababisha kuhatarisha uhai wa mgonjwa.

"Mkoa wa Mbeya ni kituo cha ukusanyaji damu Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, lakini unakabiliwa na changamoto ya uhaba wa damu na mkoa pekee unahitaji uniti 8,000 ili kuwahudumia wagonjwa, lakini hali halisi hata uniti hizo hazifiki. Tunaomba wananchi kujitolea kwa hiari kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wenzetu," alisema Meena.

Vilevile, alisema zaidi ya uniti 48,990 za damu zinahitajika katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ili kukidhi mahitaji na kwa wastani kwa mwezi zaidi ya uniti 4,082 zinahitajika.

Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, UVCCM, Mbeya Mjini, Shija Steven, alisema chama kupitia idara ya vijana kitaanza utaratibu wa kuandaa mikutano yenye lengo la kuhamasisha wananchi kuchangia damu.

Alisema ili kuokoa maisha ya wenzao utaratibu huo utasaidia kukabiliana na changamoto ya uhaba wa damu kwa wagonjwa.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (kushoto), akimkabidhi cheti Mratibu wa Safari ya Utalii wa Ndani, Dayna Saimoni, ikiwa ni ishara ya shukrani kwa kuunga mkono jitihada za Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuchochea na kuinua idadi ya watalii wa ndani katika msitu asilia wa Magoroto katika Wilaya ya Handeni mkoani Tanga juzi. **PICHA: LUSUNGU HELELA**

# MV Songoro kuokoa mikoa Nyanda za Juu Kusini

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

MELI ya abiria yenye uwezo wa kubeba watu 200 na tani 200 za mizigo inayojengwa kwenye Bandari ya Itungi, Ziwa Nyasa, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya inatarajiwa kukamilika hivi karibuni ili kuondoa changamoto ya usafiri wa majini katika ukanda wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mhandisi wa Kampuni ya Ujenzi wa Meli ya Songoro Marine, Salehe Songoro, alisema hayo mbele ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa meli katika Bandari ya Itungi, wilayani Kyela.

Songoro alisema meli hiyo ni miongoni mwa zile tatu ambazo zilijengwa kwa lengo la kurahisisha shughuli za usafiri ndani ya Ziwa Nyasa kwa wananchi wa mikoa ya Mbeya, Njombe, Ruvuma na nchi jirani ya Malawi ambao wanaishi kando mwa Ziwa Nyasa.

"Mpaka sasa meli mbili zinafanya kazi, moja ikitumika kusafirisha abiria na nyingine kwa ajili ya kubeba mizigo, usafiri huu umekuwa mkombozi wa wananchi kwa sababu ya gharama nafuu na kufika maeneo yalikuwa hayafikiki," alisema Mhandisi Songoro.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema kutokana na uhitaji mkubwa wa meli katika Ziwa Nyasa, serikali inafikiria kuanza ujenzi wa meli kubwa zaidi ya mizigo ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema meli hiyo itakapokamilika itatoa huduma kwenye bandari 15 za mikoa ya Mbeya, Njombe, Ruvuma na kwa sasa hutegemea usafiri wa mitumbwi ambao sio salama kwa kuwa baadhi ya wananchi hupoteza maisha.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Issah Solomon, alisema kukamilika kwa meli hiyo na ujenzi wa barabara kuelekea Bandari ya Itungi kutaongeza fursa mbalimbali za kiuchumi.





# Askofu atoa somo kwa vijana

**Na Peter Mkwavila, KONDOA**

VIJANA wametakiwa kuibua miradi itakayowawezesha kujiajiri wenyewe badala ya kukaa vijiweni na kuinyooshea serikali kidole kutokana na kukosa kazi ya kuajiriwa.

Wito huo ulitolewa na Askofu wa Kanda ya Kati Kanisa la EAGT, Dk. Livingstone Denis, alipokuwa akizungumza na waumini wa madhehebu mbalimbali ya dini kwenye ufunguzi wa kanisa hilo wilayani Kondoa.

Alisema vijana wana uwezo mpana wa uelewa wa kuibua miradi mbalimbali ambayo inayoweza kuwafanikisha kujiajiri badala ya kusubiri serikali kuwaajiri.

Alisema kuwa tatizo lililopo vijana wengi wamekuwa na mtizamo ambao wanashindwa kujiongeza wenyewe badala yake wanasubiri kuwekezwa na serikali suala ambalo hivi sasa limepitwa na wakati kutokana na uwapo wa fursa nyingi zilizopo.

"Taifa letu limejaa vijana ambao hawafanyi kazi kutokana na kukaa vijiweni na kupotoshana na kuilaumu serikali huku wenyewe hawana kazi ya kufanya hata ile ya kujiajiri wenyewe kupitia fursa mbalimbali zilizopo kwa hivi sasa hapa nchini," alisema.

Kadhalika, aliwataka Watanzania kuendelea kuwaombea viongozi waliopewa dhamana kwa ajili ya taifa ili waweze kuifanya kazi yao kwa bidii.

"Pia tuombee uchaguzi wa serikali za mitaa ili viongozi watakaochaguliwa wasiwe wapinzani wa shughuli za kimaendeleo ambazo Rais amekuwa akizifanya kwa ajili ya Watanzania bila kujali vyama vya siasa, dini, rangi au kabila," alisema.

Mchungaji kiongozi wa kanisa hilo wilayani Kondoa, Eliya Chiloleti, alisema kuwa kutokana na juhudi za kuiunga mkono serikali katika jitihada zake za kimaendeleo wameweza kujenga kanisa hilo kwa gharama za Sh. milioni 73.

Alisema kuwa fedha hizo zilitokana na waumini wenyewe kwa kufanya kazi kwa bidii kama serikali inavyoagiza.

# Kiwango cha mwanamke kuzaa sasa chapungua

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema ongezeko la watoto wanaoandikishwa shule linatokana na mpango wa elimu bure na si kwamba watoto wengi wanazaliwa nchini kwa kuwa kiwango cha mwanamke kuzaa kimepungua kutoka watoto saba hadi watano.

Ummy alitoa kauli hiyo jana katika hafla ya kutiliana saini kati ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Ditopile na wanafunzi wa kike waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano mkoani Dodoma ambao amejitolea kusomesha watoto hao 100 na kuwagharamia michango yote.

Akizungumza katika hafla hiyo, Ummy alisema takribani watoto 500,000 walikuwa wanabaki nyumbani baada ya wazazi wao kushindwa kuwahudumia, lakini kutokana na mpango huo umeongeza wanafunzi kwa zaidi ya asilimia 40.

"Sasa ongezeko hili mtu anaweza kusema kwa sababu watoto wengi wanazaliwa, hapana takwimu zetu zinaonyesha kiwango cha mwanamke mmoja kujifungua kinazidi kupungua kutoka watoto saba hadi watano, kwa hiyo watoto wanazidi kupungua," alisema.

Alisema serikali imeendelea kuwekeza kwenye elimu kwa kuwa ni moja ya uwekezaji muhimu.

"Takwimu zinaonyesha zipo sababu kubwa za kuwafadhili watoto wa kike, kwa mfano mwaka 2017 watoto hao ambao wamemaliza kidato cha nne ni 1,025,700 wakati wa kiume ni 965,305, sasa wangapi wanaoenda A-level kati ya wanafunzi 100, wanaoenda kidato cha tano na sita, 51 ni wasichana," alisema.

Hata hivyo, alisema takwimu zinaonyesha wasichana 51 si wote wanaokwenda kidato cha tano kutokana na kushindwa kuendelea na elimu.

"Wasichana ambao tulikuwa nao zaidi ya milioni moja wanaokwenda kidato cha tano ni 66,252 na wavulana wanaoenda ni 91,198, tunakuta wasichana ni 42 kati ya 100, huku wavulana ni 58 kati ya 100," alisema.

Kufuatia hali hiyo, alihimiza kuwapo na msukumo wa elimu kwa watoto wa kike na kwamba ufadhili uliofanyika utasaidia kujiepusha na mimba za utotoni, hivi sasa mabinti 27 kati ya 100 wanapata mimba hizo.

Vile vile, alisema vifo vya wajawazito, utapiamlo kwa watoto, chanjo, matumizi ya vyandarua, upelekaji watoto kliniki unatokana na kiwango cha elimu cha mama.

Awali, Mbunge Ditopile alisema hatua hiyo ametimiza ahadi yake aliyoiweka ya kusomesha watoto wa kike waliofaulu kuingia kidato cha tano katika shule za serikali na tayari ameshatoa Sh. milioni 20 kwa ajili ya kusomesha watoto 100.

"Rais wetu John Magufuli wakati anaingia madarakani aliahidi na ametekeleza kusomesha watoto bure kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha nne, mimi kwa nafasi yangu nikajiuliza nifanye nini ili kumuunga mkono Rais wangu nikasema nisomeshe watoto hawa ili nami iwe ni mchango wangu kwa wana Dodoma na taifa kwa ujumla, hivyo utekelezaji wa Ilani anaoufanya Rais wetu ndio umenisukuma kufanya hivi.

"Kuna watu wanajiuliza kwanini watoto wa kike, mara nyingi wamekuwa wakisahaulika, tukitoa misaada kwa vijana wa bodaboda unakuta ni watoto wa kiume tupu, tukisaidia michezo unakuta vijana wa kiume, hata kwenye halmashauri zikitoka nafasi za kuhusisha vikundi vya kijamii unakuta kundi lina vijana wa kiume tupu hapa kama viongozi inabidi tuliangalie hili na tubadilike," alisema Ditopile.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (kushoto), akizungumza na wajumbe wa Tume ya Utumishi ya Polisi, Uhamiaji na Magereza wakati wa kikao cha kujadili utendaji wa vyombo vilivyopo chini ya wizara, kilichofanyika jijini Dodoma jana. Wa pili kushoto ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu. **PICHA: WMN**

# Takukuru Dodoma yaokoa mamilioni

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Dodoma imeokoa Sh. milioni 67.5 katika mradi wa maji wa kijiji cha Kelema Kuu Wilaya ya Chemba baada ya kubaini thamani ya fedha iliyotumika kutoendana na kazi halisi.

Mradi huo ulikuwa na thamani ya Sh. milioni 222.9 uliokuwa chini ya kampuni ya Juin Limited na ulipaswa kukamilika tangu mwaka 2015.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Takukuru mkoani humo, Sosthenes Kibwengu, alisema uchunguzi wao ulibaini thamani ya fedha haikupatikana na uwepo wa malipo zaidi ya kazi halisi zilizofanywa, huku mradi ukishindwa kutoa maji.

Alisema baada ya kubaini hilo, m kandarasi wa mradi huo ulio chini ya Juin Company Limited ameridhia kurekebisha upungufu uliobainika na tayari ameanza kazi ya kubadili mabomba na kuweka yanayostahili ikiwamo kurejesha malipo yaliyolipwa ya ziada wakati alikuwa hastahili.

"Tunatarajia kuanzia sasa wananchi watapata huduma ya maji, kwa sababu mkandarasi tayari ameanza kazi ya kurekebisha upungufu," alisema Kibwengu.

Aliwatoa hofu wakazi wa eneo hilo kuhusiana na mradi huo kwa kuwa mkandarasi tayari ameanza kazi ya kurekebisha upungufu.

Katika hatua nyingine, alisema taasisi hiyo inamshikilia Mkurugenzi wa Global Space East Afrika Limited, aliyepewa kazi ya ujenzi ya kituo cha afya cha Mima kilichopo wilayani Mpwapwa jijini Dodoma, baada ya kubaini kampuni hiyo imelipwa isivyo halali kiasi cha Sh. milioni 86.4 kwa kazi ambazo hazikufanyika katika mradi huo.

Aidha, alisema katika robo ya mwaka ambayo wamebainisha Takukuru Mkoa wa Dodoma imefuatilia na kukagua miradi 34 yenye thamani ya Sh. bilioni 32.5 sawa na asilimia 95.4 ya matumizi ya fedha za miradi ilionekana kufanyika vizuri na thamani ya fedha kupatikana.

Pia alisema wamebaini viashiria vya jinai katika miradi minne, wameanzisha uchunguzi kuhusu uhalali wa malipo ya jumla ya Sh. bilioni 1.4 yaliyofanyika katika miradi hiyo ya miundombinu, afya, elimu na kilimo.



# Wadau wataka kanuni kudhibiti udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WADAU wa kusimamia masuala ya udhalilishaji katika wilaya tatu za Unguja, wamekiomba Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), kuhakikisha kanuni ndogo zitakazoanzishwa kwa pamoja zinatekelezwa ili zilete matunda katika kuondoa udhalilishaji.

Waliyasema hayo jana katika ukumbi wa Malaria, Mwanakwerekwe, wakati wakijadili kanuni hizo za kamati za shehia juu ya mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Kanuni hizo zinazotarajiwa kuanzishwa na chama hicho, zitasaidia kupunguza au kutokomeza udhalilishaji nchini.

Wadau hao walisema kabla ya kupitishwa kwa kanuni hizo, ni vyema kukaa pamoja na kuangalia kwa makini suala la walimu wa madrasa ambao wamedaiwa kuwa kichocheo kikubwa cha vitendo vya udhalilishaji, hususan kwa watoto wa kiume.

Ofisa Wanawake na Watoto kutoka Wilaya ya Magharibi A, Sabra Mwinjuma, alisema ni vyema Tamwa wakakaa na ofisi ya Mufti Zanzibar ili kuona njia gani zitakazotumika katika kuwatambua walimu wa madrasa katika kutokomeza vitendo hivyo.

Alisema tayari mchakato wa kuwasajili walimu wa madrasa ikiwamo kuwa na vyeti vitakavyowafanya kufundisha katika madrasa ulishaanza, hivyo Tamwa haina budi kushirikiana na ofisi ya Mufti Zanzibar ili kujua mchakato huo umefikia katika hatua gani kabla ya hizo kanuni ndogo kuanza kufanya kazi.

Naye Haji Mohammed kutoka Dawati la Jinsia Tunguu, alisema kanuni hizo pamoja na kuweka masharti maalum kwa walimu wa madrasa, ni vyema kuzingatiwa suala la historia ya mwalimu katika chuo anachosomesha na wakati wa kuhama kwenda sehemu nyingine.

Alisema ni vyema wamiliki wa madrasa hizo kuwatambua walimu wanaohamia katika vyuo vyao kwa kufuatilia chuo alichotoka ili kujua tabia ipi iliyomhamisha katika chuo hicho.

"Wamiliki wa madrasa wasiwapokee walimu kwa kuangalia uzoefu wao ikiwamo wamehifadhi vitabu vyote, wana sauti nzuri ya kusoma Kurani lakini wanapaswa kufuatilia madrasa walizotoka kujua historia zao kwani baadhi ya walimu ni waharibifu wa watoto na mara nyingi wakishaharibu watoto wanahama. Kesi kama hizo nyingi zinaletwa ofisini kwetu," alisema.

Wadau hao pia walisema ni vyema kuthibiti utolewaji wa vibali vya ngoma ambazo nazo ni kichocheo kikubwa cha vitendo vya udhalilishaji kwa watoto hususani katika maeneo ya vijijini.

Mwanasheria kutoka Tamwa, Walid Adam, akiwasilisha kanuni hizo, alisema zimeainisha makosa ya udhalilishaji ikiwamo kubaka, kujaribu kubaka, kutorosha, kulawiti na makosa mengine.

Akizungumzia viashiria vya makosa hayo, alisema ni pamoja na kuwapo kwa kumbi za starehe katika maeneo ya makazi ya watu, mavazi yasiyo na heshima, kupungua kwa maadili ya walimu, michezo ya gemu, kupotea kwa malezi ya pamoja na kuwapo kwa maboma katika mitaa.

Naye Ofisa Mwandamizi kutoka Tamwa, Asha Abdi Makame, alisema kanuni hizo ndogo ndogo zitakapomalizika, zitatumika katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar kwa lengo la kudhibiti matukio ya udhalilishaji na kuhakikisha yanaondoka.



Askofu na Mwanzilishi wa Kanisa la Kingdom Assemblies International, Alfred Juma, akimwekea mikono Askofu Mkuu mpya wa kanisa hilo, Humphrey Juma (aliyepiga magoti) wakati wa ibada ya kuwasimika viongozi wapya iliyofanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Ataka walimu kuwa wabunifu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Shule ya Elimu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (Suza), Mariam Jaffar Ismail, amewataka walimu kuwa wabunifu katika kubuni njia za kuwapa elimu ya 'shule direct' ambayo itaendana na mahitaji ya masomo yao na baada ya kumaliza masomo.

Akifunga mafunzo yaliyoshirikisha walimu 25 wa shule za sekondari Zanzibar kuhusu matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) yaliyofanyika Malindi mjini hapa jana, alisema mafunzo hayo yanatarajia kubadilisha mfumo wa ufundishaji ili kuimarisha matumizi ya Tehama na kuimarisha ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Mariam alisema duniani kote wanatumia mifumo ya sayansi na teknolojia, hivyo ni vyema walimu kuendana na mabadiliko katika kuendana na wakati.

Aidha, alisema wakati umefika kwa walimu kuyafanyia kazi mafunzo hayo ili kukuza uelewa wa wanafunzi katika masomo yao pamoja na kunufaika na fursa za elimu katika nchi mbalimbali.

Sambamba na hayo, aliwataka walimu hao kuimarisha ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ili malengo yao kufikiwa.

Akizungumza kwa niaba ya walimu wenzake, Bimkubwa Ali Ubwa alisema wanashukuru kupatiwa mafunzo hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yamewasaidia katika majukumu yao ya utekelezaji kazi.

Alisema wakiwa walimu, wanaondoka hapo wakiwa na jukumu moja la kueneza elimu hiyo kwa walimu wenzao ili lengo la kupatiwa kwao mafunzo lifikiwe.

# Wataalamu maradhi sugu kutoa huduma Z'bar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea na utaratibu wa kuleta wataalamu wa afya ili kusaidia huduma za matitabu kwa wananchi hususan ya saratani yanayowakabili baadhi ya wananchi.

Waziri wa Afya wa Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, alisema hayo jana alipokuwa akifungua kambi ya matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja.

Alisema serikali itaendelea kuleta wataalamu ili kuwawezesha wananchi kupata huduma za matibabu kwa urahisi.

Huduma hiyo ambayo inatolewa bila malipo, inatarajia kudumu kwa mwezi mmoja kuanzia juzi ili wananchi wapate fursa ya kupima afya zao kama ilivyokusudiwa na serikali.

Alisema kuwapo kwa kambi hiyo kutawawezesha wananchi wasio na uwezo wa kumudu gharama za huduma hiyo kujua matatizo yanayowakabili na kupatiwa matibabu ya haraka kabla ya kusababisha athari kubwa mwilini mwao.

Waziri Hamadi alisema kuwapo kwa mradi wa upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake, kutawawezesha wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuongeza uzoefu wa kutoa huduma kutoka kwa wataalamu wa China ambao ndio wanaongoza huduma hiyo ili kujijengea uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa wa saratani wanaohitaji huduma ya vipimo katika hospitali hiyo.

Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuendekeza mila potofu katika kuamini kuwa maradhi ya saratani yanatibiwa kwa waganga wa kienyeji badala yake watumie fursa hiyo kupatiwa matibabu.

Naye Mkurugenzi wa Mambo ya Nje kutoka Hospitali ya Najing Drum Tower nchini China, Jasmine Qi, aliwataka wanawake kupima afya zao mara kwa mara ili kujua maradhi yanayowakabili na kuwahi matibabu.

Alisema saratani ni ugonjwa ambao unapaswa kuwahi matibabu yake mara moja unapogundulika na ni wajibu wanawake wakisaidi kwa kupima mara kwa mara.

Meneja wa Kitengo cha Maradhi Yasiyoambukiza Zanzibar, Omar Mwalim Omar, alisema kuwapo kwa kambi hiyo kutaisadia serikali kukusanya takwimu za uhakika za wagonjwa wa saratani pamoja na takwimu sahihi juu ya ugonjwa huo.

Alisema kutokana na wananchi wengi kutokuwa na uwezo wa kufanya vipimo na kutomudu gharama za matibabu, kupitia kambi hiyo kutawasaidia kujua matatizo yao bila ya kutumia gharama.

# Waziri aita wenye mawazo mapya utalii

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ametoa nafasi kwa wadau wa utalii nchini kuwa uongozi wa wizara upo tayari kupokea ushauri, mapendekezo pamoja na mawazo mapya yatayosaidia kuchochea na kuinua idadi ya watalii wa ndani.

Kanyasu ametumia nafasi hiyo kwa kuwataka watu binafsi, mashirika pamoja na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wenye nia ya kutaka kuwekeza kwenye sekta ya utalii wasisite ofisi yake ipo wazi kwa mtu yeyote.

"Kwa yeyote atakayetaka kuniona kwa ajili ya kukuza na kuendeleza utalii hasa utalii wa ndani kwangu mimi pamoja waziri milango ipo wazi muda wote," alisisitiza Kanyasu.

Alisema hayo alipokuwa akizungumza na watalii wa ndani wapatao 200 kutoka jijini Dar es Salaam ambao walitembelea katika msitu asilia wa Magoroto katika Wilaya ya Handeni mkoani Tanga kwa ajili ya kutalii ndani ya msitu wenye kila aina ya vivutio vya utalii likiwamo ziwa la kutengenezwa.

Kundi hilo la watalii wa ndani liliratibiwa na Kampuni ya Dalida Tours and Travel Agency kupitia chini ya usimamizi wa mratibu wa safari hiyo, Emma David.

Kanyasu alisema moja ya mkakati wa wizara ni kutaka watalii wa ndani wawe namba moja kwa kutembelea vivutio vya utalii badala ya kutegemea watalii wa kutoka nje kama ilivyo sasa.

Aidha, alisema pia wizara ipo tayari kupokea na kutoa msaada wa hali na mali kwa mtu au kikundi cha watu kitakacholenga kuhamasisha utalii wa ndani.

Aliongeza kuwa idadi ya watalii wa ndani hairidhishi, hivyo kunahitajika mkakati wa pamoja katika kuhamasisha utalii wa ndani kwa Watanzania ili waweze kutembelea vivutio hivyo.

Katika hatua nyingine, Kanyasu alisema kama nchi haiwezi kuifanya sekta ya utalii kama injini ya uchumi endapo wazawa wenyewe wataendelea kuwa nyuma, huku utalii wa ndani ukiwa na mwitikio mdogo.

"Kama taifa na kwa mwananchi mmoja mmoja bado hatujaitendea hali sekta ya utalii ni sekta ambayo haijaguswa hata kidogo ni lazima wananchi wawekeze na wakati huo huo wananchi watembelee vivutio vya utalii," alieleza.

Naye Emma David, mratibu wa kundi hilo la watalii wa ndani alisema wamejipanga kuhamasisha idadi kubwa zaidi ya watalii wa ndani kwa kupitia mitandao ya kijamii ili waweze kutembelea vivutio mbalimbali vilivyopo nchini.

"Sisi tumejipanga kutembelea mikoa yote lengo letu ni kuunga mkono jitihada za wizara katika kuhamasisha utalii wa ndani, alisisitiza Emma.

Aidha, aliishukuru wizara kwa jitihada inazozifanya za kutengeneza mazingira rafiki kwa watu wenye nia ya kutaka kuwekeza kwenye utalii wa ndani.

Naye, Meneja wa Magoroto, Jeremia Mchechu, alisema mwitikio wa watalii kutoka ndani na nje ya nchi umekuwa mkubwa tangu walipoanzisha eneo hilo kama kivutio cha utalii na eneo la ziwa ambalo ni la kutengeneza limekuwa kivutio kikubwa cha utalii.

Alisema watalii wengi wanaofika katika eneo hilo wamekuwa wakipendelea kupanda milima, kupanda baiskeli milimani pamoja na kutembelea vijijini kwa ajili ya kujifunza tamaduni za wakazi wa Tanga.

# Msichana wa kazi matatani tuhuma za kuiba mtoto

**Na Christina Haule, MOROGORO**

JESHI la Polisi mkoani Morogoro, linamshikilia msichana wa kazi kwa tuhuma za kuiba mtoto wa mwaka mmoja wilayani Kilosa, na kupatikana wilayani Nzega mkoani Tabora.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Wilbroad Mutafungwa, tukio la wizi wa mtoto huyo lilitokea Juni 25, mwaka huu majira ya asubuhi katika eneo la Manzese A wilayani Kilosa na juhudi za kipolisi zilifanikisha kupatikana kwa mtoto huyo akiwa wilayani Nzega mkoani Tabora Juni 29, mwaka huu.

Kamanda Mutafungwa alimtaja mfanyakazi huyo kuwa ni Christina Claudi (23), mkazi wa Manzese A ambaye alimdanganya dada na kufanikiwa kumuiba mtoto Thomas Degratius (1).

Akielezea tukio hilo kamanda Mutafungwa alisema, siku ya Juni 25 mfanyakazi huyo alimuaga dada wa mtoto aliyeibwa aliyejulikana kwa jina la Marietta Degratius (16) kuwa anaenda na mtoto bombani kufua huku akiwa na amembeba mgongoni.

Kamanda huyo alisema msichana huyo wa kazi hakurudi hadi taarifa ziliporipotiwa polisi na mama wa mtoto huyo, Flora Thomas (32) na kumpata mtoto huyo mkoani Tabora.

Kamanda Mutafungwa aliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao katika malezi ili kuepusha wizi wa watoto kama ilivyotokea kwa mtoto huyo.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi waliosoma Tosamaganga (TOSA), Danford Mbilinyi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu maandalizi ya kuianzishia shule hiyo miradi endelevu. Kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Stephan Biginagwa na Katibu wa Kamati, Iddy Mwerangi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TADB kuongezea nguvu kiwanda cha kahawa

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imeahidi kukiongezea uwezo Kiwanda cha Tanganyika Instant Coffee (TANICA) kinachochakata kahawa mkoani Kagera kwa lengo la kukuza mnyororo wa thamani wa zao hilo nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ziara yake mkoani humu,

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, amesema ni muhimu kuongeza nguvu kiwanda hiki kwani kuwepo kwake kunatoa fursa kwa soko la uhakika kwa wakulima wa kahawa.

"TADB imedhamiria kukiendeleza kiwanda cha Tanica ili kuchakate kahawa hapa hapa na kuiongezea thamani na kuifanya iwe ni kahawa yenye ushindani katika soko la ndani na nje," alisema Justine.

Alisema kuna kila sababu ya kukiongezea nguvu kiwanda hicho kwani kuchakata kahawa kutachangia kutengeneza ajira, pia kutasaidia kujenga soko la ndani la uhakika la kahawa kwa wakulima na kuchochea uzalishaji na ubora wa kahawa.

"Benki ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 30 katika msimu wa mwaka jana zitumike katika zoezi la ukusanyaji na ununuzi wa kahawa kutoka kwa wakulima mkoani humu. Kwa mafanikio yaliyopatikana katika zao la msimu uliopita, tunataka msimu huu mgao wa kwanza uende Tanica ili kahawa yetu ichakatwe hapa hapa nchini ili thamani yake iongezeke," alieleza Justine.

Alikumbusha kwamba kiwanda kama hicho kipo toka 1963, na kuongeza kwamba kikiendelezwa kahawa ya Tanzania itapanda thamani itawavutia wanunuzi wa ndani na nje, na kuwafanya Watanzania kutumia kahawa iliyotengenezwa hapa hapa nchini.

Amesema kwa sababu ya juhudi ya pamoja ya msimu uliopita kahawa imezalishwa kwa wingi na imekuwa na ubora unaotakiwa katika soko na kusema ni muhimu sasa kujikita katika kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata kahawa ili kuiongezea thamani na kuifanya kahawa ya Tanzania kuwa ya ushindani katika masoko ya nje.

"Tunaendelea kutekeleza kwa vitendo azima ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Na hili limejidhihirisha kupitia mafanikio yanayoonekana kwa wakulima," alisema Justine. Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliishukuru benki hiyo kwa ushirikiano ambao amesema umeleta mafanikio katika kuboresha na kukuza uzalishaji wa zao la kahawa mkoani Kagera.

"Mkoa utaendelea kutoa ushirikiano katika uamuzi wa TADB wa kukiendeleza kiwanda cha Tanica jambo hili litachochea ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira kwa vijana," alisema Gaguti.

Alisema azima ya serikali ni kujenga viwanda nchini, hivyo kwa kukiendeleza kiwanda cha Tanica kunaonyesha agizo la serikali kujenga viwanda limefanyiwa kazi na watendaji wake.

## Uturuki, China wapanua uhusiano licha ya tofauti za kisiasa

**BEIJING, China**

UTURUKI na China zimepanua ushirikiano wao, lakini uhusiano baina ya nchi hizo bado unakabiliwa na hali ya kutoaminiana pamoja na ushindani.

Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan ameanza ziara yake mjini Beijing jana na kukutana na mwenzake wa China, Xi Jinping.

Mataifa hayo mawili yana nia ya kukuza ushirikiano wao kiuchumi na kisiasa wakati wakipitia kipindi kigumu katika mahusiano yao na Marekani.

Uhusiano wa Uturuki na Marekani pamoja na washirika wake wa Mataifa ya Magharibi umezidi kuingia doa kufuatia tofauti zao katika mgogoro wa Syria.

Kuharibika kwa uhusiano huo kumezua hisia kutoka kwa baadhi ya waangalizi kuwa Uturuki, ambaye ni mwanachama wa Jumuiya ya kujihami (NATO) huenda ikawa inapanga mikakati ya kuelekeza uhusiano wake kutoka Magharibi kuelekea Mashariki.

Hata hivyo, wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema mkutano huu wa nane na Rais XI tangu mwaka 2012, unahusu zaidi uchumi na kupanua uhusiano wao, lakini sio sehemu ya mpango wa kimkakati wa kuegemea upande wa Mashariki.

"Uhusiano wa Uturuki na China hauwezi ukachukua nafasi ya ushirikiano wa taifa hilo na Marekani au na Umoja wa Ulaya, Uturuki ina uhusiano mkubwa na ulio na faida na mataifa ya Magharibi," alisema Altay Atli ambaye ni mhadhiri katika chuo kikuu cha Koc mjini Istanbul aliyebobea katika masuala ya uhusiano kati ya Uturuki na mataifa ya Asia.

Atli alieleza kuwa sera za kigeni za Uturuki zinalenga kuifanya nchi hiyo kuwa na ushawishi kimataifa na kupanua uhusiano wake na mataifa yote, tofauti na hali ilivyokuwa katika vita baridi ikiwa imejisogeza zaidi upande wa Magharibi.

Alisema kati ya mambo ambayo China na Uturuki wanatofautiana ni mgogoro wa wenyewe kwa wenyewe wa Syria, ambapo Uturuki inaunga mkono upinzani na China imekuwa ikiiunga mkono serikali ya Assad kiuchumi na kisiasa.

***DW***

# Mwili wa mzamiaji waanguka kutoka kwenye ndege

**LONDON, Uingereza**

MWILI wa mtu anayedhaniwa kuzamia kwenye ndege ya Shirika la Kenya Airways umeanguka wakati ndege hiyo ikitua katika Uwanja wa Ndege wa Heathrow jijini London.

Mwili huo ambao ni wa mwanaume ulipatikana katika bustani ya Clapham ukiwa umedondoka kutoka katika ndege hiyo.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi mjini London Uingereza imeeleza kuwa mtu huyo alianguka kutoka kwenye ndege ya Kenya Airways iliyokuwa ikisafiri kutoka mjini Nairobi.

Imeeleza mtu huyo alikuwa amebeba mkoba, maji na vyakula abavyo vilipatikana katika eneo lililo chini ya gia, linapokaa tairi.

Polisi wa Jiji la London wameeleza kuwa mwili huo utafanyiwa uchunguzi kubaini kilichosababisha kifo chake.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Ndege la Kenya Airways ilieleza kuwa ndege hiyo imefanyiwa uchunguzi na hakuna hitilafu yoyote iliyoripotiwa.

Msemaji wa Shirika hilo la ndege alisema: "Ndege hii huchukua saa 8 na dakika 50 kukamilisha safari yake. Inasikitisha kuwa mtu alipoteza uhai wake baada ya kuingia kwenye ndege yetu kisiri".

"Kenya Airways inashirikiana na mamlaka husika mjini Nairobi na London katika uchunguzi wa tukio hili."

Sio mara ya kwanza kifo kama hicho kuripotiwa katika ndege inayoelekea Uwanja wa Kimataifa wa Heathrow.

Juni, 2015, mtu mmoja alikutwa amefariki katika paa la makao makuu ya Notonthehighstreet.com katika barabara ya Kew Road, Richmond, huku mwingine akipatikana katika hali mahututi baada ya kuning'inia katika ndege ya British Airways kutoka mjini Johannesburg Afrika Kusini.

Agosti, 2012, mwili wa mwanamume ulipatikana kwenye buti ya ndege iliyokuwa ikitoka mjini Cape Town Afrika Kusini, ilipotua katika Uwanja wa Kimataifa wa Heathrow.

***BBC***



Polisi katika Mji Mkuu wa Kinshasa nchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo wakiwatawanya wanachama wa upinzani waliokuwa wakifanya maandamano. **PICHA: REUTERS**

# Sudan si salama kwazidi kutokota

**KHARTOUM, Sudan**

UMOJA wa Falme za Kiarabu umezitolea wito pande zinazozozana nchini Sudan kuendelea na mazungumzo, kujizuia na machafuko baada ya viongozi wa waandamanaji kuitisha kampeni ya siku moja ya uasi wa kiraia.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Anwar Gargash aliandika kwenye ukurasa wa mtandao wa Twitter akisema ni muhimu kwa Sudan kuendeleza mazungumzo yatakayosababisha kupatikana kwa makubaliano ya mpito, lakini pia kujiepusha na machafuko.

Alisema mabadiliko yoyote yatapaswa kuhakikisha kunaanzishwa mfumo thabiti wa kikatiba.

Viongozi wa waandamanaji nchini humo juzi waliitisha kampeni hiyo ya uasi wa kiraia kwa nchi nzima ifikapo Julai 14, ikiwa ni siku moja baada ya kuandaa maandamano makubwa dhidi ya baraza tawala la kijeshi lililochukua mamlaka, baada ya kuondolewa madarakani aliyekuwa Rais wa nchi hiyo Omar Al-Bashir, Aprili mwaka huu.

Kulingana na viongozi wa waandamanaji, hatua zaidi za kuongeza shinikizo dhidi ya baraza hilo la kijeshi kukabidhi madaraka kwa utawala wa kiraia, zinatarajiwa kuchochewa na maandamano Julai 13. Viongozi hao wameitisha uasi wa kiraia ifikapo Julai 14, katika tangazo walilolitoa juzi, siku moja baada ya kuandaa maandamano makubwa ya kulipinga baraza hilo la kijeshi, lililoitumbukiza nchi hiyo kwenye mzozo mkubwa wa kisiasa.

Kiongozi wa muungano wa uhuru na mabadiliko, Shareef Othman alinukuliwa akisema: "Jumamosi ya tarehe 13 kutakuwa na maandamano ya Melloni na maandamano haya yatakuwa ni kwa ajili ya mauaji ya kikatili ya Arbainia na kukabidhiwa mamlaka ya kiraia katika maeneo ya Sudan, katika mji mkuu na vijiji vya Sudan".

"Jumapili ya Julai 14, itakuwa siku ya uasi wa kiraia na mgomo mkubwa wa kisiasa katika sekta zote za kitaaluma katika mji mkuu na maeneo mengine pamoja na maandamano nje ya Sudan".

Wito wa kampeni hiyo unakuja katika wakati pande hizo mbili zinazozozana zikilaumiana kwa machafuko wakati wa maandamano makubwa yaliyofanyika siku ya Jumapili na kusababisha vifo vya watu 10 na mamia kujeruhiwa.

Maelfu ya wananchi waliandamana katika mitaa ya Mji Mkuu Khartoum na maeneo mengine yakiwa ni maandamano makubwa kufanyika tangu vikosi vya usalama vilipowatawanya waandamanaji waliokuwa wamekusanyika mbele ya jengo la Wizara ya Ulinzi, mwezi uliopita.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, Stephane Dujarric alisema katibu mkuu huyo ameitolea wito kwa mara nyingine Sudan kwa kuzitaka pande zote mbili kurejea kwenye mazungumzo ya kisiasa, ili kuundwa kwa serikali ya mpito haraka, lakini pia ametaka kuchukuliwa hatua kwa wahusika wa mauaji yaliyotokea juzi.

Marekani imelaani matumizi ya risasi za moto dhidi ya waandamanaji, na kusema utawala wa kijeshi unapaswa kuwajibika kwa mauaji ya raia.

***DW***

# Ongangi apatikana Mombasa

## Ni siku 9 baada ya kutoweka

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA wa Kenya, Raphael Ongangi anayedaiwa kutekwa nyara nchini amepatikana mjini Mombasa zikiwa zimepita siku tisa tangu atoweke.

Ongangi anadaiwa kutekwa Jumatatu ya Juni 24, usiku katika mtaa wa Oysterbay jijini Dar es Salaam na watu wenye silaha akiwa na mke wake Veronica Kundya.

Msemaji wa Chama cha ACT -Wazalendo, Ado Shaibu, alithibitisha kupatikana kwa mfanyabiashara huyo jana lakini akasema mke wake ndiye atakayetoa taarifa zaidi.

Mke wa mfanyabiashara huyo Veronica hakupatikana kwa njia ya simu, lakini aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kuwa anafurahi sana kushuhudia ukuu wa Mungu kwani mume wake amepatikana mjini Mombasa akiwa salama.

"Namshukuru Mungu sana sina mengi ya kusema zaidi ya kushukuru kwa kuwa yeye ni Mungu wa miujiza maana ametenda, nawashukuru wote kwa niaba ya familia yangu kwa sala na kwa kujitolea kwenu katika kipindi hiki kigumu," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa zilizoripotiwa na vyombo vya habari nchini Kenya na Tanzania, watu wasiojulikana waliwafuatilia wanandoa hao na kisha kulizuia gari lao na kumchukua mfanyabiashara huyo na kuondoka naye.

Awali, Veronica alisema aliamriwa na watu hao ambao alidai walijitambulisha kama maofisa wa usalama kuwa asiseme chochote mpaka atakapotaarifiwa nao.

Taarifa zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zinaripoti kuwa Ongangi aliingia Tanzania mwanzoni mwa miaka ya 2002 kwa masomo ya elimu ya juu katika moja ya vyuo vikuu nchini humo.

Ilielezwa kuwa baada ya masomo alibaki nchini na kuanza biashara na inaripotiwa kuwa ana miliki na kuendesha biashara ya kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Rwanda, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Tukio la Ongangi kutekwa lilichukua sura mpya baada ya Kiongozi wa chama cha upinzani cha ACT-Wazalendo Zitto Kabwe kuhusisha kushikiliwa kwake mateka na kudukuliwa kwa mitandao yake ya kijamii.

Zitto aliwaambia waandishi jijini Dodoma wiki iliyopita kuwa waliomteka Ongangi walidukua mitandao yake ya kijamii.

Uongozi wa ACT-Wazalendo baadaye ulitoa taarifa kuwa mfanyabiashara huyo alihusika kwa kiasi kikubwa katika kufunguliwa kwa mitandao hiyo na ndiye mtu pekee ambaye alikuwa na nywila (pasword) mbalimbali na Zitto mwenyewe.

Zitto ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini kwa tiketi ya ACT -Wazalendo, juzi alizungumza na waandishi wa habari na kuitaka serikali ichukue hatua kuhusu tukio hilo huku polisi wao wakisema wamepata taarifa za madai ya kutekwa mfanyabiashara huyo na wanazifanyia kazi. Alipotafutwa kuzungumzia suala hilo juzi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Musa Taibu alikiri kupokea taarifa kutoka kwa Zitto kuhusu sehemu anayohisi kuwa huenda Raphael anashikiliwa.

Oktoba 11, mwaka jana saa 11 alfajiri mfanyabiashara maarufu Mohamed Dewji maarufu kama MO alitekwa na watu wasiojulikana kwenye hoteli ya Colosseum Oysterbay jijini alikokuwa anakwenda kufanya mazoezi .

MO alipatikana akiwa hai zikiwa zimepita siku tisa na alikuwa ametelekezwa ndani ya gari maeneo ya Gymkhana.




Meneja Uhusiano wa Airtel Tanzania, Jackson Mmbando, akiongea na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa ofa maalum kupitia Samsung A10 na A2 core inayolenga kuwafaidisha wateja wake katika msimu huu wa Sabasaba ambapo mteja atapata intaneti ya bure ya 36GB kwa muda wa miezi 12. Kulia ni Meneja wa Huduma za Smartphone wa kampuni hiyo, Nicky Mlelwa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wauza ramani holela mitaani waonywa

**Na Grace Semfuko,** MAELEZO

BODI ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) imewataka wafanyabiashara wa ramani za majengo nchini kuacha kuuza ramani hizo mara moja kwa kuwa zimekuwa chanzo cha ujenzi usiozingatia viwango vya ubora.

Pia imesema kumekuwa na matatizo ya kuporomoka kwa majengo, nyumba kuwa na nyufa na ujenzi unaoziba miundombinu mingine hali inayotokana na wenye nyumba wengi kutofuata sheria za ujenzi.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Ludigija Bulamile, alisema watu wanaouza ramani hawaangalii wala kupima viwango vya ujenzi unaotakiwa mahali husika.

"Wauza ramani wote nchini waache mara moja, hawana utaalamu wa kumshauri mtu kuhusiana na jengo linalohusika. Wanauza ramani ovyo watu nao wananunua tu. Hii inasababisha nyumba nyingi kupata nyufa na kubomoka, hivyo kuhatarisha maisha ya watu," alisema Dk. Lidigija.

Alisema kuna maeneo hayaruhusiwi kujenga nyumba za ghorofa au nyumba kubwa kutokana na ardhi iliyopo na wakati mwingine ardhi zinakuwa na maji, hivyo kuhitaji msingi mkubwa na mchanganyiko wa zege imara lakini watu wananunua na kujenga kwenye maeneo hayo bila kuzingatia athari zinazoweza kutokea.

"Nawashauri wakati wa kujenga watu watumie wataalamu waliosomea fani ya ubunifu na ukadiriaji majenzi ili kuepukana na hasara ya kujenga nyumba mara mbili. Unajua usipotumia wataalamu hawa eti unasema unaokoa gharama matokeo yake unajikuta unatumia gharama mara mbili zaidi kwani yanabomoka au wanapindisha nyumba, hawazingatii viwango na mchangayiko mzuri wa nyenzo za ujenzi" alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Geraldine Kikwasi, alisema wakadiriaji majenzi wamekuwa na mchango mkubwa kuhakikisha majengo yanakuwa imara, hivyo kuwaomba Watanzania kuwatumia ili kuimarisha sekta hiyo.

# Takukuru yazuia mali za watuhumiwa wa KCBL

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Kilimanjaro, imetangaza 'kuzizuia' mali za watuhumiwa wawili wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) wanaotafutwa kwa kujihusisha na mazao ya uhalifu ikiwamo kumiliki mali za kufuru kama nyumba za kifahari na magari maeneo mbalimbali.

Wanaotafutwa ni aliyewahi kuwa Meneja Mkuu wa benki hiyo, Joseph Kingazi na aliyekuwa Mhasibu wa benki hiyo, Ombeni Masaidi.

Taarifa ya kuwataka wananchi wa Moshi na miji ya jirani kutojihusisha na mazao ya uhalifu yanayotokana na watuhumiwa hao imetolewa jana na Mkuu wa Takukuru, mkoani Kilimanjaro, Holle Makungu.

Mali zinazomilikiwa na Kingazi ni pamoja na nyumba za kifahari zilizoko katika kiwanja namba 204 kilichopo Kitalu GGB, barabara ya Arusha, nyumba katika kiwanja namba 345 GG barabara ya Arusha, nyumba mbili zilizopo eneo la Olasiti Arusha na nyumba ya kifahari iliyoko Barabara ya Moshi – Arusha eneo la kwa Mrefu.

Mali nyingine ziko katika Kiwanja namba 437 kitalu HHHA sehemu III Mtaa wa Khambaita, Manispaa ya Moshi, mali zilizopo kwenye viwanja namba 1312, Kitalu 'A' Ngarenairobi Wilaya ya Siha na kiwanja namba 1998 kilichoko Kitalu 'B' Wilaya ya Siha.

Aidha, zimo nyumba katika Kiwanja namba 925, Kitalu 'A' Wilaya ya Siha, kiwanja namba 908 kitalu 'A' Wilaya ya Siha, kiwanja namba 1025, kitalu 'A' Wilaya ya Siha, kiwanja namba 908 'N'1 na 2 iliyoko kitalu 'N' station Same.

Nyumba nyingine za Kingazi ziko Soni-Mponde Tanga, magari T706 DCL Toyota Spacio, T795 WRSuzuki Escudo, T 936 CMC Volkswagen Touran, T604 DKY Toyota IST na Pikipiki MCA 490 AAZ.



# BENITEZ

## KOCHA MPYA DALIAN YIFANG YA CHINA

**BEIJING, China**

RAFAEL Benitez ameteuliwa kuwa Kocha wa Klabu ya Ligi Kuu ya China, Super League, Dalian Yifang.

Mhispania huyo alimaliza mkataba wake na Newcastle Jumapili, huku Benitez akisema kwamba aliamua kuachana na klabu hiyo kwa sababu haina mtazamo wa kutafuta mafanikio zaidi.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 59, aliposti video kwenye ukusara wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter akisema kwamba jana Jumanne amejiunga na Klabu ya Dalian.

Katika video hiyo fupi, kocha huyo wa zamani wa Liverpool na Real Madrid 'alishea' ujumbe wa kumkaribisha kwenye klabu hiyo uliosomeka: "Karibu Rafa Benitez: Changamoto mpya, ukurasa mpya.

Halafu yeye akaandika: "Baada ya safari ndefu, naanza tena changamoto mpya. Nina furaha kuanza mradi mpya na Da-



# RAIS WA LA LIGA HATAKI NEYMAR ARUDI HISPANIA

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Javier Tebas amesema hataki Neymar achezee klabu ya nchini humo kwa sababu tabia yake nje ya uwanja si nzuri kwa mashindano hayo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliondoka Barcelona miaka miwili iliyopita kwenda kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Paris Saint-Germain kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222 na ameripotiwa kwamba anataka kurudi tena kujiunga na mabingwa hao wa Hispania kipindi hiki cha msimu wa majira ya joto.

"Mara zote tunapenda kuwa na wachezaji wakubwa na makocha wa kiwango cha juu kwenye Ligi Kuu ya La Liga, kwa ajili ya ubora wa mashindano," alisema Tebas akiiambia redio Onda Cero.

Akaongeza kusema: "Kwa upande wa Neymar, kwa mtazamo wangu tabia yake nje ya uwanja sidhani kama ni nzuri kwa mashindano yetu."

Neymar mwenye umri wa miaka 27, alifungiwa mechi tatu kufuatia kumpiga ngumi shabiki wa Rennes baada ya PSG kufungwa kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa Mei mwaka huu.

"Mwisho wa siku, habari inakuja kuhusu mchezaji huyu kwamba kafanya vile au hivi, hiyo si nzuri kwa ligi yetu," alisema Tebas.

"Tumefanya kazi kubwa mno kuijenga thamani na taswira ya La Liga, na tunataka hilo liendelee."


# Sanchez aibuka atupa dongo

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Alexis Sanchez ameibuka na kuwabeza wale wote wanaohoji kiwango chake akiwa anaichezea klabu yake ya pale Old Trafford.

Sanchez tangu ajiunge na Man United akitoka Arsenal kipindi cha majira ya baridi, kiwango chake kimekuwa si cha kuvutia, huku muda mwingine akitumia akiwa benchi kutokana na majeraha.

Lakini kwa sasa nyota huyo ameonekana kuwa kwenye kiwango bora wakati akiichezea nchi yake ya Chile kwenye michuano ya Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, yanayoendelea nchini Brazil.




Alexis ameonyesha kiwango cha maana akiwa na kikosi chake cha Chile na ameifikisha timu katika hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Mchezaji huyo ni miongoni mwa nyota wa Chile ambao walipata penalti walipoingia muda wa matuta na Colombia kisha kuibuka kwa ushindi wa penalti 5-4 mwishoni mwa wiki.

Katika siku za karibuni, mchezaji huyo amekuwa akizomewa kwa kufanya vibaya katika ngazi ya klabu.

Sanchez aliposti picha katika mitandao ya kijamii ikimwonyesha anashangilia huku akiwa kifua wazi na kusema; "Wanaongea upuuzi juu yangu, tazameni kiwango changu."

## HABARI MICHEZO




# GRIEZMANN

## ACHELEWESHA USAJILI WA FELIX ATLETICO

**MADRID, Hispania**

USAJILI wa Atletico Madrid wa euro milioni 126 kwa mshambuliaji, Joao Felix kutoka Benfica umesubirishwa kwanza wakiwa wanasubiri kupata euro milioni 120 kwa mauzo ya Antoine Griezmann, kwa mujibu wa ESPN FC.

Benfica ilithibitisha wiki iliyopita kwamba, Atletico wamekubali kutoa ofa kubwa kwa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ureno, ambaye atakuwa mchezaji wa tano kwenye historia ya Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, kununuliwa kwa bei kubwa zaidi.

ESPN FC imeripoti kwamba, kwa sasa Atletico na Benfica wameshakubaliana pamoja na maslahi binafsi ya mchezaji mwenyewe na kwa sasa wanasubiria tu uhamisho huo kukamilika.

Wakati huo huo, majaliwa ya Griezmann bado hayajulikani, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa akiwa tayari alishawaambia Atletico ataondoka mwishoni mwa msimu uliopita.

"Bado tunamsubiria Griezmann, kwani yeye mwenyewe alituambia hatakaa na sisi msimu ujao," kilisema chanzo kimoja kutoka klabuni hapo kikinukuliwa na ESPN FC.

Na taarifa zaidi zinaeleza kuwa, hadi sasa hakuna klabu yoyote iliyofanya mawasiliano ya kutaka kumnunua Griezmann.

Griezmann anatarajiwa kuhamia pale Camp Nou, na kwa mujibu wa ESPN FC, Barca kwa sasa wanakamilisha taratibu za malipo kwa ajili ya mchezaji huyo ambaye anaweza kutangazwa kuwa mchezaji wao wiki hii.

# Andy Ruiz Jr atamba atamchapa tena Joshua

**NEW YORK, Marekani**

BINGWA wa masumbwi duniani kwa uzito wa juu, Andy Ruiz Jr, amemtambia Anthony Joshua kwa kusema kuwa si bondia mzuri akiwa ulingoni na hata wakirudiana atamchapa tena.

Ruiz Jr, ambaye ni bondia kibonge, amesema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kuwapo tetesi kuwa wawili hao wanataka kuzichapa kwa mara nyingine.

"Nishajua makosa yake, naweza kufanya kitu bora zaidi, kitu pekee anachoweza yeye ni kukimbiakimbia uwanjani, si mzuri akiwa ulingoni tukirudiana itakuwa vilevile, lazima nimchape tena," alisema Ruiz Jr.

Aidha, Andy Ruiz Jr, amepata umaarufu mkubwa sana baada ya kumchapa bondia, Joshua katika raundi ya saba katika mchezo uliopigwa Juni Mosi, mwaka huu.

Hata hivyo, promota wa Joshua, amesema kuwa wawili hao wanaweza kuzichapa tena Novemba 16 au Desemba 14, mwaka huu.



## LAMPARD AANZA KUAGWA DERBY

**LONDON, England**

KLABU ya Derby imemruhusu kocha wake, Frank Lampard asihudhurie mazoezi ya kabla ya msimu kuanza, wakati klabu hiyo ikimtarajia kupata nafasi ya kukifundisha kikosi cha Chelsea.

Lampard hakuwapo kwenye mazoezi juzi, Jumatatu na jana Jumanne wakati mazungumzo yakiendea na Klabu ya Chelsea, ambayo aliichezea kwa miaka 13.

Derby ilifanya maamuzi, hivyo uhamisho huo utakamilika haraka iwezekenavyo kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail.

Kama Lampard ataondoka, Derby inategemea kutangaza atakayechukua nafasi yake mwishoni mwa juma.

Hata kocha msaidizi, Jody Morris pia hakuwapo kwenye mazoezi hayo na kuna hisia kuwa atahamia Chelsea pamoja na Lampard.

Kiungo huyo wa zamani wa England atamrithi Maurizio Sarri, ambaye ameondoka Stamford Bridge na kujiunga na Juventus mwezi uliopita.

Wachezaji wa Derby walifanyiwa vipimo vya afya, hivyo klabu inaona kuwa itakuwa inaendelea na majukumu yake bila kuwa na kiongozi.

Kikosi hicho kinatarajia kusafiri kwenda Florida nchini Marekani kwa ajili ya kambi ya mazoezi kesho, Alhamisi.

Taarifa ya Derby iliyotolewa Jumatatu, ilieleza: "Siku chache za mwanzo za kabla ya msimu kuanza wataanza na mazoezi ya viungo na wataendelea kwa kuzingatia mwongozo wa wataalamu wa viungo, kitabibu na sayansi ya michezo."

Nahodha wa zamani wa Chelsea, John Terry kwa sasa kocha msaidizi wa Aston Villa, amesema hakuna mwenye uwezo wa kuiongoza Chelsea isipokuwa mchezaji mwenzake huyo wa zamani.

Lampard aliichezea 'Blues' mara 648, na kushinda makombe 11 na kikosi hicho, baada ya kujiunga akitokea klabu yake ya utotoni ya West Ham kwa kitita cha pauni milioni 11 mwaka 2001.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAMFUATA ZAHA NA OFA KIDUCHU

Kaka yake atoa matumaini ya kutua Emirates kutokana na kazi kubwa aliyoifanyia klabu hiyo huku...

**LONDON, England**

Arsenal imewasilisha ofa ya wazi ya takriban pauni milioni 40 kwa mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha.

Lakini hakuna wachezaji waliotolewa kama sehemu ya mpango uliopendekezwa wa kuuzwa, na ofa hiyo ya Arsenal itakataliwa na Palace.

Zaha, 26, yupo tayari kuondoka klabuni hapo majira haya ya joto na anatoa nafasi zaidi ya kujiunga na Arsenal, lakini 'Eagles' hao wanamthaminisha nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast na zaidi ya pauni milioni 80.

Hata hivyo, 'The Gunners' watakuwa wakitumai kufanyika maelewano ili kufikia dau hilo la chini na kulipa.

Bajeti ya usajili ya Arsenal majira haya ya joto imeshushwa kutokana na kushindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Baada ya kushindwa kufanikiwa kurudi Manchester United, Zaha alijifunga jumla Palace mwaka 2015 na ana miaka minne imebaki katika mkataba wake, ambao alisaini majira ya joto yaliyopita.

Tangu alipoisaidia Palace kurejea tena Ligi Kuu msimu wa 2012-13, wameweza kufanikiwa kumaliza katikati ya msimamo wa ligi mara moja tu, wakishika nafasi ya 10 msimu wa 2014-15, wakati Zaha aliporejea kwa mkopo wa muda mrefu akitokea United.

Kaka yake Zaha, Judicael, aliiambia Sky Sports News: "Kutokana na yote ambayo Wilfried amewapa Crystal Palace kuwasaidia kubaki Ligi Kuu, natumai Palace itaweza kuona njia ya kukubaliana na Arsenal ambayo itamruhusu Wilfried kutimiza ndoto yake ya kuichezea klabu ya Ulaya aliyokuwa akiipenda tangu utotoni. "

Zaha kwa sasa yupo na timu yake ya Taifa, Ivory Coast kwenye fainali za Mataifa ya Africa (Afcon) na juzi aliiwezesha kutinga hatua ya 16-bora ya michuano hiyo.

## KWA UFUPI

**UNITED YAKWAMA KWA FERNANDES**

Manchester United imekataliwa ofa yao ya pauni milioni 31 kwa kiungo Mreno Bruno Fernandes, 24, anayeichezea Sporting Lisbon. ***(Gazzetta dello Sport, via Express)***

**SOLSKJAER AMTAKA LONGSTAFF**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ameueleza uongozi wa klabu hiyo kuhakikisha wanaipata saini ya kiungo wa Newcastle United, Muingereza Sean Longstaff, 21, kwa dau la pauni milioni 25 wiki hiki. ***(Star)***

**ARSENAL YAITIWA FEKIR**

ARSENAL imepewa ofa ya kuinasa saini ya mshambuliaji wa Lyon na Ufaransa, Nabil Fekir, 25, amabaye alikuwa akilindwa Liverpool - kwa takriban pauni milioni 30 tu. ***(Mirror)***

**VIEIRA AITOLEA NJE NEWCASTLE**

NYOTA wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa, Patrick Vieira anaonekana kukataa mwenyewe kwenda kuinoa Newcastle baada ya kueleza kuwa bado ana lengo la kuendelea kuinoa Nice kwa "muda mrefu". ***(Mail)***

**ARSENAL, BRAHIMI WAJICHIMBIA**

Arsenal ipo katika mazungumzo na kiungo mshambuliaji, Mualgeria Yacine Brahimi, 29, ambaye yupo huru baada ya kuondoka Porto. ***(Sky Sports)***

**SANE HAKIELEWEKE KUTU BAYERN**

WINGA wa Manchester City, Mjerumani Leroy Sane, amekuwa miongoni mwa wachezaji waliotumika kutangaza jezi mpya za msimu wa 2019-20 za klabu hiyo licha ya kuhusishwa na kujiunga na Bayern Munich. ***(Express)***

**SAFARI YA NEYMAR BARCA YAANZA**

WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa Paris St-Germain, Neymar, 27, jana walikuwa wakijiandaa kukutana rasmi na uongozi wa Barcelona kujadili uwezekano wa nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kurudi kwa mabaingwa hao wa Hispania. ***(Esporte Interativo, via Mail)***

**GRIEZMANN ASHUSHWA BEI SOKONI**

DAU la kuvunja mkataba wa mshambuliji wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann, 28, limeshuka kutoka pauni milioni 179 hadi pauni milioni 107 na sasa Barcelona ipo tayari kuinasa saini ya nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa. ***(Star)***

**BENITEZ KUIBUKIA UPYA CHINA**

KOCHA wa zamani wa Newcastle, Rafael Benitez, amekubali kuwa kocha mpya wa Klabu ya Dalian Yifang ya China kwa mkataba utakaomwezesha kuvuna pauni milioni 12 kwa mwaka baada ya kuondoka St James' Park. ***(Sky Sports)***

**LOVREN, MILAN WATETA RASMI**

WAWAKILISHI wa beki wa kati wa Liverpool, Dejan Lovren, 29, wamefanya mazungumzo rasmi na AC Milan kuhusu uwezekano wa nyota huyo wa kimataifa wa Croatia kujiunga nao. ***(Mirror)***

**LAMPARD, CHELSEA WAKUBALIANA**

DILI la kocha wa Derby County, Frank Lampard kurudi Chelsea lilifanyika Jumatatu na kiungo huyo wa zamani wa 'Blues' amekubali kulipwa pauni milioni nne kwa mwaka huku kukiwa na motisha wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

**POGBA AJIFUA KIVYAKE NEW YORK**

KIUNGO Mfaransa Paul Pogba, 26, amekuwa akifanya mazoezi mwenyewe jijini New York, Marekani wakati wachezaji wenzake wa Manchester United wakiripotiwa kurudi kujiandaa na msimu mpya. ***(Sun)***

**MARTINEZ AUNDIWA MKAKATI BARCA**

Barcelona ipo tayari kulipa pauni milioni 100, zinazohitajika ili kuvunja mkataba wa straika wa Inter Milan, Muargentina Lautaro Martinez, 21. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

## HABARI MICHEZO

## Viwanja vya soka Z'bar intaneti bure

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF) limeingia mkataba na Kampuni ya Zanlink wa upatikanaji wa huduma za mtandao wa intaneti katika viwanja vya soka visiwani hapa.

Mkataba huo wa mwaka mmoja kwa kuanzia ulitiwa saini jana na Meneja Masoko wa Zanlink, Joseph Albert na Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu katika ofisi za Zanlik zilizoko Majestik mjini hapa.

Akizungumza katika hafla hiyo ya utiaji saini, Albert alisema wameamua kudhamini huduma hiyo kwa lengo la kuona kwamba tasnia ya soka inatangazika.

Alisema Zanlink itatoa huduma hizo katika viwanja vitatu vikubwa vinavyotumika kuchezea soka ikiwamo Uwanja wa Mao, Amani na Gombani kwa siku ambazo kutakuwa na mechi zinazosimamiwa na ZFF.

Hata hivyo, alisema huduma hiyo itatolewa wakati ambao mpira unachezwa na kutoa wito kwa taasisi nyingine kuamka na kushiriki kwenye kuliwezesha shirikisho hilo ili kusaidia mpira wa miguu Zanzibar.

## Machomane kuwasha moto Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Machomane kutoka kisiwani Pemba imeungana na Kipanga ya Unguja kucheza Ligi Kuu ya Zanzibar katika msimu mpya unaotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

Machomane ambayo imepanda daraja baada ya kushinda michezo yake ya mwisho na kufikisha alama 62, hivyo kumpiku mpinzani wake wa karibu, Young Island iliyomaliza na alama 56 na kushika nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba.

Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba ilishindwa kumalizika kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali ambazo hazikuweza kuepukika kwa wakati huo ikiwa ni pamoja na kupisha mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao ulisababisha ligi zote kusimamishwa.

Kuelekea msimu mpya, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussen Ahmada, ameitaka timu ya Machomane ambayo itacheza Ligi Kuu kuhakikisha inafanya usajili kwa wakati husika ni wakati huu dirisha likiwa wazi.

Katika ligi hiyo ya Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba, timu nne zimeshuka daraja ambazo ni Ziwani iliyomaliza nafasi ya 13 ikiwa na alama 28, Mantar ambayo ina pointi 27 ikiwa nafasi ya 14, Cossovo (pointi 20) ikiwa nafasi 15 na Bungo iliyoburuza mkia ikiwa na pointi 14.

# TAIFA STARS KUREJEA KESHO, KUIVAA SUDAN

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupoteza michezo yake yote mitatu kwenye michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, inayoendelea nchini Misri, timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) inatarajia kuwasili kesho ikitokea nchini humo tayari kuanza maandalizi ya kuwania kufuzu mashindano ya wachezaji wanaocheza Ligi za Ndani barani Afrika (CHAN) dhidi ya Sudan.

**Taifa Stars imepoteza mechi zote tatu za Kundi C, kufuatia kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Senegal na kisha kuchapwa 3-2 dhidi ya Kenya (Harambee Stars) kabla ya kuhitimisha kwa kulala 3-0 dhidi ya Algeria.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana, makao makuu ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ofisa Habari wa shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, timu hiyo itaondoka nchini Misri leo usiku moja kwa moja kabla ya kuwasili nchini kesho.

"Tunasikitika timu yetu ya taifa imepoteza tena mchezo wake wa jana, watawasili hapa nchini keshokutwa (kesho) mchana, tunaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi kuipokea timu yetu ambayo ilikuwa inaitangaza nchi yetu Misri," alisema Ndimbo.

Aliongeza kuwa wachezaji ambao walitumika katika michuano ya Afcon kuna uwezekano mkubwa wakatumika kwenye michuano ya CHAN isipokuwa wale wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi na kuwataka Watanzania wazidi kumpa kocha, Emmanuel Amunike ushirikiano.

"Nafikiri wale wachezaji ambao walitumika kwenye mashindano ya Afcon mwalimu anaweza kuwapendekeza wakacheza katika mashindano ya CHAN ispokuwa kwa wale wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi," alisema msemaji huyo.

Aidha, aliwataka Watanzania kuwa na subira licha ya timu yao kupata matokeo hayo na badala yake wasubiri mwalimu atakaporudi atatoa tathmini nzima ya mashindano ilivyokuwa katika michezo yote aliyocheza ikiwa ni pamoja na kuzungumzia mapungufu ya kila mchezaji.

Katika mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki michuano ya CHAN inayotarajiwa kufanyika Januari mwakani nchini Cameroon, Taifa Stars inatarajiwa kuanzia nyumbani dhidi ya Sudan Julai 26, mwaka huu.

Cameroon imepewa nafasi ya kuandaa michuano hiyo baada ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kuinyang'anya Ethiopia wenyeji huo Aprili mwaka huu.



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akibanwa na mabeki wa Algeria kwenye mechi ya Afcon iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Al Salaam na timu hiyo ya Tanzania kuchapwa mabao 3-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Singida United yaahidi 'majembe' zaidi*

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Klabu ya Singida United umesema wanaamini msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakuwa mzuri kutokana na uimarishaji wa kikosi chao unaoendelea.

Singida United tayari wamefanya usajili wa wachezaji wanne kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu ujao na bado wameahidi kuongeza 'majembe' zaidi.

Kiongozi wa timu hiyo, Festo Sanga, jana alimwambia mwandishi wetu kuwa, wanachokifanya kwa sasa ni kukiimarisha kikosi chao kwa kuwasainisha wachezaji wenye uwezo wa juu.

"Kama viongozi, tunaendelea na taratibu za kukijenga kikosi chetu, tunaamini msimu ujao kwa hiki tunachokifanya tutafanya vizuri na kusahau msimu uliopita," alisema Sanga. Alisema bado wanaendelea na mchakato wa usajili ambapo hivi karibuni watatangaza wachezaji wengine watakaojiunga na timu hiyo.

Tayari dirisha la usajili Ligi Kuu Bara limefunguliwa na linatarajiwa kufungwa rasmi Julai 31, mwaka huu.

# Michezo

Jumatano Julai 3, 2019

Nipashe




Arsenal yamfuata Zaha na ofa kiduchu

UKURASA 30




Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori (kushoto), akimtambulisha Deo Kanda baada ya jana kumwaga wino wa mwaka mmoja kuitumikia klabu hiyo akitokea TP Mazembe. **PICHA: SIMBA**

## Amunike afunguka Stars kuaga Afcon

**Na Somoe Ng'itu,** CAIRO

TUMETOKA darasani! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, aliyoyatoa baada ya kikosi chake kupoteza mechi zote tatu za Kundi C katika fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019, zinazoendelea nchini Misri.

Kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Algeria katika mchezo uliochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Al Salaam kilihitimisha safari ya Taifa Stars Afcon na kuanza kurejea nyumbani Tanzania bila ya pointi baada ya awali kuchapwa 2-0 na Senegal na baadaye Kenya (Harambee Stars) kuwafunga 3-2.

Algeria iliongoza kundi hilo ikiwa na pointi tisa ikifuatiwa na Senegal wenye pointi sita wakati Harambee Stars wao wameondoka na pointi tatu na Taifa Stars ikiburuza mkia bila ya kupata pointi hata moja.

Akizungumza na gazeti hili, Amunike, alisema kuwa mchezo wa juzi ulikuwa ni wa kuvutia, lakini uzoefu mdogo wa wachezaji wake ulionekana baada ya kumalizika kwa dakika 30 kipindi cha kwanza cha mechi hiyo.

Amunike alisema kuwa timu yake ilitengeneza nafasi za kufunga, lakini wachezaji wake walishindwa kuzitumia nafasi hizo, huku wapinzani wao Algeria wakitumia makosa waliyofanya kupata mabao.

"Uzoefu ni jambo muhimu sana, hasa katika mashindano kama haya, katika mchezo wa soka unatakiwa kutumia vizuri kila nafasi moja utakayopata, maana wakati mwingine huja mara moja, tulipata nafasi lakini hatukuzitumia ipasavyo, na baadaye tukaadhibiwa," alisema Amunike.

Aliongeza kuwa mashindano ya mwaka huu kwake ameyachukuliwa kama sehemu ya kujifunza na anaamini katika fainali zijazo watakuwa wameimarika.

"Tumejifunza, mwaka 2019, kwetu tulikuwa katika mafunzo, yatatusaidia kuboresha vipaji vyetu," kocha huyo aliongeza. Mnigeria hiyo pia aliwatakiwa mafanikio Algeria katika hatua wanayokwenda kwa sababu hawakubahatisha kufika hapo.

# Simba yanasa winga 'teleza', Okwi agoma

**Na Mwandishi Wetu**

●●● Ni aliyebeba ubingwa wa Caf na kucheza Klabu Bingwa Dunia akiwa na TP Mazembe, wamwelezea kuwa...

HUKU ikiendelea kuhaha kuipata saini ya mshambuliaji wao, Mganda Emmanuel Okwi, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wametangaza rasmi kuingia mkataba wa mwaka mmoja na winga wa Kimataifa wa DR Congo, Deo Kanda Mukok, anayeaminika ni mkali wa 'kuteleza' na mpira akitokea pembeni kuingia kati.

Taarifa kupitia ukurasa wa Instagram wa Simba ikiambatana na mchezaji huyo akitia saini mkataba wake akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Crescentius Magori, ilieleza: "Kazi ya kusajili wakali watakaohakikisha kikosi cha mabingwa kinazidi kuwa tishio kwa wapinzani inaendelea. Mshambuliaji raia wa Congo DR, Deo Kanda (29), amejiunga na mabingwa wa nchi.

**"Kanda amesaini mkataba wa mwaka mmoja kukipiga Msimbazi akitokea TP Mazembe ambapo alikuwa mmoja wa wachezaji ambao waliiwezesha kushinda ubingwa wa Afrika mwaka 2009, 2010 (aliifungia bao kwenye mchezo wa fainali dhidi ya Esperance) na 2013, lakini pia akiwa ameshiriki Kombe la Dunia la Klabu mwaka 2009, 2010 na 2013. #Nguvu Moja."**

Kanda anakuwa mchezaji mpya wa tano wa kigeni kusainishwa kuichezea Simba msimu ujao baada ya Wabrazil watatu, mabeki Gerson Fraga Vieira kutoka ATK ya Ligi Kuu ya India na Tairone Santos da Silva kutoka Atletico Cearense FC, mshambuliaji Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino, zote za Daraja la Nne nchini Brazil na kiungo Msudan Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman (Al Hilal ya Sudan).

Kwa upande wa Okwi, kwa mujibu wa taarifa zilizolifikia Nipashe jana kutoka chanzo chetu cha uhakika ndani ya Simba, zimeeleza kuwa suala la kuipata saini ya nyota huyo wa kimataifa wa Uganda bado kuna mvutano mkubwa kutokana na kuhitaji dau kubwa.

"Ni kweli tunahitaji saini ya Okwi lakini anahitaji dau kubwa kiasi cha Sh. milioni 115 ili asaini mkataba wa mwaka mmoja, na amekiwa kupewa kiasi hicho lakini kwa mkataba wa miaka miwili jambo ambalo hataki kuliafiki.

"Yeye anataka kama ni miaka miwili apewe fedha zaidi ya hizo, jambo ambalo uongozi nao haujaafiki, ila subirini mambo yakiwa tayari mtafahamishwa," kilieleza chanzo chetu.

Okwi ambaye yupo nchini Misri kwenye Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019, na akiwa ameiwezesha timu yake ya Taifa ya Uganda kutinga hatua ya 16-bora, amemaliza mkataba na Simba na hataki kuingia mkataba mpya kwa sasa na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo wapo Misri kwa ajili ya kuendelea kuzungumza na nyota huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002